## Thou Shalt Call and I Will Answer

**Betty Burton Choate**

Oh, my Father, in the morning,
In the dawning of my days,
Thou shalt call and I will answer
With a song of ringing praise.

In the happy dreams of childhood,
In the years of growing joy,
Thou shalt call and I will answer,
In Thy work my hands employ.

Through the burning of the noonday
When I stumble in the heat,
Thou shalt call, oh loving Father,
And my tongue will answer Thee.

Though so weary from the burden
In the sultry afternoon,
Thou shalt call and I will answer
For my rest comes sure and soon.


Oh, my Father, in the sunset,
When the warmth dies with the light,
Thou shalt call and I will answer,
Unafraid to face the night.

Thou shalt call me through the darkness
When my work at last is done;
I will hear the wings of angels
Sent from Thee to bring me home.

Chorus:
Thou shalt call me, oh my Father,
Endless work there is to do;
Take my hands, my feet, and use them,
Let me live and die for You!

(Recorded hymn available at WorldEvangelism.org website)

THE VOICE OF TRUTH INTERNATIONAL
VOLUME 90



VOLUME NINETY

# THE VOICE OF TRUTH INTERNATIONAL

The close of God's beautiful day!

# The Voice of Truth International

Mawio ya siku nzuri ya Mungu!

Toleo la 90 (Volume 90)

Tafsiri, Ubunifu na Mpangilio
(Translation, Design and Layout)
**Shadrack S. Msambaza**
(Mshirika wa Kanisa la Kristo pia ni mwalimu na mhubiri wa Injili)

Mhariri
(Proof reading)
**Peter Kamatula**
(Mshirika wa Kanisa la Kristo pia ni mwalimu na mhubiri wa Injili)

Nakala hii kwa lugha ya Kiswahili imetolewa na ***Swahili Gospel Team*** **(SGT),** na kudhaminiwa na ***World Evangelism Team,*** chini ya **Kanisa la Kristo.**

**Mawasiliano:**

+255 (0) 764 792 979
+255 (0) 784 880 470
+255 (0) 765 098 981
Kisongo, Arusha, Tanzania

**"…makanisa yote ya Kristo yawasalimu"**
(Warumi 16:16)

## WAANDISHI

George Akpabli
Felix O. Aniamalu
Rex Banks
Wayne Barrier
Paula Bates
Roy Beasley
Mike Benson
Ron Bryant
Charles Burch
Kyle Butt
Frank Chesser
Betty B. Choate
Glenn Colley
Lance Cordle
Sunny David
Hans Dederscheck
David Deffenbaugh
Clarence DeLoach, Jr.
Bill Dillon
Bobby G. Dockery
Hershel Dyer
Earl Edwards
Demar Elam
Raymond Elliott
Reuben Emperado
David Everson
Royce Frederick
E. Claude Gardner
Alex Gibson
Gary C. Hampton
Jack Harriman
Parker Henderson
Gordon Hogan
Wayne Jackson
Ancil Jenkins
Jeff Jenkins
John Kachelman, Jr.
Dayton Keesee
Dalton Key
Michael L. King
J. Randal Matheny
Cecil May, Jr.
Wes McAdams
Colin McKee
Stan Mitchell
Kevin L. Moore
Owen D. Olbricht
David Pharr
Neal Pollard
Mark Posey
Steve Reeves
Rebecca Rushmore
David A. Sargent
David Tarbet
J.J. Turner
Ken Tyler
Allen Webster
R.H. Tex Williams

# WOKOVU WA NUHU NA WOKOVU WETU
# 1 Petro 3:20-21; Warumi 15:4

| WOKOVU WA NUHU | WOKOVU WETU |
|---|---|
| 1. Katika ulimwengu wa dhambi Mwanzo 6:1-5 | Katika ulimwengu wa dhambi. 1 Yohana 5:19; Warumi 3:23; Yohana 3:16-17 |
| 2. Aliamua kufanya mapenzi ya Mungu. Mwanzo 7:1-5; 6:22 | Amua kufanya mapenzi ya Mungu. Yohana 17:17 |
| 3. Alimsikiliza Mungu. Mwanzo 6:9; Amosi 3:3 | Sikia Neno la Mungu. Mathayo 17:1-5; Kum 18:15 |
| 4. Alimwamini Mungu, Alimtii. Waebrania 11:7; Yohana 3:36 | Amini Neno la Mungu katika Kristo. Waebrania 11:8; Yohana 8:24; Warumi 10:17 |
| 5. Aliongozwa na hofu ya Mungu. Waebrania 11:7 | Ongozwa na hofu ya Mungu. Mhubiri 12:13,14; Warumi 2:4; Mdo 17:30-31 |
| 6. Mungu alileta wokovu katika Safina. Waebrania 11 Mwanzo 6 | Mungu anaokoa katika Mwili mmoja, Kanisa. Mdo 2:47; Wakolosai 1:18; Waefeso 1:22-23,4:4 |
| 7. Wachache waliokoka kwa maji. 1 Petro 3:21; Mwanzo 6-9 | Ubatizo ndio unaotuokoa kwa sasa. 1 Petro 3:21; Mdo 2:38; 22:16 |
| 8. Lazima kuwa ndani ya Safina. Mwanzo 7-9 | Lazima kukaa katika Mwili mmoja. Ufunuo 2:10; 2 Petro 2:20-22; Wagalatia 3:26-27 |
| 9. Uhusiano ulibadilika…Mpya. Mwanzo 7:24 | Uhusiano unabadilishwa ndani ya Kristo. Wakolosai 1:13; Warumi 6:3-4; 2 Wakorintho 5:17 |
| **MFANO** | **WOKOVU** |

# Kanisa safi

**Waefeso 5:25-27**

**MUNGU ANALITAMANI**
**Waliookolewa wapo ndani ya Kanisa**
**Mdo 2:47**
**1 Wakorinto12:13**
**Waliookoka ni Wasafi**
**1 Petro 1:22**
**1 Wakorintho 6:9-11**
**Lazima wabaki kuwa safi**
**Mathayo 5:13-16**
**1 Yohana 1:7**

**DHAMBI INALICHAFUA**
**Kumrejesha mkosaji**
**Mathayo 6:1**
**Mathayo 18:15-17**
**Baadhi ya dhambi ni za kukusudia**
**Waebrania 10:26**
**2 Petro 2:21-22**
**Lazima kujiondoa**
**2 Wathesalonike 3:6**
**Warumi 16:17**

**MUNGU ANALISAFISHA**
**Kanisa ni Safi tena**
**1 Wakorintho 5:7**
**Waefeso 5:27**
**Lina hadhi nzuri**
**Mdo 2:46-47**
**Mdo 5:11, 14**
**Mungu anatukuzwa**
**Waefeso 5:21**
**1 Timotheo 3:15**



# SI KILA KITU NI JARIBIO LA USHIRIKA

**Louis Rushmore**

Si kila kitu ni jaribio la ushirika, lakini vitu vingine kwa hakika ni jaribio la ushirika. Pamoja na kuwa kuna vitu vingi katika maisha na dini ambavyo havina maana, kuna idadi ya vitu, ikiwa ni pamoja na imani za kidini na matendo ambavyo vilikuwa na umuhimu hapo kale, vina umuhimu sasa, vitakuwa umuhimu kesho, na vitakuwa na umuhimu milele. Hivyo basi, ni lazima tushikilie maelekezo ya Mungu pale ambapo tutajihusisha na mambo ya maisha haya na ya milele***.“Ee BWANA najua ya kuwa njia ya mwanadamu haimo katika nafasi yake, kuelekeza hatua zake si katika uweza wa mwanadamu”*** (Yeremia 10:25).

Kitabia, kwa kawaida binadamu amepewa zaidi (kuzidi), hivyo katika maisha yake atajihusisha na (mfano;- Siasa, dini, mashirika ya kijamii, kazi n.k). Baadhi ya watu ni wadhaifu sana katika kutii masharti na mwongozo, wakati wengine ni kinyume kwa sababu wanatii kwa ukamilifu utaratibu na imani na hatua zinazostahili. Katika kanisa la Bwana baadhi ya Wakristo hawafanyi bidii sana kutenda maagizo ya Biblia, wakati wengine wanajaribu kwa bidii sana kutii na kutenda maagizo ya Biblia. Wote walioko upande wa kushoto kwenye Biblia wanapoteza mafundisho ya Mungu tuliyopewa, yaani unakuta ndugu katika Kristo wanaweka masharti ambayo Mungu hakuweka. Injili ya Kristo ni ngumu kiasi kuiweka katika maisha ya mtu, kwa maana hiyo

mtu asijichukulie fursa hiyo kufanya kuwa ngumu zaidi, (Wagalatia 1:6-9, Ufunuo 22:18-19).

Kuhusiana na washirika wa kanisa la Bwana ambao hulegeza masharti katika Maandiko, ni upotoshaji na udanganyifukwa wao kujiona kuwa wanasoma au kujifunza zaidi na kukua au kukomaa zaidi katika imani ya Ukristo kuliko wale ambao hawakubaliani nao katika mafundisho ya Agano Jipya. "Ah tulikuwa tukiamini kama ninyi mwanzoni lakini tumechunguza maandiko kwa undani zaidi na tumekomaa kiimani zaidi kwa sasa." Hii hali ya kujikuza zaidi imekuwa chanzo cha maneno ya kuanzisha matumizi ya vyombo vya muziki (na mengineyo pia). Katika ibada ya Kikristo, licha ya ukweli kwamba Agano Jipya linafafanua muziki unaokubalika katika ibada ni ***"mkisemezana kwa zaburi na tenzi na nyimbo za rohoni…"*** (Waefeso 5:19) na ***"…mkifundishana na kuonyana kwa zaburi, na nyimbo, na tenzi za rohoni; huku mkimwimbia Mungu kwa neema mioyoni mwenu."*** (Wakolosai 3:16)




Ile hali ya chochote kutokukatazwa wazi wazi katika Maandiko (Agano Jipya) halafu ikiruhusiwa inachanganya Ukristo, inaweka kando mamlaka ya neno la Mungu kuongoza maisha yetu na kuchukua nafasi kama ya alama za barabarani kutoka duniani kwenda mbinguni (Uzimani) kwa kuongezea inazuia mamlaka ya Biblia kuelekeza amri zake na kuweka pembeni mifano iliyothibitishwa na mafundisho ya mitume na yale ya Agano Jipya kwa ujumla (ambayo kwayo tumeaswa kuyafanya kwa usahihi na kwa kile ambacho tunapaswa).

Zingatia kuwa **Matendo ya mitume 20:7** ni uthibitisho na mafundisho ya mitume kuhusu siku ambayo (siku ya kwanza ya juma) katika siku za wiki kushiriki meza ya Bwana. Si ajabu kwamba wale ambao hawazingatii mifano ya Biblia iliyothibitishwa, hawana mipaka katika kuzingatia siku ya kushiriki meza ya Bwana yaani Jumapili, au

kwamba ni lini na ni mara ngapi inastahili (kwa mwezi, robo mwaka, nusu mwaka, mwaka) au katika matukio gani (mfano harusi).

Zingatia kwamba kwa kila amri katika Agano Jipya kwa binadamu wa sasa, ni lazima afahamu kuwa, yale yaliyoamriwa kwa watu wa karne ya kwanza, pia yanawahusu wale ambao hakutajwa katika maandiko na wale ambao hawakuandikiwa. Bila kidokezi na kujua sababu yake , basi hakuna katika Neno la Mungu jambo ambalo lingemhusu mtu ye yote leo!

Kama jaribio la mwisho kuhalalisha kukengeuka kutoka katika mamlaka ya neno la Mungu (na kuwanyamazisha wapinzani kwa uasi wao), waasi wanadai kwa nguvu na kwa uvumilivu kwa kuegemea katika Warumi 14. Hili pia ni tusi kwa muktadha wa kibiblia. Warumi 14 inahusu mambo ambayo ndugu katika Kristo wanakuwa na hali ya kutofautiana kwa maoni na siyo misingi au mambo yanayohusiana na mafundisho ya Agano Jipya. Ni kosa kubwa kujaribu kuhalalisha ukengeufu kutoka katika neno la Mungu na kulileta katika maoni ya mwanadamu.

Kukengeuka kutoka katika imani ya kikristo kulishatabiriwa na maonyo mengi yalishatolewa. ***"Maana utakuja wakati watakapoyakataa mafundisho yenye uzima; ila kwa kuzifuata nia zao wenyewe watajipatia waalimu makundi makundi, kwa kuwa wana masikio ya utafiti; nao watajiepusha wasisikie yaliyo kweli, na kuzigeukia hadithi za uongo."*** (2 Timotheo 4:3,4). ***"Ndugu zangu, nawasihi, waangalieni wale wafanyao fitina na mambo ya kukwaza kinyume cha mafundisho mliyojifunza; mkajiepushe nao. Kwa sababu walio hivyo hawamtumikii Bwana wetu Kristo, bali matumbo yao wenyewe; na kwa maneno laini na ya kujipendekeza waidanganya mioyo ya watu wanyofu."*** (Warumi 16:17,18). ***"Kila apitaye cheo, wala asidumu katika mafundisho ya Kristo, yeye hana Mungu. Yeye adumuye katika mafundisho hayo, huyo ana Baba na Mwana pia. Mtu akija kwenu, naye haleti mafundisho hayo, msimkaribishe nyumbani mwenu, wala msimpe salamu. Maana yeye ampaye***

***salamu azishiriki kazi zake mbovu."*** (2 Yohana 9-11). Si kila kitu ni jambo la ushirika, lakini baadhi ni jaribio la ushirika.

Pongezi kwa ndugu Byron Nichols! Yeye na mkewe Gay wamefanya kazi na *The Voice of Truth International* kwa miaka 25 sasa. Akiwa amefika katika umri wa heshima wa miaka 79, ndugu Nichols ameamua kuachia taratibu na kuhamisha baadhi tu ya mzigo wa kazi zinazohusiana na uzalishaji wa jarida la miezi mitatu kwa washirika wa timu ya Uinjilisti Duniani. Vinginevyo, kila kitu kinabaki vilevile, na wasomaji wanaweza kutarajia ubora uleule na makala za kidini zenye kujenga ambazo wamekuwa wakizitegemea kwa muda mrefu.

Toleo hili la *The Voice of Truth International, (Sauti ya Ukweli Kimataifa).* Ndugu Byron anatwaa cheo cha Mhariri Mstaafu, na ataendelea kutusaidia kwa uhariri wake bila mipaka. Yeye na dada Gay wamedhamilia kuendelea kulikuza jarida kama ambavyo wamekuwa wakifanya kwa muda mrefu.

Tunayo furaha ya kuwa na wahariri wa nne, Louis Rushmore, kama Mhariri, Jerry Bates Mhariri Mwenza, Byron Nichols kma Mhariri Mstaafu na J.C. Choate kama Mharir Mwanzilishi.



# BIBI ARUSI WA KRISTO

**JERRY BATES**

Biblia inatumia mifano mingi kutusaidia kuweza kulielewa kanisa, kila mfano hutupa sura yake na mifano hii haitupatii picha kamili ya kanisa. labda moja kati ya mifano itakayotupatia picha halisi ni ile ya bibi arusi. Pauolo alisema katika 2 Wakorintho 11:2 ***"maana nawaonea wivu, wivu wa Mungu, kwa kuwa nimewaposea mume mmoja ili nimletee Kristo bikira safi".*** Kwa muda mfupi hebu tutazame mambo ambayo mfano huu unatuambia kuhusu kanisa.

Tabia ya kwanza ni uaminifu au kijitoa. Kama tunavyofahamu mtu anapoingia katika mkataba wa ndoa, mkataba wa undani hufanyika, na mmoja akikiuka (kusaliti), uaminifu huo inakuwa vigumu kusamehe. Vilevile hii inaelezea uaminifu ambao Mkristo anatakiwa kuwa nao kwa Kristo. Unapofanyika kuwa Mkristo unafanya mkataba na Kristo. Umeingia kwenye mkataba wa mahusiano na Kritso na unakuwa wa Kristo, kama vile mume na mke kila mmoja kwa mwenzake. ***"lakini yeye aliyeungwa na Bwana ni roho moja naye"*** (1Wakorintho 6:17). Tunapaswa kuuthamini huu uhusiana zaidi ya uhusiano mwingine wowote au milki (Luka 14:26,27).

Jambo la pili na linalokaribia kulingana na hayo tuliyojadili hapo juu, tunaingia katika mahusiano ya karibu ambayo hayaonekani. Hakuna mahusiano ya karibu katika ulimwengu huu yanayolingana na mahusiano ya mume na mke. Katika Waefeso 5:22,23, Paulo ametumia mahusiano ya mume na mke kulielezea kanisa. Alisema, mke na amtii mume wake. Siku hizi wanawake wengi wanakaidi kutenda hili. Hata hivyo, wakati mtu anapozingatia tabia za mume wake ambazo katika hizo anamtii, haipasi kuona ugumu. Huyu mume alimpenda mke wake kiasi kwamba alikuwa tayari kufa kwa ajili yake. Katika mfano huu wa mume na mke, Paulo, alielezea kifungo baina ya Mkristo na Kristo. Kanisa linamtazama Kristo kama kichwa chake kikamilifu. Yeye ambaye analipenda sana kanisa na akalifia ili alifikishe kwa Mungu kama kanisa takatifu lisilo na doa wala mawaa, (Waefeso 5:25-27). Mtu anapolielewa hili kwa kweli haitakuwa vigumu kwake kusalimisha maisha yake kwa uongozi na mamlaka ya Kristo.

Jambo la tatu, ni kwamba tunafurahia baraka tele za upendo wa Kristo na uangalizi. Yesu anatoa [zawadi ya] wokovu wa uzima kwa kanisa lake (Waefeso 5:23), pia analiendeleza na kulipendezesha (Waefeso 5:29. Analipatia uhai, kwa kutupa chakula na maji ili tusiwe na njaa wala kiu (Yohana 4:13,14;6:35). Hata hivyo, baraka zake hizi ni kwa ajili ya wale tu walio katika Kristo au walio wake (Waefeso 1:3). Hivyo basi, tusipokuwa sehemu ya kanisa au bibi harusi hatutafurahia baraka hizi za rohoni.

Jambo la nne, kanisa linafurahia ahadi za kweli. Mume na mke wameunganishwa kila mmoja kwa mwenzake katika "raha na shida". Hakuna anayefahamu baadaye imebeba nini kwa familia katika ulimwengu huu, sasa hili halina ukweli wowote kwa kanisa kwa sababu kanisa ni Mungu anayetawala yajayo. Paulo katika Warumi 8:17, amesema tu warithi pamoja na Kristo. Chochote kile ambacho Kristo atakifurahia katika baraka za mbinguni na sisi pia tutafurahia. Ndiyo, tunaweza kuteseka kidogo katika ulimwengu huu, kama Kristo naye alivyoteseka, hata hivyo Paulo akiendelea na mfano wake akisema kwamba, kama tukiteseka pamoja naye, ***"tutatukuzwa pamoja naye.***

***Kwa maana nayahesabu mateso ya wakati huu wa sasa kuwa si kitu kama utukufu ule utakaofunuliwa kwetu."*** (Warumi 8:17,18). Katika 2 Wakorintho 4:17 Paulo analinganisha ***"dhiki yetu nyepesi"*** na ***"utukufu wa milele uzidio kuwa mwingi sana"*** Kristo mwenyewe aliahidi katika Mathayo 19:29 haijalishi tunamtolea nini, tutapokea ***"mara mia na kurithi uzima wa milele".*** Hatuwezi kupata picha juu ya uzuri wa baraka na ahadi ambazo Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana alizozihifadhi kwa ajili ya bibi harusi wake.

Mwishowe, bibi arusi apendekeza uzuri. Uzuri huu umefunuliwa kwenye Ufunuo 21:2 ***"Nami nikauona mji ule mtakatifu, Yerusalemu mpya, ukishuka kutoka mbinguni kwa Mungu, umewekwa tayari, kama bibi-arusi aliyekwisha kupambwa kwa mumewe."*** Hakuna linalozidi upendo wa bibi-arusi akiwa amelivaa gauni lake la harusi hasa kwa mumewe. Bwana arusi utumia gharama na muda mwingi kumchagulia gauni, vivyo hivyo na Mungu huandaa nguo kwa ajili ya bibi-arusi wake. ***"Nitafurahi sana katika Bwana, nafsi yangu itashangilia katika Mungu wangu; maana amenivika mavazi ya wokovu, amenifunika vazi la haki, kama bwana arusi ajipambavyo kwa kilemba cha maua, na kama bibi arusi ajipambavyo kwa vyombo vya dhahabu"*** (Isaya 61:10). Bibi-arusi wa Mungu amevikwa gauni jeupe safi la wokovu ambalo Mungu mwenyewe amempatia. Wote tunafahamu jinsi ambavyo bwana arusi anavyofurahi anapomwona bibi-arusi na hilo linawakilisha jinsi Kristo anavyomwona bibi-arusi wake ***"na kama vile bwana arusi amfurahiavyo bibi arusi, ndivyo Mungu wako atakavyokufurahia wewe."*** (Isaya 62:5).



Kwa maana kanisa ni bibi-arusi wa Kristo na atafurahia baraka zote zilizotajwa. Kwa nini mtu asitamani kuwa sehemu yake? Mtu yeyote anayefikiria kanisa sio muhimu, kwa hakika hafahamu asili ya kanisa. Mungu anamwalika kila mmoja wetu afurahie baraka za kuwa bibi-arusi wake. Kwa njia ya imani katika Kristo, tunaunganishwa na Kristo katika ubatizo (Warumi 6:3-5; Wagalatia 3:27) *"**Kwa maana katika Roho mmoja sisi sote tulibatizwa kuwa mwili mmoja, kwamba tu Wayahudi, au kwamba tu Wayunani; ikiwa tu watumwa au ikiwa tu huru; nasi sote tulinyweshwa Roho mmoja.**"* (1 Wakorintho 12:13); hivyo, tuna uwezo wa kufurahia ahadi za kifahari na baraka ambazo ni Mungu pekee anayeweza kutoa kwa ajili ya bibi-arusi wake, hapa (duniani) na kwa umilele wote. Inawezekanaje kwa mtu yoyote asitamani kuwa bibi-arusi wa Kristo?



# MAJINA YA BIBLIA KWA WAFUASI WA YESU

**Byron Nichols**

Watoto wa Mungu au watu katika Agano la Kale waliitwa "Waisrael", lakini wafuasi wa Yesu waliitwa nani katika Agano Jipya? Walitambulikaje? je, walipewa jina maalum, kama ndivyo, lilikuwa lipi?

Maswali haya ni sahihi na muhimu, na yana stahili kujibiwa kwa kuzingatia kile ambacho Biblia inasema kuhusu hayo. Kiukweli majina ni muhimu, na tutaona majina manne yakitumika katika Agano Jipya kuwatambua wafuasi wa Yesu.

Jina **"mwanafunzi"** ni jina linalotawala likitumika katika Injili [Vitabu vya Injili]; limetumika mara chache katika Matendo ya mitume na halikutumika kabisa katika vitabu 22 vya mwisho katika Agano Jipya. Neno hilo limetumika kwa wafuasi wa Kristo, likimaanisha utiifu binafsi kwa mafundisho yake. Yesu alifahamika sana kama mwalimu, na jina hili linaonesha uhusiano wa mwanafunzi na mwalimu. Wafuasi wa Kristo sasa ni **wanafunzi**, kama ilivyokuwa katika nyakati za Agano Jipya.

Jina la pili walilopewa wafuasi wa Yesu ni ***"ndugu"*** (kaka na dada). Yesu aliwaambia wanafunzi wake katika Mathayo 23:8 ***"ninyi nyote ni ndugu."*** Jina hili lilitumika sana baada ya kupaa kwa Kristo. Katika 1 Petro 2:17, Petro alirejelea kanisa kama ***"undugu"***. Paulo alitumia jina ***"ndugu"*** mara nyingi katika nyaraka zake. Zingatia mifano hii (1) katika 1Wakorintho 6:8 alilikemea kusanyiko la Korintho kwa kutenda mambo mabaya ***"…kwa ndugu zenu."*** (2) katika Wagalatia 6:1 aliyaambia makusanyiko ya Galatia, ***"Ndugu zangu, mtu akighafilika***

***katika kosa lo lote,"*** (3) Katika Warumi 12:10 Paulo aliwasihi wale wa kanisa la Rumi ***" Kwa pendo la udugu, mpendane ninyi kwa ninyi; kwa heshima mkiwatanguliza wenzenu;"***

***"Ndugu"*** inaonesha kwamba tuna majukumu na wajibu sisi kwa sisi ambao ni maalum na tofauti na yale kutoka kwa watu [marafiki wa kidunia] kwa ujumla. Uhusiano wetu kama ***"ndugu"*** ni mtakatifu sana kiasi kwamba kumtenda dhambi ***"ndugu"*** ni sawa na kuwa na hatia ya kumtenda dhambi Kristo. ***"Hivyo, mkiwatenda dhambi ndugu zenu na kuitia jeraha dhamiri iliyo dhaifu, mnamtenda dhambi Kristo."*** (1Wakorintho 8:12). Kama wafuasi wa Yesu, tumepewa fursa ya kuwa ndugu **kaka** na **dada**.



Utambulisho wa tatu kwa wafuasi wa Kristo ni ***"mtakatifu".*** Kwa sababu ya jina hili kutumika vibaya mara nyingi katika ulimwengu wa kidini, inaonekana kwamba tunataka kuondoa aibu kwa kutolitumia, hata wengine husema, **"Ah, mimi sio mtakatifu."** Hatupaswi kuwa na shaka kutumia jina hili la kipekee sana.

Neno ***"mtakatifu"*** limetumika katika Biblia likimrejea mtu aliye safi, aliyejiweka wakfu kwa Mungu, ambaye ni mwenye haki. Halikutumika kwa mtu ambaye alionekana na Mungu kama kuwa ni

shujaa wa kidini, bali kwa mtu yeyote ambaye ni mwenye haki na safi katika macho ya Mungu.

Jina ***"mtakatifu"*** linaonekana mara nyingi katika Agano Jipya. Kwa mfano, katika Matendo ya mitume 9:13, Anania alisema, ***"Bwana, nimesikia habari za mtu huyu kwa watu wengi, mabaya mengi aliyowatenda watakatifu wako Yerusalemu;"*** halafu aya ya 41 inazungumzia Petro alivyomfufuo Dorkasi: ***"…hata akiisha kuwaita wale watakatifu na wajane akamweka mbele yao, hali yu hai."*** Katika Agano Jipya Kuna idadi kubwa ya marejeo ya wafuasi wa Kristo kama [wakiitwa] ***"watakatifu".*** Ndiyo, wafuasi wake wote waaminifu ni **watakatifu.**

jina la nne na maarufu linalotumika leo kuwarejelea wafuasi wa Yesu ni ***"Mkristo".*** Jina hili, kwa bahati mbaya, sasa hivi linatumika vibaya na wengi kurejea kwa wote ambao wanaonesha imani yoyote katika Kristo. Ukiangalia matumizi ya jina hili katika Agano Jipya utaona kwamba lilitumika tu kwa wale ambao ni wafuasi wa kweli wa Kristo, na si kwa wale ambao maisha yao yanaonesha udhaifu au kutokujitoa kihalisia kwa Kristo.

***Kuvaa jina Mkristo, Mtakatifu, ndugu wa kiume au wa kike, au mwanafunzi yote mawili ni fursa na wajibu.***

Waumini watiifu wa kwanza katika Kristo hawakujulikana kwa jina ***"Mkristo"*** mara tu baada ya kuongoka kwao. Hatuna maelezo kwa jinsi gani hili lilitokea, lakini tunajifunza kutoka katika Matendo ya mitume 11:26 kwamba ***"… Na wanafunzi waliitwa Wakristo kwanza hapo Antiokia."*** Jina hili pia linapatikana katika Matendo ya mitume 26 wakati Paulo alipokuwa akimfundisha Mfalme Agrippa kuhusu Kristo, na katika aya ya 27 aliuliza, ***"Mfalme Agripa, je! Wawaamini manabii? Najua ya kuwa wawaamini."*** Halafu katika aya ya 28 Agripa akajibu, ***"Agripa akamwambia Paulo, Kwa maneno machache wadhani kunifanya mimi kuwa Mkristo."*** Tunaona kwamba Agripa alielewa kwamba kuwa Mkristo kunahusisha zaidi kuliko tu kuamini, yeye tayari aliamini, lakini hakuwa Mkristo. Hakukabidhi nafsi yake katika mapenzi

ya Mungu kwa kuwa muumini mtiifu. Tunaona Mkristo kwa mara ya tatu katika 1Petro 4:16, ***“Lakini ikiwa kwa sababu ni Mkristo asione haya, bali amtukuze Mungu katika jina hilo.”***

Kuvaa majina **Mkristo, mtakatifu, ndugu wa kiume au wa kike, au mwanafunzi** ni fursa na wajibu. Wote tunaweza kuomba kwamba tuyavae [majina hayo] ipasavyo.

# Shukrani kwa Maxie B. Boren

**Byron Nichols**

Jumapili asubuhi, 14/08/2016, jeshi la Bwana lilipoteza mmoja kati aksari makada wake. Maxie B. Boren alifariki katika umri wa miaka 84, baada ya kuteseka kwa matatizo ya kiafya kwa miaka michache iliyopita, lakini hususani katika miezi ya hivi karibuni. Pamoja na hayo, aliendelea kuhubiri hata mapema mwaka huu.

Maxie alikuwa mmoja wa wafanyakazi waandishi wa *Sauti ya Ukweli Kimataifa* (*The Voice of Truth International)* tangu mwanzo na kuwa mhamasishaji makini wa jarida.

Alipendezwa na kuhubiri kwa miaka 62. Ametumika katika makusanyiko kadhaa kama mhubiri wao na kuhubiri katika mikutano ya Injili zaidi ya 700 kutoka pwani hadi pwani na katika nchi nyinginezo. Alijulikana na kuheshimiwa kwa kiwango cha juu kwa maarifa yake ya Maandiko na upendo wake kwa roho za watu kila sehemu.

Maxie alikuwa na uhusiano wa muda mrefu na kujitoa pamoja na kusanyiko la Brown Trail huko Bedford, Texas. Hapo alikuwa ni mhubiri wa mimbarini; kwa miaka mingi alitumika kama Mkurugenzi wa kila mwaka Ngome ya Thamani ya Hotuba (the annual Fort Worth Lectureship) iliyodhaminiwa na kusanyiko la Brown Trail. Awali alitumika kama Mkurugenzi wa Shule ya Mahubiri ya Brown Trail, na amekuwa akitumika kama mmoja wa wazee wa kusanyiko la Brown Trail kwa miaka kadhaa.

Kwa miaka mingi Maxie na mkewe kipenzi Fran wamekuwa ni wakipekee sana na marafiki wa karibu kwa mke wangu Gay na mimi. Tuna huzuni sana kwa huku kupoteza, lakini tunafurahia maarifa ya juu yatokanayo na Kristo ambayo yamekuja kama matokeo ya juhudi za wote wawili Maxie na Fran.



1932-2008

# Tulifanye Kanisa Liwe katika Mwendo!

J.C. Choate

Si jambo jipya kuona maelezo karibu katika kila mada ya Injili ikizungumzia kusanyiko fulani ambalo liko kwenye mwendo. Kuthibitisha hili imeelezwa kwamba jarida likiwa limetumwa kwa kila mshirika. Mahudhurio yanaongezeka, idadi ya waongofu inaongezeka (ingawa kwa sasa si mara nyingi kama awali), jingo jipya linaongezeka au ukumbi wa ushirika unajengwa,n.k. wakati haya yote yakionekana kuendelea, mara nyingi nimekuwa nikistahajabu kwa nini shughuli inawekewa ukomo kwa makusanyiko machache tu yaliyotawanyika kote katika nchi, na ni kwa nini kuna uchache wa mipango yoyote inayotajwa ya uinjilisti? Kwa nini kanisa la kila sehemu lisipaswe kuwa katika mwendo?

Nenda katika kila mji uuchaguao ambapo kuna makusanyiko ya mwili wa Bwana na, ukihitaji maelezo, utagundua kwamba katika mambo mengi moja au mawili kati yao ndiyo yanasonga mbele, wakifanya maendeleo fulani, wakati mengine yanabaki kugharimu tu. Kwa nini ni lazima iwe hivi? Kwa nini haipaswi yote kukua na kutafuta kufanya zaidi? Kwa nini mengi miungoni mwao hayako katika mwendo?

Katika ulimwengu wa uinjilisti halisi wa nyumbani na kazi za umisionari nchi za ng’ambo, utashangazwa kuona ni wachache kiasi gani wanaofanya kazi, wakati wengi wao wanaweka kiasi kidogo sana cha bajeti yao na juhudi za washirika wao katika uinjilisti wa nyumbani

au ng’ambo. Ndugu wengi wanatumia hoja ile ile ambayo baadhi ya miji yetu hutumia, na hiyo ni, “Tumia fedha zako nyumbani.” Lakini hata fedha zinazotumika nyumbani mara nyingi zaidi ni katika ujenzi au baadhi ya safari za ushirika au kwa mradi fulani kwa ajili ya faida/burudani ya wale ambao ni washirika. Kufikia wengine kuko wapi?

Kinachohitajika zaidi kuliko kitu kingine katika ulimwengu huu wa nafsi zilizopotea ni kwa kanisa lote kuwa katika mwendo na bado haitoshi kuwepo tu “katika mwendo”. Baadhi yanaenenda vizuri, lakini yanarudi nyuma! Kanisa linahitaji kuwa katika mwendo, na maono na lengo la makusudi. Mikutano ya mkakati inapaswa kulenga katika ufanisi wa mipango iliyobuniwa ya kuelimisha na kuvutia kanisa kuifikia kila nyumba katika jamii/miji yao na kujihusisha katika kazi nzuri za kigeni [za nje tunahitajika kuungana katika kujitoa kwetu kuipeleka Injili kwa taifa letu na kwa kila taifa lingine lililo chini ya mbingu. **Ni miradi gani ambayo inahitaji kuendelezwa?**

- Panga ratiba ya kubisha hodi kwa washirika kugawa vipeperushi, waarike watu kwenye mkutano wa Injili, watoto kwa VBS, au kwa shughuli fulani iliyopangwa ya kanisa. Fanya hivi kwa kurudia rudia ili kanisa liweze kujulikana.
- Kuwa na darasa la kuwafundisha washirika, hatua kwa hatua, jinsi ya kufundisha Injili kwa mtu mmoja mmoja katika masomo ya nyumbani.
- Omba kibali cha kuweka onesho kila mwezi nje ya duka Wal-Mart au katika maduka mengine maarufu kugawa vipeperushi, kozi za Biblia, na masomo ya nyumbani kwa watu wenye shahuku ambao huja hapo.
- Weka orodha ya wagonjwa wote, wazee, na washirika wasio waaminifu, na upange makundi ya kujitolea kuwatembelea kila juma wale wenye uhitaji au wale ambao hawakuhudhuria kanisani.
- Husisha vijana katika huduma za miradi kwa ajili ya jamii.

- Unga mkono moja au zaidi juhudi za umisheni za ng'ambo. Shirikini taarifa ya kazi na kanisa, na ikiwezekana wafanye wazee waitembelee kazi hiyo ili kwamba mahitaji na mafanikio yawe halisi zaidi kwa wote waliohusika.

Tunapoikamata roho halisi ya Ukristo na kupoteza ubinafsi wetu na kujipendelea wenyewe, tutakuwa tumefanywa upya kwa bidii, na tutajiona tukisonga katika muelekeo sahihi. Hatutakuwa tukitilia mkazo vitu vya ulimwengu, vya kidunia, vya kimwili, vitu vya fahari katika maisha, na kile tunachoweza kujipatia, lakini tutakuwa tukiweka mkazo sehemu sahihi kwa Mungu, Kristo, kwa kanisa, mapenzi ya Bwana, umilele, mbingu, na roho za binadamu. Ikiwa sisi sote tukifanya upya huku kujitoa, hapo halitakuwa jambo la makusanyiko machache yaliyo katika mwendo, bali kanisa lote litakuwa katika mwendo! Matokeo yatahisiwa kote ulimwenguni, Bwana, aiharakishe siku hiyo

# YALIYOMO


**MUNGU**

Dhambi – Ina thamani gani?..................................Dale Jankins…………25
Mwanamke Hatari zaidi Ulimwenguni……Stan Mitchell……………………...27
Azazeli…………………………………………………Jack W. Carter……………………..30

**USHAHIDI**

Taswira ya Mwisho: Mageuzi ya Mwanadamu……...….Paul Holland……32
Zaburi 19:1-3………………..Author Unknown………………………...……………..33
Pomboo aongea………………………………...…..David Everson…………………..…36

**NENO LA MUNGU**

Maajabu Saba ya Neno……………………..Charles Pugh III……………...……..…39
Kulitumia Neno kwa halali Kunahitaji mafunzo sahihi ya Biblia…David R. Kenney………………………………………………………………………………………...….42
Kitabu chake cha thamani……………………David A. Sargent…………….….45

**WOKOVU**

Kitabu cha Uzima cha Mwana-kondoo……………..…..David R. Pharr……….51
Swali kubwa: Ipi?.........................Carroll Sites……………………………….…..54
Na Hakutakuwa na Usiku Kule…………….Ardron Hinton………………...…..56

**KANISA**

Kisababishi cha Ukuaji wa Kanisa…………….…Wayne Barrier…………….59
Wasifu kutoka Makaburini…………………Bobby Dockery…………………….62
"Upendo wa Ndugu na Udumu" Waebrania 13:1.….Cecil May Jr…......65
Moja ni nzuri kama nyingine……..?...................Bill Dillon………………...67

**FUNDISHO LA KUISHI KWALO**

Kumwita Bwana……………….…Owen D, Oibricht…………………….………......68
Je, Ukweli unajalisha?...........................Bobby Key…………………………..71
Uhalali wa Ombi la Marejesho……………….Jim Howard…………………….72
Umoja na Fundisho………………………….……..Ben Jones………………………74

**UKRISTO KATIKA MATENDO**

Huna tumaini? Si haraka hivyo………..….Steve Higginbotham……….….78
Aliendelea Kuhubiri Injili…………………….Wyne Brewer……………………80
Miaka 24 katika Ngazi ya Kwanza!.............Jess Whitlock,,,,,,,,,,,..,,,,,,82

## IBADA

Nini unacheweza kufanya Jumamosi kuifanya Jumapili kuwa ya Ibada zaidi?................................J. Randal Matheny……………………………..85
Ombeni Bila Kukoma………………………..Dalton Key…….......................88
Kuonesha Shukrani katika Meza ya Bwana…Maxie B. Boren…….………..90
Maneno ndiyo kila kitu?....................Andy Robison……………………….…94

## MAISHA YA KILA SIKU YA MKRISTO

Bado Sauti ni Ndogo………………………Rani Timoti………….……………100
Kielelezo cha Ukristo……………………………Neil Richey…………………...102
Nini kinachomfanya mtu kuwa Mtumishi wa Mungu? Bob Plunket…………………………………………………………………………...104
"Baba yangu, Mhubiri"…………………...Mark N. Posey.……………………..106
Sikufanya vyakutosha! ……………………...Dayton Keesee…………………108

## NYUMBA YA MKRISTO

Ndoa ni kipimo cha Jaribu?.......................Danny Boggs……………..…110
Familia Yako inaendeleaje?..................John Gipson………………….….113
Okoa Ndoa……………………………………..Dale Grissom…………………..115

## MASOMO KATIKA ANDIKO

Sura ya furaha ya Biblia…………………..David Shannon…………………..118
Mwisho wa Yote………………………………Jim Laws…………………………..121
Je, Haya Majibu yanafaa?.............Betty Burton Choate…………………124

## WAHUSIKA WA BIBLIA

Hivi Sivyo Jinsi Unavyoanza……………..Jimmy Clark……………………129
Stefano……………………………………………Jack Harriman……………..…132
Epafra, Mtumwa wa Kristo Yesu…………….Harvey Porter………………..134
Vipi kuhusu Gharika?..........................Dennis Gulledge…..……………137
Mfano wa Ubatizo una umuhimu gani?..........Charles R. Rose………..138
Wanikolai, walikuwa akina nan?...................Mike Riley…………………141

## CHATI NA MUHTASARI

Masomo mazuri kutoka kwa Ayubu………Therman Hodge……………..142
Kwenda Mbali………………………………………Ken Tyler……………………..144

## HISTORIA YA KANISA

Marejesho ni Lengo la kutamanika?..............D. Gene West…………...146

**VIPENGELE, MASHAIRI NA VIJAZO**

Isaya 49:14-16……………………....…Upande wa ndani wa Gamba la mbele
Wokovu wa Nuhu & Wokovu Wetu……………..…Donnie S. Barnes…….…..3
Kanisa safi………………………………..Donnie S. Barnes…………….…………….4
Si kila kitu ni Jaribio la Ushirika…………………Louis Rushmore…………..….5
Bibi-Arusi wa Kristo……………………………..…Jerry Bates……….……………..9
Majina ya Biblia kwa Wafuasi wa Yesu…………....Byron Nichols……..…..13
Shukrani kwa Maxie B. Boren……….…………..Byron Nichols…………..….17
Tulifanye Kanisa liwe katika mwendo……………J.C. Choate………………18
Picha katika Ukuta…………………………..……..Joslyn Ramsubhag…..…………..24
Je, Ulijua?............................Rebecca Rushmore………….29,38,41,61,107
Tafuta Aya………………………………….…Jerry Bates……………………………..48
Jipime na Biblia…………………………Louis Rushmore…………………………58
Wazo la Haraka juu ya aya muhimu..…Betty Burton Choate……………..77
Je, Unapimaje?.......................Betty Burton Choate…………………………..84
Je, Umesali?....................................Chad Ezelle…………………………….…93
Uchangamfu: Mithali 17:22…………..…Byron Nichols………………….…..97
Kazi yangu iko wapi?.......................Louis Rushmore…..…………………109
Kwanini Waliitwa Wakristo?................Jerry Bates………………………..123
Mwokotezaji Mawindo………………………Rebecca Rushmore………….128

# Picha katika Ukuta

**Joslyn Ramsubhag**

Kuna picha inaning'inia
Ndiyo, juu ya ukuta.
Imefichika na kuwekwa salama,
Hatuthubutu kuiacha idondoke.

Daima kuna wapiti njia,
Siku zote hutamani mkao wake.
Ikiwakazia macho kila anayeangalia,
Kwa hiyo haitambui kelele

Kuna aliyeketi katika kiti cha kale,
Kama aliyewa na hisia,
Mtu huyu mwuungwana katika vazi zuri,
Inaonekana katika ibada takatifu

Ikiwa daima ulionekana,
Kama picha hii katika ukuta,
Wengine wangeacha kukutamani?
Au wangeweza kuona dosari yako?

Kama ni lazima uwe picha,
Kwa ulmwengu kuona,
Kwa upole geuza maisha yako nyuma;
Kuwa mwangalifu…ni wewe halisi.

Halafu, wakati wengine wakikutazama mara nyingi,
Na kutaka kukufanya kielelezo,
Vuta picha…Oh ni nzuri kiasi gani,
Maisha yao yote yatakuwa ni kweli

# Dhambi – Inathamani gani?

## Dale Jenkins

**DHAMBI** Itakupeleka mbali kuliko unavyotaka kwenda. Itakugharimu zaidi kuliko unavyotaka kulipa. Itawaumiza watu wengi kuliko ambavyo ungeweza kufikiri ingeumiza Itakuacha mwenye baridi, ukijiuliza na kujiona mjinga. Itakuacha ujione huna kitu, mchafu, na usiye na thamani. Itakudanganya, kukuongopea, na kukuumiza. Itakuchukua kwa yote ambayo una thamani. Itazaa maumivu, hatia itajirudia-rudia ambayo itakufanya usiamini wengine kwa sababu huwezi kujiamini mwenyewe. Itazaa hofu. Itakutenga na yote ambayo ni mazuri, sahihi, na yenye uzuri. Italeta maisha mafupi kwa kitambo kulidhika kwa kidunia matakwa ambayo yatakuwa yameondoka mara baada ya dhambi kutulia.Unapozeeka itakufanya uwe wa baridi, uwe mbali, uwe mbaya, mjinga, na mwenye kujawa na chuki. Itaiba furaha yako, amani yako, na marafiki zako, lakini zaidi ya yote itaitupa roho yako katika jehanamu ya milele.

**MUNGU** Atakupenda zaidi kuliko ulivyowai kupendwa. Atakutana na mahitaji yako ambayo hata huwezi kutambua kuwa unayo. Atakuwepo wakati adui yako mkuu akijaribu kukushambulia au rafiki yako wa karibu akusalitipo. Atajibu maswali ambayo uliamini hayana majibu.

Atakuacha ukiwa umetimilika, umetakasika, na mwenye thamani. Atakuambia ukweli, kamwe hatakuongoza katika majaribu, na atakushikilia karibu yake katika ulinzi wake mwenyewe. Atakupenda hata utakapojihisi huna thamani. Atazalisha usafi na dhamiri safi na utulivu. Atazitupa mbali hofu zote. Atakusaidia uwe mwema, sahihi, na kupendeza. Atakupatia raha ya ndani ya kina na furaha ambayo itadumu wakati ulimwengu wote unaokuzunguka ukivunjika. Unapozeeka, atakufanya uwe na joto, mwenye upendo, mzuri, mwenye matumaini, na kupendwa. Atakupa raha isiyoweza

kufafanishwa, amani ipitayo ufahamu, marafiki wa karibu kuliko ndugu, lakini zaidi sana, atakuhakikishia umilele Mbinguni.

Nataka upendo wa Mungu! Nahitaji upendo wa Mungu! Mungu, nisaidie niwatie mafuta wengine kwa upendo wako upitao kiasi katika kila kukutana kwangu. Nisaidie kuepuka dhambi ambayo itanidhoofisha lakini kwa hakika itanitenga mimi nawe. Nipe upendo ule daima, na nifundishe kupenda.

***"Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi." (Warumi 5:8)***

***"Basi, tuseme nini juu ya hayo? Mungu akiwapo upande wetu, ni nani aliye juu yetu? Yeye asiyemwachilia Mwana wake mwenyewe, bali alimtoa kwa ajili yetu sisi sote, atakosaje kutukirimia na mambo yote pamoja naye? Ni nani atakayewashitaki wateule wa Mungu? Mungu ndiye mwenye kuwahesabia haki. Ni nani atakayewahukumia adhabu? Kristo Yesu ndiye aliyekufa; naam, na zaidi ya hayo, amefufuka katika wafu, naye yuko mkono wa kuume wa Mungu; tena ndiye anayetuombea. Ni nani atakayetutenga na upendo wa Kristo? Je! Ni dhiki au shida, au adha, au njaa, au uchi, au hatari, au upanga? Kama ilivyoandikwa, ya kwamba, Kwa ajili yako tunauawa mchana kutwa, Tumehesabiwa kuwa kama kondoo wa kuchinjwa. Lakini katika mambo hayo yote tunashinda, na zaidi ya kushinda, kwa yeye aliyetupenda. Kwa maana nimekwisha kujua hakika ya kwamba, wala mauti, wala uzima, wala malaika, wala wenye mamlaka, wala yaliyopo, wala yatakayokuwapo, wala wenye uwezo, wala yaliyo juu, wala yaliyo chini, wala kiumbe kinginecho chote hakitaweza kututenga na upendo wa Mungu ulio katika Kristo Yesu Bwana wetu."*** (Warumi 8:31-39)

**Dale Jenkins anahubiri katika kusanyiko la Spring Meadow katika Spring Hill, Tennessee, Marekani.**

# Mwanamke Hatari zaidi Ulimwenguni

**Stan Mitchell**

Alikuwa, ni Adolph Hitler aliwai kusema, “mwanamke hatari zaidi katika England.” Alikuwa nani? Mpelelezi? Mwana sayansi wa nyuklia katika hatihati ya ugunduzi wa silaha ya maangamizi?

Alimwendeleza Hitler, Goering, Himmler, na Mengele, watu wanne wa kutisha. Churchill, Roosevelt, Montgomery, na MacArthur, watu waliosimama kwa jambo fulani sahihi, pia, walikufa kitambo. Huenda Wamerekani na kizazi kipya kwa taifa katika siku zile za giza.

Wakati washambuliaji wa Hitler walipomulika usiku kwa vifaa vya uchunguzi, wakati London ilipochomwa, wakati watu wa London walipokusanywa katika makazi, hatimaye usiku uliingia wakati kasri la Buckingham liliposhambuliwa pia. Ndani ya kasri kulikuwa na mabinti wawili wa kifalme, Elizabeth (baadaye akawa Malkia Elizabeth II) na



Margaret. Wasiwasi wa waandishi wa magazeti walitembelea kuta za kasri siku iliyofuata waliuliza swali lililokuwa katika akili ya kila mmoja: “Haipaswi mazingira ya familia ya kifalme, mabinti wa kifalme kuwa mbali na katikati ya London kwa usalama wao wenyewe?” Jibu la mama malkia lilikuwa la hali ya juu: “Watoto hawataondoka labda mimi niondoke,” alianza, “Sitaondoka labda baba yao akiondoka,” aliongeza, “na kwa vyovyote mfalme hataiacha nchi katika mazingira yoyote.”



Elizabeth, Mama Malkia jasiri, alikuwa ndiye haswa kilichohitajika kwa taifa kwa wakati huo. Lazima kulitakiwa kuwe na ushawishi usiozuilika kwa ajili ya utii si kwa kushiriki katika shida yake. Baada ya yote, hata Mama Malkia anawapenda watoto wake! Kwa cheche ya moshi na miale ya moto angani na kelele za mabomu yanayodondoka juu ya kichwa, familia ya kifalme ya Uingereza ilibaki London.

Wakati ulimwengu ulipowaka kwa chuki na dhambi, Mungu angeweza kumchukua Mtoto wake hata Mbinguni kwenye faraja, lakini hakufanya hivyo. Yesu akafanyika mwanadamu na kustahimili aibu ya ubinadamu. Alitembea katika mitaa ya vumbi ya Palestina, ***"hakuwa na hata sehemu ya kulaza kichwa chake",*** na akateseka hata kifo, hakika ni sababu ya wanadamu wote kuwa nayo. Alikuja katika sayari inayoteketea na aliungua kwa mapenzi yaleyale sisi sote tunajua. Hii ilimpa Yeye uelewa kwamba watu wote mashuhuri katika historia walipitia. Anaelewa taabu yetu. Kutoka katika mtazamo wa Shetani, hiyo inamfanya Yesu kuwa ni mtu hatari zaidi katika historia!

***"Na kwa kuwa mwenyewe aliteswa alipojaribiwa, aweza kuwasaidia wao wanaojaribiwa."*** (Waebrania 2:18).

**Stan Mitchell anafundisha katika Kitengo cha Biblia katika Chuo kikuu cha Freed-Hardeman huko Henderson, Tennessee, USA. Imetumiwa kwa ruhusa kutoka Forthright.net.**

# Je, Ulijua?

Mefiboshethi alikuwa ni mtu mwenye sifa nzuri. Ingawa angeweza kurudisha familia yake katika ufalme wa Israeli, lakini alibaki kuwa mnyenyekevu. Kwa uungwana alipewa ardhi ya baba yake hata hivyo hakuwa na tamaa ya kutaka zaidi au kudai kile kilichokuwa ni "haki" yake. Ingawa mfalme aliyemtumikia alikuwa akitawala katika kasri ya babu yake, Mefiboshethi alimwonesha mfalme heshima ya hali ya juu. Wakati ardhi yake ilipochukuliwa kwa ujanja, hakutafuta kisasi. Katika mambo yote, Mefiboshethi alitosheka na kile alichokuwa nacho na kushukuru kwa Baraka katika maisha yake. Unaweza kusoma kuhusu Mefiboshethi katika 2 Samweli 4, 9, 16, 19, and 21.

# AZAZELI

Jack W. Carter

Mtu huyu ametajwa katika sura moja tu (Mambo ya Walawi 16), lakini namchukilia yeye kama mmoja wa wahusika muhimu zaidi wa Biblia. Hili linaweza kuonekana ni jambo geni hususani kwa kuwa yeye ni mbuzi. Neno : ***"Azazeli"*** limeambatanishwa na mbuzi huyu aidha kama jina au lina rejelea mwisho wa safari yake.

Kwa kawaida na hususani, anarejelewa kama "msingiziwa", na alishiriki sehemu yake katika Siku ya Upatanisho. Katika siku hii, mbuzi wawili walichaguliwa, mmoja kama dhabihu na mwingine kama ***"mbuzi wa maondoleo".*** Walichaguliwa kwa kupigiwa kura. Baada ya mbuzi wa kwanza kutolewa kafara, Haruni (Kuhani Mkuu) aliweka mikono yake katika kichwa cha mbuzi wa pili na kukili dhambi zote za kusanyiko lote la Israeli. Halafu mbuzi huyu aliongozwa kwenda nyikani na kuachiwa. Mtu aliyemwongoza alitakiwa kuoga na kubadili mavazi yake pindi aliporudi.

Umuhimu wa hili unakuwa wazi mara moja, ni njia ya Mungu kuonesha jinsi anavyotuondolea dhambi zetu moja kwa moja mbali nasi. Daima najumuisha hili na kifungu katika Kitabu cha Zaburi. *"**Maana mbingu zilivyoinuka juu ya nchi, Kadiri ile ile rehema zake ni kuu kwa wamchao. Kama mashariki ilivyo mbali na magharibi, Ndivyo alivyoweka dhambi zetu mbali nasi."*** (Zaburi 103:11,12). Ni kosa kabisa kumdhania Mungu kama mtu ambaye anakumbatia chuki. Je, tunamdhania namna hii kwa sababu kukumbatia chuki ndio mwelekeo wetu? Wakati Mungu anapotusamehe dhambi zetu, huo ndio mwisho wake. Kifungu kingine kinachonisaidia kuelewa hili ni, ***"Ni nani aliye Mungu kama wewe, mwenye kusamehe uovu, na kuliachilia kosa la watu wa urithi wake waliosalia? Hashiki hasira yake milele, kwa maana yeye hufurahia rehema. Atarejea na***

***kutuhurumia; atayakanyaga maovu yetu; nawe utazitupa dhambi zao zote katika vilindi vya bahari."*** (Mika 7:18,19).

Kila ninapoelekea kuishi katika dhambi ambayo imelimbikiza katika maisha yangu, najaribu kurejea vifungu hivi. Halafu nasonga mbele na maisha yangu.

**Jack W. Carter (1930-2013) alikuwa mhubiri kwa miaka mingi huko Colorado, Marekani.**

# Taswira ya Mwisho: Mageuzi ya Mwanadamu

**Paul Holland**

Paleontolojia ni somo kuhusu mtu wa kale. Imekuwa ikirejelewa kama “kiima” cha sayansi zote za baiolojia. Hiyo ni kwamba, kuna hisia nyingi na maoni mbali mbali katika palentolojia kuliko ugumu wa vithibitisho. William Fix, mwana sayansi mwandishi, anasema: “mtu angeweza kuwa na fikra kwamba historia ya eneo hili ilikuwa ni uthibitisho wa kamba ya ushindi isiyokatika; badala yake ni orodha ya kushindwa” (*Bone Peddlers: Selling Evolution* 4). Hapa ni kuonesha udhaifu wa mambo mawili katika hadithi ya sasa ya mageuzi ya mwanadamu.

## Ushahidi wa Mtu wa Zamani umetiwa Doa:

Fikiria kuhusu “Mtu asiyestaarabika”. Mara nyingi, wana sayansi watasema, “Sayansi ni kujisahihisha”. Ndiyo, iko hivyo, kama wewe ni mtu wa kupokea mawazo mapaya, hukupofushwa na itikadi. Lakini fikiria ni watu wangapi waliodanganywa na huu udanganyifu! Ilichukua miaka 40 kwa ukweli kutoka hadharani!

Nimetoka kumaliza kusoma Gap. Sayansi inayotutenga kutoka kwa Wanyama, kimechapishwa 2013, ambacho kinaendelea kutumia Mtu wa Java [mabaki ya mtu wa kale yaliyopatikana huko Java, hivyo yalipewa jina la Java Man] kama mfano wa mageuzi ya mwanadamu! (252). Haikuwa muda mrefu sana tangu Mtu wa Java ilipogunduliwa katika miaka ya 1800 ambayo ilithibitishwa kwamba meno na fupa la paja vilikuwa vya mtu lakini fuvu lilikuwa la tumbili! Hata hivyo, “Mtu wa Java” bado anaendelea kutangazwa kama “kiungo” katika mnyororo wa mageuzi ya mwanadamu!

## Hii ni Sanaa au Sayansi?

Michoro ya "sokwe watu" ni **dhana ya msanii**. Usiache hoja hii iingie kwa sikio moja na kutoka kwa lingine! Mwana mageuzi na mtaalam wa mambo ya asili na mahusiano ya kijamii Frederick Hulse, ambaye alifundisha katika Chuo kikuu cha Arizona State wakati mmoja aliandika kitabu chake, aliandika *Aina za Binadamu: Utangulizi wa Umbile kuhusu binadamu:* "…kuumbwa upya kwa wanyama wote kutoka katika kipande fulani kidogo cha mfupa iko nje ya swali" (79). Anaendelea, "wakati huo huo, lazima tuelewe kwamba marudio ya matengenezo ni kazi ya kufikirika na kwa hivyo ni matokeo ya mawazo katika akili ya mtengenezaji [sic]. Picha za zamani za kale za wazee wetu wenyewe, mara nyingi hutumika kuelezea vitabu kuhusiana nao, inaweza kuwa upotoshaji hatari, kwa kweli hakuna tunachojua kuhusu kiwango chao cha rangi ya asili, kiwango cha nywele za mwilini, au unene wa midomo yao" (80).

## Asili ya Mtu Kibiblia:

Kama tunashauku na ukweli, kile kinachohusiana na uhalisia, hivyo Biblia ndio chanzo pekee cha maelezo ambayo yanahusiana na uhalisia pindi unapotokea utatanishi juu ya asili na mwanzo wa binadamu. Bila shaka, Mwanzo 1:26 inasema, ***"Mungu akasema, Na tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu; wakatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na wanyama, na nchi yote pia, na kila chenye kutambaa kitambaacho juu ya nchi."***

Kwa historia hii, wote Yesu na waandishi wa Agano Jipya wako ndani ya makubaliano. Yesu anathibitisha hilo mwanzoni, Mungu aliumba mtu mwanamume na mwanamke (Mathayo 19:4). Hawakugeuka; via vya uzazi havikugeuka. Vyote vilumbwa na kuundwa na Mungu.

Yesu anathibitisha kwamba Adamu alikuwa ni mtu wa kwanza (Marko 10:6). Hakukuwa na binadamu kabla, viumbe aina ya sokwe. Adam alikuwa mdogo kuliko dunia kwa siku tano tu. Je, Adamu aliishi katika pango pindi alipofukuzwa kwenye Bustani ya Edeni? Kuna

uwezekano. Hapo kabla ya vifaa vya ujenzi viliboreshwa, binadamu waliishi katika mapango. Pango la kwanza kutajwa katika Biblia lipo katika Mwanzo 19 wakati Lutu alipoishi katika pango wakati Mungu alipoiharibu miji ya Sodoma na Gomora. Kuishi katika mapango si ishara ya mtu wa kale wala si ishara ya elimu duni au maarifa duni.

Mtume Paulo pia alithibitisha kwamba Adamu alikuwa mwanamume wa kwanza (1 Wakorintho 15:45) na kwamba Hawa alikuwa ni mwanamke wa kwanza (1 Timotheo 2:13). Kwa hiyo waandishi wa Agano Jipya wana kauli moja, ukimjumuisha na Yesu Mwenyewe. Hivyo maelezo ya Biblia kuhusu uumbaji yanayopatikana katika kitabu cha Mwanzo ni historia ya kweli na sahihi ya mwanzo halisi wa binadamu.

Maelezo ya wana sayansi kuhusu mwanzo wa binadamu yamejaa nyufa. Ni Biblia pekee inayotoa maelezo sahihi ya mwanzo wa bindamu. Tumeumbwa kwa sura na mfano wa Baba wa Mbinguni.

**Paul Holland ni mhubiri wa Kanisa la Kristo Swartz Creek huko Swartz Creek, Michigan, Marekani.**

# Zaburi 19:1-3

### Mwandishi Asiyejulikana

***" Mbingu zauhubiri utukufu wa Mungu, Na anga laitangaza kazi ya mikono yake.Mchana husemezana na mchana, Usiku hutolea usiku maarifa. Hakuna lugha wala maneno, Sauti yao haisikilikani.."***

Dunia inazunguka katika muhimili wake kwa takribani maili 1000 kwa saa. Kama hiyo ingekuwa maili 100 kwa saa, mchana na usiku ungekuwa mrefu mara 10 zaidi, na sayari yetu ingeungua bila shaka na hali ya kuganda. Chini ya mazingira hayo, mimea isingeweza kuishi.

Kama dunia ingekuwa ndogo kama mwezi, nguvu ya mvutano ingekuwa dhaifu sana kuweza kuhifadhi hali ya hewa sahihi kwa ajili ya mahitaji ya mwanadamu, lakini kama ingekuwa kubwa kama Jupita, Saturn, au Uranus, kungekuwa na nguvu kubwa ya uvutano ambayo ingefanya harakati za binadamu kushindikana.

Kama tungekuwa karibu na jua kama sayari Venus, ukali wa joto usingevumilika. Kama tungekuwa mbali sana kama vile sayari Mars, tungeona theluji na barafu kila usiku, hata katika mikoa yenye joto.

Kama bahari zingekuwa nusu ya vipimo vyake vya sasa, tungepata tu robo ya mvua tunayoipata sasa. Kama zingekuwa moja ya nane ukubwa wake (bahari), kunyesha kwa mvua kungeongezeka mara nne zaidi, na dunia hii ingekuwa bwawa kubwa lisilokalika.

Maji huganda katika kipimo cha nyuzi 32 juu ya sifuri. Ingekuwa maafa kama bahari zingewajibika kwa sheria hiyo. Hata hivyo, kiwango cha ncha za baridi za mikoa zisingekuwa na uwiano, na barafu ingejikusanya kwa karne zote. Kuzuia balaa la jinsi hii, Bwana aliweka chumvi katika bahari kubadilisha kiwango chake cha kuganda.

***"tena mtaifahmu kweli, nayo hiyo kweli itawaweka huru"*** (Yohana 8:32).



# Pomboo Aongea

**David Everson**

Pomboo ni washirika wa kundi la kipekee sana la wanyama ambao Mungu ameweka uwezo fulani wa kushangaza. Wapo kwenye kundi la wanyama linaloitwa "Nyangumi wenye meno" au odontoceti [kundi la samaki wakubwa wenye meno] ambao wana uwezo wa kuwasiliana katika namna ambayo inakataa katakata maelezo yoyote mengine kuliko yale ya Mungu Muumbaji. Tuangalie kidogo kile ambacho Mungu ameumba ndani ya hawa mamalia.

Pomboo wanatumia uwezo wao wa kuwasiliana kwa sauti inayozalishwa na mapokezi, uongozaji katika giza na maji yenye giza, na kwa ajili ya eneo la chakula. Aina za mwito, mguno, sauti ya kutetemesha, sauti za kukoroma, sauti za kulia na miluzi vimeumbwa bila ya vitunga sauti (viungo vya mwilini vinavyofanya kazi ya

kutengeneza sauti, nyuzi-nyuzi). Kisanduku cha sauti, au zoloto (sehemu ya mwanzo ya koromeo inayohusika kutoa sauti), ya nyangumi wenye meno inakosa vitunga sauti, lakini inaonekana kuwa na uwezo wa kutengeneza baadhi ya sauti. Pia wana ukanda uitwao Vifuko vya sauti za Nazali. Eneo hili linamiundo maalum iitwayo misuli ya sphincter ambayo inahusika katika uzalishaji wa sauti. Sauti zenyewe uenda zinatengenezwa wakati hewa inaposukumwa katika mrija wa upepo na vifuko vya nazali za sauti. Wakati baadhi ya sauti za mitetemeko, Pomboo watatoa hewa kutoka shimo la kishindo, lakini wana sayansi wengi wanaamini hii ni kwa ajili ya matokeo ya kuona na sio lazima iunganishwe na kutengeneza sauti.

Sauti zinazalishwa katika marudio ya masafa ya hezi 0.25 hadi 150. Inaoneka kwamba masafa haya ya mapana ya sauti yanatumika na Pomboo kwa kazi mbalimbali. Masafa ya chini kabisa yanaonekana kuhifadhiwa kwa ajili ya mawasiliano ya kijamii na mengi yapo katika ukanda wa hezi 40. Marudio ya sauti ya juu katika vipimo vya mwaliko sauti vya hezi 40 hadi 150 huenda vinatumika kimsingi kwa ajili ya jambo fulani linaloitwa kipimo cha mwangwi. Mchakato huu unawawezesha nyangumi wenye meno na mamalia wengine wa baharini "kuona" kwa kutegemea "masikio" yao. Vifuko vinapeleka taarifa kwenye mifumo katika vichwa vyao ambayo inawawezesha kujua nini kilichopo mbele yao.

Paji la uso wa Pomboo lina eneo linaitwa tikiti ambalo limejaa mafuta. Vifuko vinapita kupitia tikiti, na inaonekana kufanya kazi kama dawa ya lenzi kufuatilia mawimbi ya sauti katika mhimili mwembamba. Halafu hii inasafiri kwenda nje katika maji karibia maili moja kwa sekunde. Halafu mhimili unagonga mbele ya Pomboo na kurudi kama mwangwi, pale ulipochukuliwa na mifupa ya taya ya chini iliyojaa. Halafu sauti hii inaongozwa katikati na halafu sikio la ndani kwa ajili ya kusikiwa katika kiini cha kusikizia cha ubongo.

Pomboo anaonekana kutambua kwa kusikia aina zake pendwa za chakula, na huenda hata "kuona" akilini kiwango cha picha ya chakula, yaani samaki anayetazamiwa kwa chakula. Uwekaji huu wa kipekee

wa viungo kwa ajili ya kuwasiliana na "kuona" unawapa wanyama hawa kutokuwa na uwezo wa kuongea kunakolingana.

Wakati inaelekea kwa wataalam wengi wa wanyama kwamba hakuna lugha kwa Pomboo, wanaweza kutambuana kwa ishara za kipekee za miluzi. Mluzi wa akina mama unaonekana kuwa ni endelevu kwa siku kadhaa kwa watoto baada ya kuwazaa ili kuwasaidia watoto hao kutambua na kujua mama yao alipo katika bahari kubwa.

Majike katika jamii ya Pomboo pia wanastaajabisha katika ukweli kwamba wanaweza kujitengenezea mitandao midogo ya ushirika. Mitandao hii inaonekana kuwa na uwezo wa kusafirisha maelezo kuhusu mazingira yao na mawasiliano mengine. Wana utata kama ilivyo katika kundi lolote la wanyama ambalo Mungu ameumba na wana ustaarabu kukaribia mtandao wowote wa binadamu au mfumo wa mtandao wa mawasiliano.

Na tumsifu Mungu kwa uumbaji wa kushangaza tunaoweza kuuona katika ulimwengu aliouumba kwa ajili yetu na upendo na tumtumikie Yeye katika siku zote za maisha yetu.

**David Everson ni mzee katika kanisa la Kristo Belington, Virginia Magharibi, Marekani na ana miaka mingi ya elimu ya baiolojia.**

# Je, Ulijua?

Mungu alimwambia Nuhu atengeneze safina ambayo ilikuwa na mita 300 urefu, upana mita 50, na mita 30 kwenda juu (miguu 450 urefu, miguu 75 upana, miguu 45 kwenda juu) (Mwanzao 6:15). Wajenzi wa Meli wamegundua kwamba marefu haya, mapana na kimo (30:5:3), ni sahihi kwa meli kubwa zinazohitaji kubeba mizigo bila ya kujali kasi ya kufika katika kituo.

# Maajabu Saba Ya Neno

Charles Pugh III



Wengi wamesikia kuhusu “Maajabu Saba ya Neno”. Kuna hitaji zaidi la kusikia kuhusu maajabu ya Neno (Biblia). Mtunga Zaburi aliomba, ***“Unifumbue macho yangu niyatazame Maajabu yatokayo katika sheria yako.”*** (Zaburi 119:18). Tena, alitangaza, ***“Shuhuda zako ni za ajabu,..”*** (Zaburi 119:129). Nimevutiwa na maajabu saba ya Neno yafuatayo.

1. **Maajabu ya UVUVIO!** Si kwa sehemu – sio tu mawazo – lakini “Kila Andiko lina pumzi ya Mungu” (2 Timotheo 3:16). Mpaka yodi (Herufi ndogo kabisa) na ndogo (mchomozo mdogo sana unaotofautisha herufi moja na nyingine), umevuviwa pia (Mathayo 5:18).
2. Maajabu ya UUNDAJI! Haikuja yote kwa mara moja, lakini kwa zaidi ya takribani miaka 1600. *“…Agizo juu ya Agizo, mstari juu ya mstari, hapa kidogo, pale kidogo”* (Isaya 28:10).

3. **Maajabu ya MUUNGANIKO wake!** Ni maktaba ya vitabu 66, bado ni KITABU KIMOJA, kilichoandikwa na waandishi 40 kwa makadirio ya zaidi ya miaka 1600, bado UJUMBE NI MMOJA (Ufunuo 19:10).
4. **Maajabu ya UFUNUO wake!** Biblia imekamilika, ufunuo wa mwisho wa **"mambo ya Mungu"** (1 Wakorintho 2:10-12) ambao ulikuja, si kwa **"mapenzi ya mwanadamu",** lakini watu watakatifu wa Mungu **"waliongozwa na Roho Mtakatifu"** (2 Petro 1:20,21).
5. **Maajabu ya MAELEZO!** Ni fasihi kuu katika ulimwengu, lakini zaidi imekusanya ***"vitu vyote vipasavyo uzima na utauwa,"*** (2 Petro 1:3). Hakuna nyongeza ya maelezo inayohitajika, kwa maana yanatosha kumkamilisha mtu apate kutenda kila tendo jema (2 Timotheo 3:17).
6. **Maajabu ya UENEZI!** Kusomwa na mataifa yote, matabaka, na kabila, ndicho kinachoongoza kwa mauzo duniani.
7. **Maajabu ya UHIFADHI!** Kitabu kinachochukiwa kuliko vyote, hata hivyo bado kinadumu. ***"Bali Neno la Bwana hudumu hata milele."*** (1 Petro 1:25).

***"Nitajifurahisha sana kwa amri zako, Sitalisahau neno lako."*** (Zaburi 119:161).


**Charles Pugh III ana huduma ya uandishi na anaishi Vienna, Magharibi ya Virginia, Marekani**

## Je, Ulijua?

**Aina mbalimbali za vifaa vimekuwa vikitumika kutunza kumbukumbu za maadiko. Watu walichonga maneno kwenye mawe wakitumia vipande vya chuma vilivyochongoka au jiwe lingine gumu. Udongo wa ufinyanzi ulichimbwa kwa jiwe lililochongoka au kwa kipande cha mti huku udongo ukiwa mnyevu. Milulu, mimea iliyopatikana kando ya maziwa na mito, ilitumika kutengeneza magombo. Haya yaliandikwa juu yake kwa kutumia aina fulani ya wino ulitokana na mimea au rangi. Ngozi za wanyama ziligeuzwa na kuandaliwa kwa ajili ya kutumika kwa kuandikia. Wino ulitumika pia kwa kuandika juu ya hizo. Vifaa vingine vilivyotumika katika karne nyingi kwa kuandikia ni pamoja na mbao, pembe, mfupa, na susu.**

# Kulitumia Neno kwa Halali kunahitaji Mafunzo Sahihi ya Biblia

David R. Kenney




Kuna mitazamo miwili inayokinzana kuhusu kujifunza Biblia. Mtazamo wa kwanza ni kwamba mtu wa kawaida hawezi kuelewa Maandiko bila ya msaada wa msomi/wasomi, wanazuoni, au kama wengine wanavyosema, "mlei (mtu wa kawaida) hawezi kuelewa Maandiko bila ya wachungaji (au mapadri)," hata ingawa Biblia haina makundi yanayoitwa "walei" au "weledi/wachungaji/mapadri". Mtazamo mwingine ni kwamba Biblia inaweza kusomwa kawaida na kueleweka vizuri. Ukweli uko baina ya mambo hayo mawili yanayokinzana, wote wanaweza kuelewa Biblia kama watakuwa tayari kuweka mbele juhudi sahihi. ***"Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali neno la kweli."*** (2 Timotheo 2:15). Kujitahidi kunahitaji juhudi, na msamiati "mtenda kazi" unazidi kuweka uzito katika hoja hii. Mtu ni lazima aweke juhudi sahihi katika kusoma Biblia na kujifunza kile

ambacho Mungu anataka yeye afanye ili ampendeze na kuokolewa katika siku ya mwisho. ***“kutumia kwa halali”*** inamaanisha kushughulikia kwa jinsi ipasavyo, kufundisha ukweli kwa usahihi, jambo ambalo linahitaji njia sahihi ya usomaji wa Biblia. Bila shaka Mungu anatutarajia tuwe wahudhuriaji katika maneno aliyotupatia kusoma na kujua.

Mwanafunzi wa Biblia lazima atambue vipindi vitatu ambavyo Mungu alishughulika na mwanadamu katika Biblia. Kipindi cha kwanza kilikuwa ni cha Wazazi/mababa (Mungu alishughulika na vichwa au viongozi wa familia); halafu kipindi cha Musa (pale Mungu alipompa sheria Musa pamoja na wana wa Israel); na sasa Ukristo/Neema (wakati Mwana wa Mungu alipoanzisha Agano Jipya kwa ajili ya wote). Agano Jipya ni sheria ambayo tutahukumiwa kwayo wakati huu. Baadhi wanachanganya maagano haya kimakosa na kuleta matendo kutoka Agano la Kale na kuyaingiza katika Agano Jipya. Haya ni maagano tofauti, sio nyongeza au marekebisho ya agano la kwanza.

Kujifunza kwa usahihi Biblia kunayahifadhi maagano haya na maagizo ambayo yanaambatana nayo katika mtazamo sahihi. Nyongeza, mtu lazima awe na mtazamo wenye mantiki katika Maandiko, akitambua kwamba kuna amri za kutii, mifano ya kufuata (au ya kuepuka, kulingana na muktadha), na vidokezo ambavyo vinatuonesha jinsi tunavyopaswa kumwabudu Mungu na kuenenda.

Moja ya kanuni zinazopuuzwa katika kulitumia Neno jinsi inavyopasa ni kuheshimu ukimya wa Maandiko. Wengine wanadhani kwamba kama Biblia haisemi hatuwezi kufanya kitu, halafu tunaruhusiwa kufanya jambo, lakini tunapaswa kuchunguza katika Biblia amri, mfano, au kidokezo ambacho kwa hiyo/hicho tunaweza kufanya jambo. Kwa maneno mengine, kama tukisema, “Biblia ipo kimya siwezi kutenda hili,” tunakosa shabaha. Swali sahihi ni, “Wapi katika Biblia inapokupa mamlaka wewe ya kutenda hili?” Fikiri Biblia ingekuwa kubwa kiasi gani kama Mungu angetuambia kila tendo ambalo hatukuruhusiwa kulifanya!

Sisi sote tunapaswa kujifunza Biblia ili kwamba tuweze kujionesha nafsi zetu kukubalika kwa Mungu.

**David R. Kenney anahubiri katika kanisa la Kristo Wadsworth, Ohio, Marekani.**

***"Kwa maana sisi si kama walio wengi, Walighoshio neno la Mungu; bali ka kwa weupe wa moyo, Kama kutoka kwa Mungu, mbele za Mungu, Twanena katika Kristo"***
(2 Wakorintho 2:17 KJV).



# Kitabu chake cha Thamani

**David A. Sargent**

Kilikuwa ni rafiki yake (huyo dada) wa daima. Alikisoma mara kwa mara. Alipenda kusikiliza watu wakikisoma, kukielezea kinaganaga, na kukizungumzia. Alikuwa mwepesi kukilinda kama mtu angekizungumzia vibaya. Kulikuwa na kurasa ngumu ya kitabu chake ambayo haikuwa na baadhi ya neno au virai vilivyowekewa alama au kupigiwa mstari. Aliandika mambo mengi katika pambizo kumsaidia kukumbuka maneno na mawazo ya kitabu chake cha thamani. Alidondoa kitabu chake kwa kadiri alivyoweza, ili abaki na maneno ikitokea kimechukuliwa mbali naye. Alitafuta kuyaishi maneno ambayo aliyasoma katika kitabu chake, kwa maana maneno yale aliyakubali kama mwongozo wa maisha yake.

> ***"Kina thamani kiasi gani Kitabu kitakatifu, kwa uvuvio kilichopewa! Kinaangaza kama taa maagizo yake yanang'aa, kuongoza roho yangu kwenda mbinguni."***

Familia yake inasema kwamba alianza kusoma, kujifunza, na kukifuata kitabu chake kwa dhati wakati yeye na mumewe walipompoteza mtoto wao mchanga, Betty Jane. Alihifadhi tarehe ya kuzaliwa na kufa kwa mtoto wake katika ukurasa mtupu wa kitabu chake, na kuandika maneno haya kando ya tarehe hizo; "Nina tumaini la uhakika nitakuona tena, mtoto wangu mpendwa. Hakuna kinachoweza kumtoa yeye kutoka kwa Kristo kwa sasa. Chipukizi la ua waridi linasubiri kuchanua huko mbinguni."

Alidumu kukigeukia kitabu chake miaka ya baadaye alipompoteza mtoto wake mkubwa, Patsy. Binti yake alikuwa mgonjwa wa kisukari na figo ilishindwa kufanya kazi. Wakati ilipoonekana kwamba upandikizaji wa figo pekee ndio ambao ungeweza kuongeza maisha ya binti yake, alitoa kwa ajili yake moja ya figo zake. Patsy aliishi miaka michache mpaka alipofariki katika umri wa miaka 42. Mama yake alipata faraja katika kitabu chake.

> ***"Kwa utamu kinachangamsha moyo wangu mdhoofu, katika giza la bonde hili la machozi; Nuru katika maisha yangu bado inanigawia, Na kuzima hofu zangu zinazoinuka."***

Alipenda kuwashirikisha wengine kitabu chake. Mwishoni mwa maisha yake, alikuwa na urafiki na mwanamke mwenye umri wa miaka 94 ambaye hakuweza kuona vizuri sana. Kwa kuwa rafiki yake hakuweza kuona vizuri, alimsomea kwa sauti kitabu chake. Aliwasomea kwa sauti kitabu chake wengine wengi.

Katika umri wa miaka 80, alikuwa na urafiki na mwanamke mwingine mwenye miaka 80, Nora, aliyeishi katika ghorofa moja naye. Alishirikiana kitabu chake na rafiki yake mpya. Walijifunza kwa pamoja. Haikuchukua muda Nora alikikubali kitabu kama mwongozo wa maisha yake.

> ***"Taa hii kupitia vitaabishi vyote vya maisha vya usiku, itaongoza njia yangu, hata nitakapoona vizuri nuru ya siku ya umilele."***

Jina lake lilikuwa ni Thelma Clark. Kitabu ambacho alikipenda kilikuwa, L.O. Sanderson kilochopewa jina la wimbo kuhusu kitabu hicho hicho, "Kitabu cha Thamani cha Uungu," Biblia.

> ***"Kitabu kitakatifu cha uungu! Hazina yangu ya thamani!***
> ***Taa ya miguu yangu na nuru ya njia yangu kuniongoza***
> ***salama nyumbani."***


Thelma Clark alikipenda kitabu kwa sababu ni Neno la Mungu. Kinazungumzia upendo mkuu wa Mungu ambao alimtuma Mwanawe kuja ulimwenguni kufa msalabani ili kwamba Thelma na sisi sote tuweze kuokolewa kutoka katika dhambi zetu na kupokea zawadi ya uzima wa milele (Yohana 3:16).

Thelma alipenda kuwaambia wengine kuhusu jinsi ya kupata zawadi ya wokovu na uzima wa milele kwa kufuata maelekezo yaliyotolewa katika kitabu: lazima tuweke imani yetu na kumwamini Yesu (Mdo 16:30-31), tukiziacha dhambi zetu kwa toba (Mdo 17:30-31), kumkiri Yesu mbele ya watu (Warumi 10:9-10). Na kubatizwa (kuzamishwa) katika Kristo kwa ajili ya kusamehewa dhambi zetu (Mdo 2:38). Halafu, kitabu kinapaswa kuendelea kuwa mwongozo wetu. "Taa ya miguu yetu na nuru ya mapito yetu" (soma Zaburi 119:105). Kwa maneno mengine, Kitabu kinatakiwa kuwa cha thamani kwetu kama kilivyokuwa kwa Thelma Clark.

Hutakigeukia Kitabu na kufuata maagizo yake?

**David A. Sargent anatumika kama mhudumu wa kanisa la Kristo Creekwood huko Mobile, Alabama, Marekani**

**"Katika kuipenda kumbukumbu ya Thelma Orene Thompson Clark, aliyezaliwa November 14, 1927 na kuondoka katika maisha haya kwenda katika nyumba yake (dada) ya milele tarehe 14 – 09 – 2015. Mashairi yaliyonukuliwa katika makala hii yanatoka kitabu "The Precious Book Divine" (Kitabu cha Uungu chenye Thamani) na L.O. Sanderson.**




1. Paulo alifikiri kwamba Mkristo anapaswa kufanya chochote wanachotaka maadam hakikuwa kibaya Kimaandiko (6:12). Kweli / Si kweli
2. “Mwili si kwa ______________ bali ni kwa _______,naye _________ ni kwa mwili” (6:13).
3. Mungu alimfufua Kristo, na tena __________ sisi (6:14).
4. Miili yetu ni ________________ vya Kristo (6:15).
5. Kwa kufanya uasherati, tunakuwa _________ mmoja na kahaba (6:16).
6. Ni aya gani anayoinukuu Paulo kuweka ushahidi kwa ajili ya maelezo ya juu yake (6:16)?
7. “Yeye ___________ na Bwana ni __________ moja naye” (6:17).
8. Kwa kufanya zinaa, Paulo anasema tunafanya dhambi dhidi ya nini (6:18)?
9. Paulo anasema kwamba miili yetu ni _____________ la Roho Mtakatifu (6:19).
10. Paulo anazidi kusema kwamba tume __________ kwa thamani, ikimaanisha kwamba sisi si mali yetu wenyewe (6:20).

11. Kwa kuwa miili yetu inamilikiwa na Mungu, inapaswa kutumiwa kwa kusudi gani (6:20)?

(Angalia kwenye gamba la nyuma ya kitabu kwa ajili ya majibu)

**12** Vitu vyote ni halali kwangu, lakini si vyote vifaavyo; vitu vyote
ni halali kwangu, lakini mimi sitatiwa chini ya uwezo wa kitu cho chote.
**13** Vyakula ni kwa tumbo, na tumbo ni kwa vyakula; lakini Mungu
atavitowesha vyote viwili, tumbo na vyakula. Lakini mwili si kwa zinaa,
bali ni kwa Bwana, naye Bwana ni kwa mwili. **14** Naye Mungu
alimfufua Bwana, na tena atatufufua sisi kwa uweza wake.
**15** Je! Hamjui ya kuwa miili yenu ni viungo vya Kristo? Basi
nivitwae viungo vya Kristo na kuvifanya viungo vya kahaba? Hasha!
**16** Au hamjui ya kuwa yeye aliyeungwa na kahaba ni mwili mmoja
naye? Maana asema, Wale wawili watakuwa mwili mmoja. **17** Lakini
yeye aliyeungwa na Bwana ni roho moja naye.
**18** Ikimbieni zinaa. Kila dhambi aitendayo mwanadamu ni nje ya
mwili wake; ila yeye afanyaye zinaa hutenda dhambi juu ya mwili wake
mwenyewe. **19** Au hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho
Mtakatifu aliye ndani yenu, mliyepewa na Mungu? Wala ninyi si mali
yenu wenyewe; **20** maana mlinunuliwa kwa thamani. Sasa basi,
mtukuzeni Mungu katika miili yenu.

**KUMBUKA:** katika sehemu hii ya Maandiko, Paulo alikuwa akiwakemea Wakorintho kwa tabia zao za zinaa. Aya ya 12 na 13 inaonekana kuwa na misemo ambayo Wakorintho walikuwa wakiitumia kutetea tabia zao za dhambi. Hata hivyo, uhuru wetu katika Kristo kwa namna yoyote hautupi kibali cha kutenda dhambi (angalia pia katika Warumi 6:1-4). Kama ilivyo kwa watu wengi leo, inavyoonekana Wakorintho walidhani tamaa yoyote ya kimwili ilikuwa ni sawa na haikuwaathiri kiroho kuliko chakula walichokula ili. Hivyo, walidhani kwamba zinaa

haikuwa kitu ila ni tamaa halisi ya kimwili na haikuwa na athari katika upande wa kiroho wa mtu.

Hoja ya juu ni dhana ya uongo kwa sababu miili yetu ni zaidi kuliko tu kuwa maghara ya kimwili kwa ajili ya roho zetu. Kwa njia ya ufufuo wa Kristo, miili yetu itaishi milele. Paulo alifafanua kwamba pindi tunapofanya zinaa, tunakuwa mwili mmoja na kahaba, lakini sisi kama Wakristo tumekuwa mwili mmoja na Bwana. Hiyo inamaanisha pindi tunapofanya zinaa, pia tunafanya uzinifu wa kiroho.

Tunapaswa kutambua kwamba tumenunuliwa kwa damu ya Yesu, kama mtumwa alivyonunuliwa katika mnada wa watumwa wa kale; kwa hiyo, hatujimiliki wenyewe. Sasa tunamilikiwa na Mungu, na kazi yetu ni kumtukuza Mungu katika miili yetu na kwa roho zetu. Roho wa Mungu sasa anaishi ndani yetu, sasa tunawezaje kufikiri kuhusu kulichafua hekalu lake (1 Wakorintho 3:17). Kila kitu tulichonacho pamoja na sisi wote ni mali ya Mungu; hivyo, daima tupambane kumtukuza Mungu.

# Kitabu cha Uzima cha Mwana-kondoo

**David R. Pharr**

Kama Yesu alivyojiandaa kwa safari yake ya mwisho kwenda Yerusalemu, aliwachagua watu sabini miungoni mwa wanafunzi wake wamtangulie kuandaa ujio wake. Alionya kwamba kungekuwa na upinzani. Wangekuwa kama ***"kondoo katikati ya mbwa mwitu".*** Walipewa nguvu kubwa katika jina la Kristo waweze kutoa pepo na kuponya wagonjwa (Luka 10:1-).

Ilitarajiwa kwamba wafuasi wote wa Kristo wangekuwa na furaha kuu juu ya mafanikio katika huduma. Hivyo, pindi wale sabini waliporudi, walikuwa na taarifa ya kufurahisha, wakisema, ***"Bwana hata pepo wanatutii kwa Jina lako."*** Yesu alijua matendo makuu ambayo yalikuwa yamefanyika. Roho waovu hawakuweza kuwapinga. Hata hivyo, Yesu aliwachagua kwa jambo fulani bora zaidi kuliko hata kufanya miujiza. Alisema, ***"Lakini, msifurahi kwa vile pepo wanavyowatii; bali furahini kwa sababu majina yenu yameandikwa mbinguni."*** (Luka 10:17-20).

Jambo la kujifunza ni kwamba kuna jambo lililo bora kuliko hata kuwa na uwezo wa kutenda matendo makuu. Ni uhakika uliotolewa kwa kila mtoto mwaminifu wa Mungu kwamba jina lake liko katika Kitabu cha Uzima ambapo jina lake limeandikwa mbinguni. Kuhusiana na mbinguni, mji mtakatifu, Yohana aliandika, ***"Na ndani yake hakitaingia kamwe cho chote kilicho kinyonge, wala yeye afanyaye machukizo na uongo, bali wale walioandikwa katika kitabu cha uzima cha Mwana-Kondoo."*** (Ufunuo 21:27).

Ukweli ni kwamba majina yapo katika Kitabu cha Uzima na Biblia inatuambia kwamba Mungu anamjua killa mmoja wetu kwa undani;

Anatujua kwa majina. Kuweka mkazo wa kumjali Musa, Bwana alisema, ***“Nakujua jina lako”*** (Kutoka 33:17). Yesu alijiita kama ***“Mchungaji Mwema”,*** akisema, ***“Anawaita kondoo zake kwa majina”*** (Yohana 10:3). Paulo aliwataja washirika wake katika kazi huko Filipi, ***“ambao majina yao yapo katika Kitabu cha Uzima”*** (Wafilipi 4:3). Katika waraka wake kwa kanisa la Sardi, Kristo aliwahakikishia akisema ***“Lakini unayo majina machache katika Sardi, watu wasioyatia mavazi yao uchafu. Nao watakwenda pamoja nami hali wamevaa mavazi meupe, …sitalifuta kamwe jina lake katika kitabu cha uzima, nami nitalikiri jina lake mbele za Baba yangu, na mbele ya malaika zake”*** (Ufunuo 3:4,5).

Hivyo Mungu anatujua kwa majina pia inatukumbusha kwamba wokovu sio ushirika, bali ni wa mtu binafsi. Kitabu cha Uzima hakina orodha ya majina ya mataifa, koo, au hata makanisa, bali ni mtu mmoja mmoja. Ndiyo, watu waliookolewa ni washirika wa Kanisa la Kristo, lakini wokovu unapokelewa kama matokeo ya imani na utii wa mtu binafsi (1 Petro 1:22). Yeye ambaye anapokelewa mbinguni hatakuwa kule kwa sababu jina lake la ukoo ***“liliandikwa mbinguni”*** wala si kwa sababu alidai kuwa ni mshirika wa kanisa, bali ni kwa sababu ya uhusiano wake binafsi na Bwana.

Inahitajika isisitizwe kwamba Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo kina orodha sahihi na hakika. Mungu anajua vizuri hasa majina ya kuandika. ***“Bwana anawajua walio wake”*** (2 Timotheo 2:19). Hakuna makosa katika Kitabu cha Uzima, hakuna majina yatakayojumuishwa ambayo si ya huko na hakuna litakaloachwa ambalo linapaswa kuwepo huko. Kuna matabaka mawili tu ya watu. Watu waliozaliwa tena na wasiozaliwa tena, watu wa kanisa na watu wa dunia, watu waliosamehewa dhambi na watu wanaoishi katika dhambi, watu ambao majina yao yapo katika Kitabu na watu ambao majina yao hayakuandikwa.

Majina yanaandikwa katika kuzaliwa, kuzaliwa upya, hiyo ni wakati mtu anapozaliwa tena (Yohana 3:1-7; 1 Petro 1:23; Wagalatia 3:26,27). Tunaweza kujua kama majina yetu yameandikwa katika Kitabu cha

Uzima cha Mwana-Kondoo huko mbinguni kwa kile tunachoamini na kile tunachofuata katika Kitabu tulichonacho katika dunia, Biblia.

Pia ni muhimu kujua kwamba majina yaliyoandikwa yanaweza kufutwa. Wale ambao ni waaminifu katika kuishinda dhambi majina yao hayatafutwa (Ufunuo 3:5). Hata hivyo, kuna onyo la kutisha kwamba ***"Na mtu ye yote akiondoa lo lote katika maneno ya unabii wa kitabu hiki, Mungu atamwondolea sehemu yake katika ule mti wa uzima, na katika ule mji mtakatifu, ambao habari zake zimeandikwa katika kitabu hiki." (***Ufunuo 22:19). Yohana aliandika kuhusu maono yake ya hukumu ya mwisho: ***"Nikawaona wafu, wakubwa kwa wadogo, wamesimama mbele ya hicho kiti cha enzi; na vitabu vikafunguliwa; na kitabu kingine kikafunguliwa, ambacho ni cha uzima; na hao wafu wakahukumiwa katika mambo hayo yaliyoandikwa katika vile vitabu, sawasawa na matendo yao….. Na iwapo mtu ye yote hakuonekana ameandikwa katika kitabu cha uzima, alitupwa katika lile ziwa la moto."*** (Ufunuo 20:11-15).

**David R. Pharr ni mhubiri huko Rock Hill, Kusini mwa Carolina, Marekani.**

# SWALI KUU: IPI?

Carroll Sites

Maisha yamejaa maamuzi. Baadhi ni makubwa na baadhi ni madogo. Baadhi ni muhimu sana, na baadhi si muhimu sana. Baadhi yatakuwa na tija katika maisha ya mtu na baadhi yatakuwa na tija katika hatima ya mtu. Jinsi tunavyojibu **SWALI KUU – IPI –** ni kwa maamuzi tunayoyafanya. Tafadhali zingatia yafuatayo kwa umakini sana na ufanye maamuzi sahihi.

- Kuna njia mbili za kuianza siku – kwa maombi, au bila ya maombi. Ulianza na moja kati ya njia hizi mbili. Ipi?
- Kuna njia mbili za kuitumia Siku ya Bwana – kukaa au kuabudu. Ulitumia Siku ya Bwana njia moja kati ya hizi mbili. Ipi?
- Kuna matabaka mawili ya watu katika ulmwengu – waliookolewa na wasiookolewa. Upo katika moja ya matabaka haya mawili. Lipi?
- Kuna mabwana wawili wakuu katika ulimwengu – Mungu na Shetani. Unamtumikia mmoja wa hawa mabwana wakuu. Yupi?
- Kuna njia mbili ambazo zinatuongoza kupitia muda na umilele – njia pana na njia nyembamba. Unapita katika njia mojawapo ya hizi mbili. Ipi?
- Kuna vifo viwili ambvyo watu hufa, baadhi ***"wanakufa katika Bwana"*** wakati wengine ***"wanakufa katika dhambi zao".*** Utakufa katika moja ya hivi vifo. Kipi?
- Kuna sehemu mbili ambazo watu uenda – mbinguni au motoni. Utaenda katika moja ya sehemu hizi mbili. Ipi?

Je, kuna mabadiliko yoyote yanayotakiwa kufanywa katika maisha yako? Unapanga kuyafanya? Lini? Unapanga kwenda mbinguni? Jinsi unavyojibu maswali haya huenda yakaamua kwa njia uliyojibu **SWALI KUU – IPI!** Biblia inaongea wazi kabisa: ***"Hii ndiyo jumla ya maneno; yote yamekwisha sikiwa; Mche Mungu, nawe uzishike amri zake, Maana kwa jumla ndiyo impasayo mtu."*** (Mhubiri 12:13).

**Carroll Sites ni mzee (askofu) na mhubiri wa kanisa la Bwana huko Higden, Arkansas, Marekani.**

# Na Hakutakuwa na Usiku Kule

**Ardron Hinton**

Hili wazo, hasa katika maelezo ya *"nchi mpya"* (Ufunuo 21:1) linaweza kuwa ni fumbo kwa mtazamo wa kwanza. Kuondokana na vitu kama dhambi, ugonjwa, na kifo inaonekana kirahisi kama baraka, lakini kwa nini kuuondoa usiku? Hebu tutafakuri kuhusu hilo (Ufunuo 21:25).

## Giza la usiku linaathiri kihalisia:

- Linakuza matatizo yetu.
- Linakuza hofu zetu.
- Linafifisha na kuharibu maono yetu.

## Giza la usiku kwa zaidi linahusiana na kumbukumbu za tabu:

- Linahusishwa na uchovu, nyakati za kulala zisizokoma.
- Linahusiana na sauti ya maumivu binafsi.
- Linahusiana na kurefushwa masaa ya mkesha kitandani.

## Giza la usiku lina maana iliyojificha kwa waumini:

- Linatumika kuelezea ukosefu wa maarifa.
- Linatumika kuelezea maisha ya kikwazo na kukosa dira.
- Linatumika kuelezea ulimwengu wa uovu uliofichika katika ulimwengu.

## Giza la usiku lina utamaduni ambao hautahitajika tena:

- Linatoa ishara ya mwisho wa siku za uchovu na kuleta taraja la pumziko.
- Linashikilia mwanga wa matumaini, pindi linapopita, kwa siku bora ya kesho.
- Linasitiri wingi wa ubaya wa siku chini ya gamba la nyota zake.



Tutawekwa huru kutoka katika mazingira yanayozunguka shida za usiku na mafumbo ya giza, na hatutakuwa na uhitaji wa faida zake za sasa kwa kuwa hatutakuwa na matatizo. Hata hivyo, sababu ya msingi ya kutokuwepo kwa usiku katika *"nchi mpya"* haipatikani katika hizi picha zinazoletwa kutoka katika andiko, lakini ni kwa maelezo ya uwazi ya hilo. Aya hii pia inatuambia hakuna jua katika *"nchi mpya",* na ni uhusiano wa jua na mzunguko wa dunia ambao unasababisha usiku na mchana. Chanzo cha nishati haitakuwa dhahiri, Mungu aliumba jua, lakini moja kwa moja katika njia halisi – Muumbaji – chanzo cha mwisho cha nishati zote yuko pale (Ufunuo 21:23).

Watu wengi wanaona hili gumu kuliona kutoka uumbaji hadi kwa Muumbaji nyuma ya hili. Lakini kwa muumini, tarajio la kuondoka mbali na upeo, ila ni kwa muda tu, kuelekea katika kisichoonekana, ni umilele ni matarajio yenye nguvu zaidi katika akili ya mwanadamu. Msimamo wa Wakristo katika ufufuko wa ushirika wa mwisho wa usiku, ulimwengu wa kifo, na kutazamia mbali ya hilo kuelekea kwenye uwepo wa Mungu na mwangaza wake wa kudumu. ***"Hakutakuwa na usiku kule."***


**Ardron Hinton (1929 – 2015) alikuwa mhubiri wa Injili na mwalimishaji aliyeishi huko Blair, Oklahoma, Marekani.**



# Jipime na Biblia

Louis Rushmore

1 Mji wa Filipi
2 Kuhani mkuu wa kwanza
3 Jiwe nusu la thamani
4 Mtu wa kwanza
5 Kutupwa kwenye tunuri
6 Makanisa saba ya………………..
8 Baba wa iman
10 Nabii mdogo
11 Mji uliowashinda Waisraeli
12 Mjumbe wa mbinguni
13 Samani ya kutolea dhabihu
14 Nchi ya mashariki mwa mto
 Yordani
inayoelea/tembea




**Chini**
1 Manukato ya thamani
2 Kwanza waliitwa Wakristo hapa
4 Mume wa Sarai
7 Mji wa Filipi
8 Kitabu cha historia cha Agano Jipya
9 Mwana wa Daudi
12 Bustani ya wanyama inayoelea/tembea

# Kisababishi cha Ukuaji wa Kanisa

Wayne Barrier

Ukuaji wa kanisa unapaswa kuwa ni kipaumbele kwa kila kusanyiko. Kama kanisa lina uaminifu kwa Bwana kuhusiana na agizo la kueneza Injili kwa kila taifa na kila mtu juu ya dunia, kuwabatiza wale waliotii (Mathayo 28:18-20), hapo matokeo yake ni ukuaji. Maelezo zaidi ya matakwa kwa ajili ya ukuaji wa kanisa yanapatikana katika Waefeso 4:1-16. Kifungu hiki kinaishia na aya ya 16 ikianza kitu kinachosababisha *"ukuaji wa mwili".* Kama tukichunguza kifungu hiki, tunaweza kutambua mambo mbalimbali yanayohitajika kusababisha ukuaji.

Kwanza, aya kadhaa zinarejea ulazima wa fikra na tabia ya washirika wa kanisa ambayo inawezesha wao kuchangia katika ukuaji. Haya kujumuisha unyenyekevu, upole, uvumilivu, kuchukuliana kwa upendo, kuzungumza ukweli kwa upendo, na utayari wa kufanya kazi. Baadaye katika Waefeso 4:31-32, Paulo aliandika, ***"Uchungu wote na ghadhabu na hasira na kelele na matukano yaondoke kwenu, pamoja na kila namna ya ubaya; tena iweni wafadhili ninyi kwa ninyi, wenye huruma, mkasameheane kama na Mungu katika Kristo alivyowasamehe ninyi."***

Baadaye, Paulo aliorodhesha sehemu saba za umoja kwa ajili ya mwili wa Kristo. Aliandika katika Waefeso 4:4-6***, "Mwili mmoja, na Roho mmoja, kama na mlivyoitwa katika tumaini moja la wito wenu. Bwana mmoja, imani moja, ubatizo mmoja. Mungu mmoja, naye ni Baba wa wote, aliye juu ya yote na katika yote na ndani ya yote."*** Ni wazi kuna mengi ambayo ni lazima yaeleweke kupitia umakini na

ufahamu wa kujifunza Maandiko yote (2 Timotheo 3:16,17) kabla ya sisi kufafanua sehemu moja ya hizi saba za umoja. Hatuwezi kufanikisha hitaji hili bila ya kuchukulia uzito, kujifunza Biblia kwa kina. Wengi wanaamini mafunzo machache ya Biblia na kuwa na maarifa ya Biblia yenye ukomo. Kwa urahisi wanaweza ***"…kuchukuliwa na kila upepo wa elimu, kwa hila ya watu, kwa ujanja, tukizifuata njia za udanganyifu."*** (Waefeso 4:14).

Mwishowe, sisi wote ni lazima tuwe watenda kazi, kila mmoja akifanya kwa sehemu yake kuujenga na kuukuza mwili (Waefeso 4:16). Kanisa linapaswa kufundishwa na mitume na manabii. Maneno yao (Biblia) yamehifadhiwa kwa ajili ya mwongozo wetu. Leo wainjilisti, wazee, na waalimu wanatoa uongozi na kufundisha ambapo humjenga kila Mkristo kwa ajili ya kazi ya huduma (Waefeso 4:11,12). Kila mshirika ana uwezo tofauti, nguvu, vipaji, na vipawa. Kila mmoja ni lazima aendeleze kazi ya huduma kwa kutegemea sifa mahususi za kiasili za mtu, fursa, na tabia. Kama tulivyo kila mmoja tukifanya kwa sehemu yetu, tukitenda kazi kuhudumia mwili wa Bwana, kanisa litajengwa na litakua. Kanisa ni mwili muhimu zaidi katika ulimwengu huu. Kanisa ni mkusanyiko wa waliookolewa kutoka katika dhambi na waliotayari kwa maisha ya umilele huko Mbinguni. Ukuaji wa kanisa ni mgumu, lakini inawekana kwa njia ya utekelezaji wa mwongozo uliotolewa na Biblia. Aya hizi rahisi zina mwongozo wenye nguvu sana kwa ukuaji.

**Wayne Barrier anaishi Florence, Alabama, Marekani, na anafanya kazi za umisionari katika nchi mbalimbali**

# Je, Ulijua?

Maandiko pekee ya kale 643 ya *Illiad* yaliyogunduliwa na Homer yamesalimika hata leo. Kulinganisha na magombo 5,366 ya Agano Jipya yaliyosalimika. Ni katika Agano Jipya ambapo mtu hupata maelezo ya kutosha yaliyo halalishwa kuhusu Kanisa, utimilifu wa yote Agano la Kale (Isaya 2:2,3), na Agano Jipya (Mathayo 16:18), unabii kuhusu kuanzishwa kwake (Yoell 2:28-3:2; Mdo 2:16-21, 47).

# Wasifu kutoka Makaburini

Bobby Dockery

Nje kidogo mwa mji wa Rumi, kuna mfumo wa mahandaki chini ya ardhi takribani 60 yakijulikana kama "Makaburi". Mahandaki, yanayofikia upana wa miguu 5 na urefu kwenda juu miguu 8, yenye mfumo wa njia za kuchanganya (kumpoteza mtu) pakutokea zenye maili 600 za chini ya ardhi. Makaburi mengi yalichimbwa na Wakristo katika kipindi cha adha na yalitumika kama sehemu za makimbilio, kuabudia, na maziko wakati upinzani wa Rumi ulipokuwa mkali.



Makaburi yanasimulia hadithi ya wazi ya kuogofya ***"majaribu ya kutisha"*** ambayo yalijaribu imani ya wale watakatifu wa awali (1 Petro 4:12). Inakadiriwa kwamba Wakristo mashahidi milioni 4 mpaka 7 walizikwa katika Makaburi hayo katika kipindi cha karne ya kwanza na ya pili. Wakati vilio vya hawa watakatifu wa awali vilipokuwa wazi, ushahidi wa kutosha wa kusikitisha wa magaidi waliouvumilia kwa ajili ya Kristo ulionekana katika mifupa yao iliyokatwa kikatili.

Katika sura ya mateso hayo, tungeweza kutarajia imani ya Wakristo hawa wa awali kuwa na mashaka. Badala yake, maelezo yaliyochukuliwa kutoka katika makaburi yao ni kumbukumbu kwa kudumu kwao katika ujasiri na tumaini katika Kristo. kumbukumbu moja inasomeka, ***"Hapa analala Marcia, aliyewekwa kwenye pumziko katika ndoto ya amani"***

Nyingine inabeba ushuhuda mwepesi, ***"Washindi katika amani na katika Kristo"***. Bado nyingine inatangaza, **"Kwa kuitwa mbali, alienda kwa amani".**

Waliwezaje hawa Wakristo wa awali kuwazika wapendwa wao kwa uhakika wa utulivu huo? Waliwezaje kusema kwa ujasiri wa amani na tumaini wakati wakiwa chini ya ardhi katika hali ya ukandamizaji wa jinsi hiyo usiozungumzika? Nini ilikuwa siri yao? Waliendelezaje imani kuu namna iyo?

**Waliziimarisha imani zao kwa kusoma Neno la Mungu**. Hawa Wakristo waligundua kwamba ***"imani huja kwa kusikia na kusika kwa neno la Mungu"*** (Warumi 10:17). Kwa hiyo, ***"walidumu katika fundisho la mitume"*** (Matendo ya mitume 2:42). Walitumia kila fursa kusoma na kujifunza Maandiko. Nia yao katika kujifunza Neno la Mungu inaelezewa vizuri na mtume Paulo ambaye aliagiza ***"vitabu vyake na vile vya ngozi"*** kutokea jela ili kwamba aweze kuendelea kujifunza Maandiko ya Agano la Kale hata katika ***"mstari wa kifo"*** (2 Timotheo 4:13).

**Waliziimarisha imani zao kwa kukusanyika pamoja.** Walikutana pamoja kila mara kwa vipindi vya ibada na tafakuri. Wakati mateso yalipokuwa ya kikatili sana ambapo hawakuweza kukutana tena katika jumuiya na nyumba kwa nyumba, walikusanyika katika Makaburi. Pale, palizungukwa na giza na kifo, waliimba mashairi yao ya ushindi ya imani na tumaini. Uamuzi wao wa kutokuacha kukusanyika pamoja ulikuwa sababu ya msingi katika ujenzi wa imani yao.

**Waliziimarisha imani zao kwa kutiana moyo.** Kwa kutambua mahitaji yao kwa ***"kuonyana kila siku***" (Waebrania 3:13), walitafuta ushirika wa kila mmoja ili kwamba waweze ***"kuchocheana***

***katika upendo na matendo mema”*** (Waebrania 10:25). Walipata ujasiri wa kuishi kwa uaminifu ili wawe vielelezo na maonyo kwa ndugu zao kaka na dada katika Kristo. Kifungo cha ushirika kiliwaleta karibu kwa mtu na mtu na karibu na Kristo.

Kulikuwa na imani ambayo ilishinda ulimwengu kwa sababu walijua kwamba ***“Yeye aliye ndani yenu ni mkuu kuliko yeye aliye katika dunia”*** (1 Yohana 4:4). Je, imani yako inahitaji kuchochewa? Basi jifunze kutoka katika imani iliyoandikwa katika kumbukumbu za Makaburini!

**Bobby Dockery ni mwandishi na mhubiri anaishi Fayetteville, Arkansas, Marekani**

# "Upendo wa ndugu Na udumu" Waebrania 13:1

**Cecil May Jr**



***"Upendo wa ndugu"*** katika kifungu hiki kinatafsiri Filadelfia (Philadelphia) (sawa na jina la mji), muungano wa Maneno mawili, moja kwa ajili ya aina fulani ya upendo na moja kwa ajili ya ndugu.

*Agape* katika Agano Jipya kwa kawaida huzungumzia upendo ambao hauhitaji chochote cha kupendwa katika wale wanaopendwa (Warumi 5:8). Ni jambo la hiari kutenda wema kwa wale wanaopendwa kuliko kuwa na hisia nzuri na laini kwao (Mathayo 5:44,45).

*File,* kwa upande mwingine, una ashiria urafiki, upendo wa ndugu. Huo upo kwa sababu ya kitu fulani kila mshirika katika mahusiano anapata furaha au kuridhika katika mwingine. Nje ya ulimwengu wa dini, tunapata ***"marafiki wa mchezo wa gofu",*** na ***"marafiki wavuvi".*** Hoja ni, kuna vitu watu wanafurahia kuvifanya, na wanafurahia kuvifanya kwa pamoja kuliko kufanya kila mmoja peke yake. Kama matokeo ya kile wanachoshirikiana, wanapendana (file). Mhubiri mmoja alizoea kuhubiri umoja, akisema, ***"Fundisho hugawa; upendo huunganisha, kwa hiyo acha tupendane na kusahau kuhusu fundisho."*** Jambo moja lisilo sawa katika hilo ni kwamba liko vibaya.

Umewahi kuwa na uzoefu, kama nilionao, wa kuwa katika mkusanyiko mkubwa, katika mkutano, na kujifunza kwa ghafla kwamba mtu mwingine katika umati alikuwa Mkristo mwenzako, au kama ambavyo tungesema, ***“mshirika wa kanisa”?*** Je, hatuhisi mshikamano kwa haraka kwa ajili ya mtu huyo, hatukujihisi hivyo hapo kabla, na bado hatukujihisi hivyo kwa mtu yeyote mwingine katika umati? Pindi tulipoonana baadaye, tulitafutana, ili tukae pamoja au kula pamoja. Nini kilichotuleta pamoja? Maoni yangu ilikuwa ni upendo wa ndugu, file, lakini ulizaliwa na nini? Ingeweza kuwa nini ila ni imani ya kawaida tunayoshiriki?

Upendo tulionao kwa ajili ya ndugu zetu kaka na dada katika Kristo, upendo ambao si sawa na upendo wa agape tunaotakiwa kuwa nao kwa ajili ya wageni na maadui, bali upendo ambao unajumuisha kuheshimiana kwa upendo na furaha ya ushirikiano unategemea katika utambuzi ambao sisi ni wamoja katika Kristo, ambapo tunakusanyika katika siku ya Bwana kuizunguka meza moja, ambapo tunaye ***“Bwana mmoja, imani moja, ubatizo mmoja”***

Mara niliposajiliwa katika hoteli ambayo mavetelani wa Vita vya 2 vya Dunia wa 82 Airborne walifurahia kuungana tena. Upendo wa wazi, heshima ya pamoja, na urafiki waliokuwa nao kila mtu na mwenzake ulikuwa na nguvu ya mfano wa huduma na upendo ambao Wakristo wanapaswa kuwa nao kwa ajili ya wao kwa wao kama washirika wa mwili wa Kristo. Hata hivyo, kutokuwepo kwa imani yoyote, kusikia kokote, au kuijua Injili, fundisho lolote kuhusu au kutoka kwa Kristo, ndio hasa tumgekuwa nao kama ***“tukisahau kuhusu fundisho na kupendana sisi kwa sisi.”*** Si Ukristo. Sio kanisa. Sio ushirika wa waliokombolewa.

Vyote upendo na fundisho vinahitajika, lakini ni imani ya kawaida na fundisho tunaloshiriki ambavyo huzaa upendo maalum kama ndugu kaka na dada ambao tunaufurahia.

**Cecili May Jr. mkuu mstaafu wa wanawake kitengo cha Biblia katika Chuo kikuu cha Faulkner huko Montgomery, Alabama, Marekani**

# Moja ni Nzuri kama Nyingine?

**Bill Dillon**



Wanaume wawili walikuwa wanaongea kwa ucheshi kuhusu sifa za magari waliyotoka kununua, kila mmoja alikuwa akitoa sababu kwa nini alifikiri kuwa gari yake ni bora kuliko nyingine.

Rafiki wa heshima akatokea, wakajaribu kumuingiza katika ubishani wao wa kirafiki***. "ni gari gani ambayo ungependa kuwa nayo?"*** waliuliza.

Kwa kutokutaka kuingizwa katika mashindano, alisema tu, ***"Ah, sijui. Nadhani moja ni nzuri kama nyingine."***

***"Moja ni nzuri kama nyingine?"*** labda kwa kuzingatia baadhi ya vitu, lakini kwa kweli si vitu vyote. Mume mmoja au mke ni mzuri kama mwingine? Nyumba moja ni nzuri kama nyingine, au chakula kimoja ni kizuri kama kingine?

Biblia inafundisha kwamba Yesu alijenga kanisa, akilinunua kwa damu yake mwenyewe yenye thamani (Mdo 20:28). Hilo ndilo kanisa ambalo tunahitaji kuhusika nalo. Mtu anaongezwa katika kanisa hili kama anavyoonesha upendo wake kwa Yesu na kutii amri zake. Wewe upo wapi, katika kanisa la Bwana, au lingine?

**Bill Dillon anahubiri katika kanisa la Bwana huko Cotter, Arkansas, Marekani.**

# Kumwita Bwana

Owen D. Olibricht

Kifungu pendwa kinachonukuliwa na wahubiri wengi ambao huwaambia watu nini cha kufanya ili waokolewe ni kutoka kwa nukuhu ya Paulo kutoka kwa Yoeli katika kitabu cha Warumi ***"Kwa kuwa, kila atakayeliitia Jina la Bwana ataokoka"*** (Warumi 10:13). Petro pia alinukuu kifungu hiki katika Siku ya Pentekoste (Mdo 2:21).

## Maana ya "Kuitwa"

Tunatumia neno ***"wito"*** kwa maana nyingi tofauti tofauti. Ananiita (mwanamke) (simu) mara kwa mara. Mwamuzi Yoeli anaita mipila na kupiga katika michezo ya baseball. Mchezo uliitwa kwa sababu ya mvua. Miito mikuu kwa ajili ya msaada;  anaweka ombi kwa ajili ya msaada.

Lugha ya Kigiriki ina maneno tofauti tofauti ya neno ***"wito". "Wito"*** (Mdo 2:21); Warumi 10:13) ni tafsiri ya neno kundi (compound word) ***"juu ya"*** (upon) na ***"wito"*** (-ita), ambayo inamaanisha kumpa mtu fulani jina (la ukoo) (Mathayo 10:2),  kukata rufaa kwa mtu fulani, kama vile kwa Kaisari (Mdo 25:11), na kuitwa kwa jina (Yakobo 2:7). Hakuna muktadha wa wazi unaoonesha maana ya wito kama "kusali", kama inavyofundishwa na wengi ambao wanaamini katika wokovu kwa kupitia sala pekee.

## Wayahudi katika Siku ya Pentekoste

Baada ya Petro kunukuu maelezo ya Yoeli, ***"kwa kuwa, kila akayeliitia Jina la Bwana ataokoka"*** (Mdo 2:21), watu walimwuliza nini walichohitajika kufanya (Mdo 2:37). Petro hakurejea maelezo ya Yoeli ambayo aliyanukuu na kuwaambia waombe katika jina la Bwana, badala yake aliwaambia ***"Tubuni…na mbatizwe katika jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi"*** (Mdo 2:38). Ni dhahiri ***"kuliitia***

***jina la Bwana"*** haikumaanisha **"sala",** au Petro angeweza kuwaambia waseme **"sala ya toba**", sala ambayo haipatikani popote katika Biblia. Badala yake aliwaambia wale walioamini ***"Tubuni…na kubatizwa katika jina la Yesu Kristo."***

## Kornelio

Malaika alimwambia Mmataifa Kornelio atume mtu kwenda Yafa kumwita Petro ***"atakayekuambia maneno ambayo yatakuokoa, wewe na nyumba yako yote"*** (Mdo 11:14). Pindi Petro alipokuja nyumbani kwa Kornelio, aliwahubiri Yesu. pindi Roho Mtakatifu aliposhuka juu yao, kuonesha kwamba watu wa mataifa wangeweza kuokolewa katika namna ile ile kama Wayahudi (Mdo 15:7-9), Petro ***"aliamuru wabatizwe katika jina la Bwana"*** (Mdo 10:48), badala ya kuwaambia wasali.

## Paulo

Wakati Yesu alipomtokea Paulo, alimwambia ***Paulo, "Lakini simama, uingie mjini, nawe utaambiwa yakupasayo kutenda".*** (Mdo 9:6). Paulo alienda katika mji ambapo ***"hakula wala kunywa"*** kwa siku tatu (Mdo 9:9) na kuendelea katika kusali (Mdo 9:11).

Yesu alimtuma Anania kwa Paulo. Anania alipokuja kwa Paulo, hakumwambia aendelee katika kuomba. Badala yake akamwambia, ***"Basi sasa, unakawilia nini? Simama, ubatizwe, ukaoshe dhambi zako, ukiliitia jina lake."*** (Mdo 22:16). Dhambi za Paulo hazikuondolewa alipokuwa akiomba kwa siku tatu bali pindi alipobatizwa, na kuliitia jina la Bwana.

## Ombi Letu

Pindi tunapobatizwa, msamaha wetu upo katika jina la Yesu, ikimaanisha ombi letu kwa ajili ya kusamehewa linategemea mamlaka yake. Tunatakiwa kufanya yote katika jina la Yesu, kulingana na mamlaka yake (Wakolosai 3:17). Sababu ya kuomba kwetu katika jina lake ni ***"Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu***

***litupasalo sisi kuokolewa kwalo."*** (Mdo 4:12). Kama tukibatizwa katika jina la Yesu, kwa mamlaka yake, tutabatizwa kulingana na maelekezo aliyowapa wanafunzi wake alipowatuma kwenda ulimwenguni pote. Tunasoma ***"Yesu akaja kwao, akasema nao, akawaambia, Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari."*** (Mathayo 28:18-20).

Kama ubatizo wetu upo katika jina la Yesu, kwa mamlaka yake, utakuwa katika jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu.

**Owen D. Olibricht ni mhubiri na mwandishi anayeishi Sherwood, Arkansas, Marekani**

# Je, Ukweli Unajalisha?

**Bobby Key**

Katika mji ulio mbali kutoka sehemu unayoishi kuna wakati waliishi wanaume wawili. Wanaume hao walikuwa ni watu wa dini sana. Wote walikuwa wacha-Mungu. Hata hivyo, majirani walimtumainia mgeni kwamba wanaume hao wote walikuwa wakipekee, na viongozi maarufu wa kidini hawakuwapenda wote wawili.

Walijaribu kumnasa wa kwanza katika maneno yake mwenyewe (Luka 11:54). Walihukumu hisia zake kimakosa (Yohana 8:43; 10:20). Mtu huyo alikuwa ni Bwana Yesu Kristo. Hatimaye, walimgongomelea misumari msalabani na kumwacha afe.

Jamaa wa pili aliishi miaka michache baadaye. Alianza katika mwanzo mbaya alipobadili dini. Na kwa huruma! Alikuwa amesomea huduma chini ya waalimu bora wa wakati huo. Washirika wenzake wa kanisani, walijali zaidi tafrija za kisiasa kuliko ukweli, wakimwita yeye adui yao (Wagalatia 4:16). Walijaribu zaidi ya mara moja kumwua (Mdo 23:12). Walimwinda katika himaya yote ya Kirumi. Baadhi walisema alikuwa kando yake mwenyewe (Yesu) (2 Wakorintho 5:12). Huyo alikuwa ni mtume Paulo.

Wote wawili Yesu na Paulo walikuwa na umaarufu na ahadi za kazi zinazofanana. Hata hivyo, ukweli ulikuwa ni muhimu kwao kuliko umaarufu. Mtu anayeshawishika na hilo leo wakati mwingine huzushiwa uongo pia. Mara nyingi hukashifiwa na kuhukumiwa vibaya. Unaona, ukweli si wakati wote ni maarufu, bali daima ni ukweli. Ukweli unabaki kuwa ukweli hata kama dunia yote itaukataa! Ukweli una umuhimu gani kwako?

**Bobby Key alihubiri kwa miaka mingi katika kanisa la Bwana huki Miami, Oklahoma, Marekani.**

# Uhalali wa Ombi la Marejesho

**Jim Howard**



Uhalali wa ombi la marejesho kwa sasa umekuwa swali katika maeneo mengi ya undugu wetu. Wengi wetu tuliokulia katika harakati, tulisomeshwa katika kanuni za uwezekano kwa kupitia wazazi waliokubali urejeshaji kwa kuegemea katika nguzo rahisi ambayo muundo uliowekwa na Mungu kwa ajili ya kanisa unaoonekana katika Agano Jipya ambao ulipotea, kusahaulika, au kupotoshwa. Bado kuna mengi ya kusemwa kwa ajili ya uelewa huo.

Katika ulimwengu wa leo wenye nia ya kiutendaji nadhani tunahitaji kukumbushwa juu ya thamani ya zoezi la ombi la urejeshaji. Ombi ni la kweli sio tu kwa sababu linafanya kazi, lakini urejeshaji wa uaminifu ikizingatiwa kujithibitisha yenyewe kuwa dawa nzuri kwa matatizo mengi yaliyo makubwa yanayosumbua Ukristo. Hivi ni vielelezo vitatu vya ukweli:

1. **Mkazo wa harakati za urejesho kwa kusanyiko kujitegemea umeweka imara uhuru wetu katika Kristo.** Sio tu makusanyiko moja moja yamelindwa kutoka katika uasi wote, bali kila kusanyiko katika upekee wake lina haiba yake lenyewe na ladha ya theolojia. Kama mwanafunzi hana furaha katika ushirika mmoja, nafasi ni yake anaweza kuipata nyingine pale atakapokuwa nyumbani.
2. **Jaribio la urejesho kuirejesha roho (nia/molali) na mitindo ya ibada ya Kikristo ya awali imethibitika kuchangia kwa ukuaji wa kiroho kwa mtu mmoja mmoja.** Kuimba na kushangiria katika

mioyo yetu (Waefeso 5:19) kunahitaji kujitoa kwa nafsi zetu zaidi kuliko inavyokuwa kusikiliza kiungo cha bomba au kwaya. Utoaji wa utashi (2 Wakorintho 9:7) ni mkuu sana katika kufundisha dhabihu ya ushiriki binafsi wa mtu.

**Uigaji wa urejesho wa picha ya uongozi wa kusanyiko katika Agano Jipya kwa uwingi wa wazee wenye sifa kimaandiko umeleta faida dhidi ya miundo mbalimbali ya uongozi wa kuundwa na watu.**

3. **Uigaji wa urejesho wa picha ya uongozi wa kusanyiko katika Agano Jipya kwa uwingi wa wazee wenye sifa kimaandiko umeamua (chagua) faida dhidi ya miundo mbalimbali ya uongozi wa kuundwa na watu.** Utawala wa mchungaji mmoja unaathirika kwa kutokuwepo na muungano wa hekima wa akili na mioyo mbalimbali. Kuongoza kwa kuweka mbali sinodi (baraza la maamuzi la kanisa), uongozi wa kanisa, au walezi wa mkutano [huleta] chuki kwa upande wa Mkristo mmoja mmoja mwenye akili inayojitegemea. Urejeshaji wa Ukristo wa Agano Jipya bado ni mzuri. Tuwe waaminifu kwa kanuni hiyo.

**Jim Howard ni muelimishaji na mhubiri anayeishi Memphis, Tennessee, Marekani.**

# Umoja na Fundisho

**Ben Jones**

Umoja unatamanika, na bado mara nyingi umekuwa katika kiwango cha ndoto. Kutokuwepo na makubaliano kuhusu njia za kupelekea umoja hatimaye kunaweza kupelekea mwisho wa kushindikana kufanikisha. Kwa bahati mbaya, fundisho lenyewe limekuwa la kawaida, likijikuta kwenye moto wa ongezeko la wapinzani waliogawanyika. Katika ulimwengu wa kisasa, fundisho mara nyingi huchukuliwa kama jambo la pili na ni kizuizi cha umoja wa kidini.

Mtume Paulo alielezea muunganiko wa fundisho na umoja katika waraka kwa Waefeso. Kitabu cha Waefeso kinaweza kugawanywa katika sehemu mbili. Sura ya 1-3 zinaangazia kile ambacho Kristo alifanya kwa ajili ya kanisa, wakati sura ya 4-6 zinaangazia kile ambacho kanisa linapswa kufanya kwa Kristo. Katika muktadha huu Waefeso 4:1-6 ni aina ya kifungu unganishi kikiunganisha shehemu mbili. Katika Kristo, watu wanaitwa katika umoja wa Roho, ushirika mkamilifu uliojulikana katika mpango wa Mungu wa ukombozi wa milele. Wakristo wameagizwa kuenenda kunakostahili wito huu, *"na kujitahidi kuuhifadhi umoja wa Roho katika kifungo cha amani."* (Waefeso 4:3). Kama inavyoashiriwa na kifungu hiki, umoja wa kweli ni zao la Mungu, sio mtu. Kwa namna moja ya ufahamu, umoja unaweza kuelezewa kama mwitikio sahihi kwa neema ya Mungu, ambayo yote yanahitaji na matokeo ya kuenenda katika namna inayostahili Ukristo. Mwenendo wa jinsi hiyo unahusisha mambo mawili, uondoaji wa mtumishi na fundisho la Mwalimu (Bwana).



Kwanza, Paulo aliorodhesha mtiririko wa viwango vya kufanana na Kristo ambavyo lazima vichimbuliwe katika maisha ya kila mwanafunzi ambavyo ni; unyenyekevu, upole, uvumilivu, na juhudi. Mkristo ambaye daima lazima awe na njia yake, mara kwa mara huacha kujali, akishikamana na chuki au kukata tamaa katika dalili za mwanzoni za shida atakuwa msumbufu katika maisha ya kanisa.

Pili, Paulo alifunua mtiririko wa kipekee wa mafundisho ya Agano Jipya ambayo yanaunda msingi wa imani ya Kikristo. Mafundisho haya ni Mungu mmoja na Baba, Bwana mmoja, Roho mmoja, mwili mmoja, imani moja, ubatizo mmoja na tumaini moja. “Moja” saba zote zinatoa mfano na njia kwa ajili ya aina ya umoja unaohitajika kwa watu wa Mungu. Moja katika ufafanuzi, ni utofauti na isiyojumuisha. Inamaanisha moja na ni moja pekee. Wakristo wanaweza kuwa wema na wastahivu kwa wale ambao wanashikilia imani tofauti, lakini umoja unataka vyote viwili hali inayokubalika na wajibu katika kweli.

Chukua mfano, jambo la imani moja. Katika Agano Jipya, tumaini linahusisha matarajio ya ujasiri wa kupata kitu fulani halisia. Tumaini hili la Kikristo ni la uzima wa milele mbinguni, ambao umewekewa msingi katika uhalisia wa ufufuo wa Yesu (1 Petro 1:3) na kutobadilika kwa ahadi za Mungu (Waebrania 6:18-20). Bila ya vithibitisho hivi, hata

hivyo, imani ni zaidi kidogo kuliko ndoto ya mchana. Sasa, fikiri kanisa ambalo mtu mmoja alituaminiwa kufanyika mwili, mwingine alitumainia utawala wa Kristo miaka 1000 na watatu alitumaini kwa watu wote kuokolewa mbali na Injili. Ukweli wa kusikitisha nii kwamba kanisa la namna hiyo lisingekuwa kuliko lile ambalo kila mtu aliamini fundisho moja potofu.

Umoja wa kweli ni zaidi ya jitihada za kupatana, ni kujitoa kwa makusudi kuishi maisha ya ukristo. Njia ya kuelekea umoja inaanza na shauku ya kumjua Mungu na kutii Neno lake. Tunapokubali kwamba Biblia ni sahihi, tutaondoa vikwazo vya umoja.

**Ben Jones anahubiri katika kanisa la Kristo Chuo kikuu huko Morgantown, Virginia Magharibi, Marekani, na ni mwalimu katika Shule ya mahubiri iliyopo Virnia Magharibi.**

**Umoja wa kweli ni zaidi ya juhudi ya kuafikiana; ni lengo la kujitoa kuishi maisha ya Ukristo.**

# Wazo la Haraka Juu ya Aya Muhimu
# 1 Timotheo 2:9-15

**9 Vivyo hivyo wanawake na wajipambe kwa mavazi ya kujisitiri, pamoja na adabu nzuri, na moyo wa kiasi; si kwa kusuka nywele, wala kwa dhahabu na lulu, wala kwa nguo za thamani;**

**10 bali kwa matendo mema, kama iwapasavyo wanawake wanaoukiri uchaji wa Mungu.**

**11 Mwanamke na ajifunze katika utulivu, akitii kwa kila namna.**

**12 Simpi mwanamke ruhusa ya kufundisha, wala kumtawala mwanamume, bali awe katika utulivu.**

**13 Kwa maana Adamu ndiye aliyeumbwa kwanza, na Hawa baadaye.**

**14 Wala Adamu hakudanganywa, ila mwanamke alidanganywa kabisa akaingia katika hali ya kukosa.**

**15 Walakini ataokolewa kwa uzazi wake, kama wakidumu katika imani na upendo na utakaso, pamoja na moyo wa kiasi.**

**Kupitia malezi ya familia, mwanamke anapaswa kuwa na hizi sifa ambazo ni matokeo katika ukomavu wa kiroho na wokovu kama Kristo.**

**Jukumu la wanawake nyumbani na katika kanisa imekuwa ikijadiliwa.**

**Maandiko yanasemaje?**

Mwanaume na mwanamke waliumbwa na Mungu, na kitabu kinachotupa miongozo kiliandikwa na Yeye. Anachosema ni wazi, rahisi kueleweka, na lazima kisikike.

1. **Wanawake wameamriwa kuvaa mavazi ya kujisitiri.** Kwanini? Kwa sababu mavazi yasiyo ya kujisitiri, au kujipamba kunakokusudia kuvutia hisia, yanayotengeneza tamaa katika mioyo ya wanaume. Mwanamke anayevaa magauni mafupi/shati, au magauni yanayoacha wazi sehemu za juu za kifua na mabega, anasababisha wanaume walio karibu yake kutenda dhambi. Ni ukweli ule ule wakati sketi zake zinapokuwa fupi sana , suruali zake zikiwa za kubana sana, au kuondoa vipande "nguo inayoonesha" hiyo ni sawa na kubaki na nguo ya ndani. Mwanamke wa Kikristo hatakiwi kusababisha dhambi.
2. **Katika mikusanyiko ya ibada,** wanawake hawajapewa mamlaka na Mungu kuchukua majukumu ya uongozi wa jumuiya dhidi ya wanaume.

Wengine wanasema hii ilikuwa sheria katika karne ya kwanza pekee, na hata hivyo utamaduni umebadilika. Lakini sheria ya Mungu haiegemei katika utamaduni. Tangu *uumbaji,* Aliwaumba mwanaume na mwanamke kama pande mbili katika kitu kizima, akimwezesha kila mmoja kutimiza jukumu Alilokusudia. Mwanaume ni kichwa cha nyumba, anawajibu wa familia; mwanamke yuko kando yake, kama utimilifu wake (mwanaume). Wanawake wanaamini zaidi, wanarubunika kirahisi. Tazama Andiko. Mitume wangapi, manabii na viongozi katika jumuiya ya Mungu walikuwa wanawake?

# Huna tumaini? Si haraka hivyo

**Steve Higginbotham**

Harrison Okene kutoka Nigeria kwa kutokutarajia alijikuta katika hali ya kupoteza tumaini. Alijikuta yuko katika kina cha bahari, katika boya ndani ya boti yake ya kuvutwa iliyopinduliwa na wimbi baya. Harrison alikuwa katika giza kuu, alichanganyikiwa, alikuwa peke yake, na alikuwa amevaa kaptula tu katika hali ya hewa ya baridi kali. Kwa masaa 60, aligugumia katika giza kuu, akitetemeka kwa baridi, huku akisikiliza samaki wakila maiti za wafanyakazi wenzake, na kusubiria pumzi yake kukatika.

Halafu, wakati pumzi yake ilipokaribia kuondoka, jambo la kushangaza likatokea. Mwokozi mzamiaji akatokea. Harrison akapewa hewa (mtungi wenye hewa ya oxygen), akapelekwa katika chumba cha kupunguza mgandamizo wa hewa, na hatimaye akainuliwa hadi katika uso wa ardhi, alinyakuliwa kutoka mdomo wa kifo. Kilichoonekana kama hali ya kukosa tumaini pekee ilithibitsha kuwa ni mpango kwa ajili ya wokovu wake. Sasa Harrison anaishi akiwaambie wengine jinsi alivyookolewa.

Umewahi kujihisi kukosa tumaini kiroho? Umewahi kujisikia kwamba ulikuwa mbali na neema ya wokovu wa Mungu? Halafu, wacha nikukumbushe hili. Kama ni mlevi, baba anayejamiiana na watu wake wa karibu (Lutu), kahaba muongo (Rahabu), mzinzi mwuuaji (Daudi), na mtesaji wa kanisa (Sauli/Paulo) unaweza kusamehewa na kuinuliwa kama kielelezo cha wanaume mashuhuli na wanawake wa imani, halafu kuna tumaini kwa ajili yako pia!


Jaribu kufikiri juu ya furaha na ahueni aliyoipitia Harrison Okene wakati alipofika nje na kuwashika mikono waokozi wake! Tumaini kutoka pasipo tumaini! Vilevile, fikiria furaha na ahueni ambayo anaipitia mwenye dhambi aliyetoka nje na kushika mkono wa Mwokozi! Tumaini kutoka pasipo tumaini!

Kwa wengine miungoni mwenu ambao mmeokolewa na Mungu na sasa mna uzima, waambieni wengine kuhusu hilo! Waambieni jinsi Mungu alivyowaokoa kutoka katika hali ya kukosa tumaini na kuwapa tumaini! ***"Na waseme hivi waliokombolewa na Bwana,"*** (Zaburi 107:2).

**Steve Higginbotham anahubiri katika kanisa la Kristo Karns huko Knoxville, Tennessee, Marekani.**

# ALIENDELEA KUHUBIRI INJILI

**Wayne Brewer**



Mmoja kati ya watu wa kuvutia katika Agano Jipya alikuwa Filipo, mtu aliyeshuhudiwa wema miungoni mwa washirika wa kanisa, na ambaye alichaguliwa "kuhudumu mezani" katika Yerusalemu (Mdo 6:2,5). Filipo alithibitika kuwa ni mtumishi mzuri wa Bwana na kanisa kwa vile alivyohakikisha kwamba wajane hawaachwi kuhusiana na mahitaji yao (Mdo 6:1). Hii ilikuwa ni kazi muhimu kwa angalau sababu mbili: kwanza, ili kwamba mitume waweze kuendelea na kazi yao ya kuhubiri Injili (Mdo 6:2), na pili, kwa sababu ***"Dini iliyo safi, isiyo na taka mbele za Mungu Baba ni hii, Kwenda kuwatazama yatima na wajane katika dhiki yao,.."*** (Yakobo 1:27).

Wakati fulani baadaye, "***Siku ile kukatukia adha kuu ya kanisa lililokuwa katika Yerusalemu; wote wakatawanyika…"*** (Mdo 8:1), na mmoja kati yao aliyeuacha mji alikuwa Filipo. Luka anatufahamisha, "***Filipo akatelemka akaingia mji wa Samaria, akawahubiri Kristo***." (Mdo 8:5). Filipo anavutia kwa sababu alienda kwa watu ambao walichukiwa sana na kudharauliwa na Wayahudi, Wasamaria. Matokeo yake, ingawa walikuwa wakimfariji sana, kwa sababu "***Lakini walipomwamini Filipo, akizihubiri habari njema za ufalme wa***

***Mungu, na jina lake Yesu Kristo, wakabatizwa, wanaume na wanawake."*** (Mdo 8:12). Filipo alienda katika sehemu ya mwisho ambayo Wayahudi wangeenda, na nguvu ya Injili ikaonekana (Warumi 1:16; 10:17).

Filipo na wale wengine waliotawanyika walihubiri nini? Walilihubiri "neno", "Kristo", "Ufalme wa Mungu", na "jina la Yesu Kristo", ambayo inaashiria safu pana ya mada. Wakati fulani baadaye, Filipo alikutana na mtu kutoka Ethiopia, ***"…akianza kwa andiko lilo hilo, akamhubiri habari njema za Yesu."*** (Mdo 8:35). Inapaswa itazamwe kwamba Wakristo wa karne ya kwanza, kama Filipo, walihubiri Neno la Mungu bila ya kuhubiri tamaduni zao za kibinadamu. Mateso makali ya Yerusalemu na maeneo mengine yaliweza kumuondoa Filipo na wengine wengi kutoka katika mji, lakini hayakuweza kuwazuia kuhubiri na kufundisha Injili. Kwa kweli, mateso yalitoa fursa mpya kwa wao kuhubiri Neno.

Filipo alihubiri Injili kwa Muethiopia, mtu yule aliitii Injili (Mdo 8:38), na halafu maneno haya yameandikwa kumhusu Filipo, ***"…akahubiri Injili katika miji yote,..*** " (Mdo 8:40). Muda wa kitenzi hiki ni uliopita *"alihubri"* kihalisia ingeweza kutafsiriwa *"aliendelea kuhubiri"* licha ya vizuizi vingi ambavyo Filipo alikabiliana navyo, aliendelea kuhubiri Injili ya Kristo na habari njema za Ufalme wa Mungu. Maneno yale *"aliendelea kuhubiri"* yanapaswa kuwa tabia ya kila mwalimu na mhubiri wa Neno la Mungu leo. Ni lazima tuendelee kufundisha na kuhubiri pale watu wanapoamini na kutoamini. Ni lazima tuendelee kufundisha na kuhubiri pale watu wanapoitikia au kutoitikia. Lazima tuendelee kufundisha na kuhubiri ikiwa ujumbe ni maarufu au sio maarufu. Lazima tufanye kama Filipo na kuendelea kuhubiri, kwa sababu Injili ***"…ni uweza wa Mungu uletao wokovu…"*** (Warumi 1:16).

**Wayne Brewer anafanya kazi na kanisa la Bwana huko Mabelvale, Arkansas, Marekani**

**Mateso makali katika Yerusalemu na sehemu nyingine yaliweza kumuondoa Filipo na wengine wengi kutoka katika mji, lakini hayakuwafanya kuacha kuhubiri na kufundisha Injili.**

# Miaka 24 katika Ngazi ya Kwanza!

**Jess Whitlock**

Miaka kadhaa iliyopita habari ilinifikia mezani kwangu. Ilikuwa na kipande hiki, "Miaka ishirini na nne katika ngazi ya kwanza. Huo ndio muda ambao ingechukua kupita kama tu shule za umma zingekutana mara nyingi kama Shule ya Jumapili, na *kama hakuna darasa la Biblia ambalo lingekosekana!"*

Neno la Mungu kulingana na utafiti wa 2012 (Rankin), ulifunua kuwa 19% pekee ya "waenda kanisani" wanasoma Biblia kila siku. Wengi 25% walisema wanasoma Biblia mara chache kwa wiki. Wanaoyumbayumba ni 14% waliashiria kusoma Biblia mara moja kwa wiki. Halafu 22% walikili kusoma Neno la Mungu "mara moja kwa mwezi au mara chache katika mwezi." Miezi kadhaa iliyopita, ndugu Jack Wall, ndugu Dale Vann, na mimi tulikuwa na mjadala mrefu kuhusu mtaala wa darasa letu la Biblia. Mengi ya "fasihi yetu" yanatakiwa kuhakikiwa ili kuhakikisha upo kimaandiko, na maelekezo mengi yanatakiwa "kuondolewa," na halafu mambo ya kubuniwa ni mabaya sana. Tuliamua kuandika nyenzo yetu wenyewe. Kwa kuuliza na wengine, niliwasiliana na Gary Summers, ambaye alinijibu kwa kusema, "Tumefanya hivyo!"

Wazee (maaskofu) waliikagua hiyo nyenzo, wakaipanga, na sasa tunatekeleza nyenzo ya Biblia ambayo inaweza kuifanya Biblia nzima kufundishwa kwa miaka 5½! Hii inamaanisha vijana wetu wadogo wanaweza kujifunza Agano la Kale na Agano Jipya mara mbili kabla ya maafari ya Shule ya Juu (High School).

Hayati ndugu Eldred Stevens aliwahi kuchunguza kwamba ikiwa mtu atatumia dakika 20 kwa siku kufanya jambo lolote alilopewa kwa kipindi cha miaka 20, kwa muda huo, huyo atachukuliwa kuwa ni

“mamlaka” katika eneo hilo. Biblia hutupatia ukamilifu wote katika kila tendo jema (2 Timotheo 3:16-17), Biblia ni Kweli ambayo inaweza kutuweka huru (Yohana 8:32: 17:17), Neno la Bwana ni hakika na haki (Zaburi 119:140. Mithali 30:5,6). Na kamwe tusisahau thamani ya Neno la Mungu na ya kwamba Neno lake litakuwa ni kipimo cha mwisho cha hukumu kwa wanadamu wote (Yohana 12:48).

Hata hivyo, Mahakama Kuu sio mamlaka ya mwisho! Bodi hiyo tukufu siku moja itasimama mbele ya ***Mahakama Kuu*** halisi! **Kila mzazi na babu wanapaswa kufikiri kwa umakini kuhusu maelezo ya ufunguzi!** Watoto (wajukuu) wako wanahudhuriaje madarasa ya Biblia? Ikiwa wanafanya hivyo nusu ya madarasa yale, hiyo inamaanisha itahitajika **miaka 48 kumaliza ngazi ya kwanza!** Vipi kama Shule za umma wangekutana tu kama inavyofanyika mara nyingi katika madarasa yetu ya Biblia? Unatambua ya kwamba wengi wa vijana katika taifa hili (Marekani) wasingeishi kwa muda wa kutosha kuingia Shule ya Awali ya Juu (Junior High School)? **Hebu tutilie maanani kuhusu kujifunza Biblia!**

# Je, Unapimaje?

Msiliongeze neno niwaamurulo wala msilipunguze, mpate kuzishika amri za Bwana, Mungu wenu, niwaamuruzo. Macho yenu yameona aliyoyatenda Bwana kwa sababu ya Baal-peori; maana wote




waliomfuata Baal-peori, Bwana, Mungu wako, amewaangamiza kutoka kati yako. Bali ninyi mlioambatana na Bwana, Mungu wenu, mnaishi kila mmoja wenu, hata leo. Angalieni nimewafundisha amri na hukumu, vile vile kama Bwana, Mungu wangu, alivyoniamuru, ili mzitende katika nchi mwingiayo ili kuimiliki. Zishikeni basi, mkazitende, maana hii ndiyo hekima yenu na akili zenu, machoni pa mataifa watakaozisikia amri hizi zote, nao watasema, Hakika taifa hili kubwa ni watu wenye hekima na akili. Kwa maana liko taifa gani kubwa, lililo na Mungu aliye karibu nao, kama Bwana, Mungu wetu, alivyo, kila tumwitapo? Tena liko taifa gani kubwa, lililo na amri na hukumu zenye haki kama torati hii yote, ninayoiweka mbele yenu leo. Lakini, jihadhari nafsi yako, ukailinde roho yako kwa bidii, usije ukayasahau mambo yale uliyoyaona kwa macho yako, yakaondoka moyoni mwako siku zote za maisha yako; bali uwajulishe watoto wako na watoto wa watoto wako;



# Nini unachoweza kufanya siku ya Jumamosi ili kuifanya siku ya Jumapili kuwa ya Ibada zaidi?

**J. Randal Matheny**

Kichwa cha habari kwa ajili ya makala katika mafanikio maarufu na teknolojia ya tovuti inatoa, "Kile unachoweza kufanya siku ya Jumapili ili kuifanya siku ya Jumatatu iwe rahisi zaidi." Si jambo la kushangaza kwamba watu kushikilia maendeleo ya kitaaluma na mafanikio ya kifedha mara zote hufikiria jinsi ya kuwa mbele.

Sasa kwa nini Wakristo hawafikirii zaidi kuhusu mafanikio ya kiroho, ya kwao na jirani zao? Nini tunaweza kufanya siku ya Jumamosi ili kuifanya siku ya Jumapili kuwa ya ibada zaidi, kiroho, na ya kujenga? Haya ni maoni saba ya mambo ya kuzingatia kuyafanya siku ya Jumamosi ili kuwa tayari kwa siku ya Jumapili.

1. Nenda kalale mapema usiku wa Jumamosi. Pata mapumziko ya kutosha. kusinzia hakufai kiroho. Usijipe mzigo mkubwa sana siku moja kabla ya siku ya Bwana kiasi kwamba ukashindwa kuabudu vizuri.

2. Jitayarishe kwa ajili ya mafanikio. Uliza ni ukweli gani utakaousikia ambao utaleta mabadiriko katika maisha yako katika Kristo na kumtumikia Mungu.

3. Mtafute ambaye ni mhitaji kiroho. Mwombe Bwana akuoneshe mtu unayeweza kuwa rafiki naye.

4. Mwalike mtu aende pamoja nawe kanisani. Fafanua kabla ya muda kile kinachotarajiwa. Mwambie ni faida gani zinazoongezeka kwa mahudhurio.

5. Soma Biblia yako na kuomba siku ya Jumamosi, na siku moja kabla, na siku moja kabla ya hapo. Watu wanaomtafuta Mungu ndani ya wiki wanaweza kumtukuza Mungu vizuri zaidi siku ya Jumapili.

6. Iache nafsi yako kabla ya kuingia katika jengo, ukumbi, au chumba ambapo kanisa linakutana. Vaa husika ya Mungu, matendo yake, mapenzi yake, kusudi lake, wema wake kwa usawa katika kiini cha mtazamo wako.

7. Jenga na ujengwe. Toa na ujifunze kupokea. Jioneshe kuwa ni rafiki, na upate marafiki. Msogelee Bwana, na Yeye atakusogelea. Jifunze na utende kanuni ya usawa.

Wafanyabiashara wenye akili wanajua kwamba mafanikio hayatokei kwa bahati. Kufanya kazi nzuri kunahitaji maandalizi. Kufanya ibada mara chache na kumwabudu Mwenyezi kunatokea hivyo hivyo. Kwa hiyo, Jumamosi inaweza kuwa wakati mzuri wa kujiweka tayari kwa ajili ya Siku ya Bwana.

**J. Randal Mathen ni Mkristo mchapishaji na mhariri huko Brazil.**

# Ibada ya Agano Jipya

**Pasipo mpangilio maalum, ibada ya Agano Jipya ina matendo matano yaliyotofauti, ambayo kimsingi yanatuongoza kwa Baba yetu wa Mbinguni. Umakini wa uzingatiaji wa Agano Jipya unafunua matendo yafuatayo ya ibada.**

- **Kufundisha au Kuhubiri (Mdo 20:7)**
- **Meza ya Bwana (1 Wakorintho 11:23-26)**
- **Changizo (1 Wakorintho 16:1-2)**
- **Uimbaji (Waefeso 5:19; Wakolosai 3:16,17)**
- **Sala (1 Wakorintho 14:15)**

**Nyongeza au pungufu kuliko hii katika Siku ya Bwana haijaamriwa na Mungu katika Injili ya Kristo.**

# Ombeni Bila Kukoma

**Dalton Key**

Tunajivika wenyewe uchovu kwa hofu, tunafululiza matumbo yetu kwa msongo usababishao vidonda, na tunajipeleka wenyewe mapema katika kaburi lisiloridhika kwa sababu tumepoteza kuona kusudi na nguvu ya maombi. ***"huku mkimtwika yeye fadhaa zenu zote, kwa maana yeye hujishughulisha sana kwa mambo yenu."*** maelezo hayo bado yana ukweli (1 Petro 5:7). Inathibitisha kuwa Mungu yuko, ya kwamba Yeye ni mwenye nguvu, na ya kwamba anatujali, lazima turudi katika usitawi wa maombi, tukichukua kielelezo kizuri cha wanamaombi katika Biblia. Lazima tujifunze kuyashika maonyo ya Paulo ***"Ombeni bila kukoma"*** (1 Wathesalonike 5:17).

Tazama historia ya nyakati! Watu mashuhuri wa Mungu daima wamekuwa watu wazuri wa maombi. Isaka aliomba akiwa kondeni (Mwanzo 24:63), Yakobo, kando ya kijito (Mwanzo 32:22-24), Yeremia kutoka gerezani [gereza la chini ya ardhi] (Maombolezo 3:55), Danieli kutoka katika tundu la Simba (Danieli 6), Yona kutoka katika tumbo la samaki (Yona 2:1), Petro akiwa juu darini (Mdo 10:9), na maandiko yanaonesha kwamba mtume Paulo, mtu mkuu wa maombi, alimwomba Mungu kutoka maabusu katika matukio zaidi ya moja.

Na vipi kwa Mwokozi wetu? Wakati akiwa katika mwili, hakuwa mtu wa maombi? Je, hakutumia muda mwingi, ndiyo, nyakati zote za usiku kutokulala, kwa juhudi kujishughulisha na dua? Wanafunzi wake walistaajabishwa sana na maisha ya maombi ya Bwana wetu. Katika tukio moja, pindi alipomaliza kuomba, mmoja wa wafuasi wake alimwomba, ***"…Bwana, tufundishe sisi kusali,.."*** (Luka 11:1). Sala yake imeandikwa katika Yohana 17, sala ambayo inapaswa kuitwa "Sala ya Bwana," inafunua kina na utajiri wa maisha yake ya sala.

Haya yote, ***"ambaye ulimwengu haukumstahili,"*** sambamba na wengine wasiohesabika ambao hawakutajwa hapa, walitambua, na

kugundua umuhimu wa kanuni ya kibiblia ambayo wengi wetu kwa ujinga na kukosa imani tumeiweka kando. Hawa wote waliamini, waliamini kwa uthabiti, hivyo ***"…Kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana, akiomba kwa bidii."*** (Yakobo 5:16).

**Dalton Key ni mhariri wa Njia za Kale na anahubiri katika kusanyiko la Rockford huko Tulsa, Oklahoma, Marekani.**

# Kuonesha Shukrani katika Meza ya Bwana

**Maxie B. Boren**

Kupitia undungu, kwa dhati naamini kuna uhitaji mkubwa wa upana wa mawazo na kuonesha maana ya shukurani kama mikusanyiko ya ibada inayoongozwa katika maombi kabla ya kushiriki nembo zinazowakilisha mwili na damu ya Yesu. Ni upungufu wa kiroho kama maombi siyo ya kimaandiko na ya kumaanisha, na kama hayaleti ufahamu wa kina kama vile umuhimu wa dhabihu kuu aliyoitoa Yesu kwa ajili yetu. Kumwelezea ndugu alposali, "Ahsante Mungu, kwa ajili ya huu mkate ubariki kwa ajili ya ustawi wa miili yetu." Ni wazi, labda alikuwa na wasiwasi na hata hakugundua alichokuwa akisema, au vinginevyo hakujua kitu chochote kuhusu nini Chakula cha Bwana kinahusu. Kwa namna yoyote, ilizuia jambo zuri kutoka katika hali ya kiroho ya wakati husika.

Maombi yanayotolewa ambayo kamwe hayamshukuru Mungu kwa ajili ya kitu ambacho tunapaswa kuwa wenye shukurani tunaposhiriki Chakula cha Bwana. Baadhi ya ndugu katika maombi yao kipindi cha Meza ya Bwana wanamshukuru Mungu karibu kwa kila kitu kinachofikirika wakati kamwe hata hawafanyi marejeo ya dhabihu ya Kristo. Hii inasikitisha sana na kuweka wazi tatizo halisi katika maeneo mengi sana. **Tunawezaje kusonga mbele katika sehemu hii muhimu ya ibada?**



Kwanza kabisa, ndugu wanapaswa kusoma vitabu elekezi vyote vinavyohusiana na kumbukumbu ya Kristo ambayo inatakiwa kufanywa katika siku ya kwanza ya juma (Mdo 20:7), na tumia muda fulani wa ukimya katika kutafakuri kwa kusali juu ya hayo (Mathayo 26:26-29; Marko 14:22-25; Luka 22:14-20; 1 Wakorintho 11:23-29). Pili, vifungu vingine vinavyohusiana ambavyo vinapaswa kuzingatiwa kwa umakini sawa, kama vile  Warumi 5:6-11; 1 Wakorintho 1:18-24, 15:1-4; 2 Wakorintho 5:18-21; Wagalatia 1:3-4, 2:20; 6:14; Waefeso 1:3-14; 2:4-9; Wafilipi 3:7-12; Wakolosai 1:12-23; 1 Wathesalonike 1:10; 2 Timotheo 1:8b-10; Tito 2:11-14; 3:4-7; Waebrania 2:9-18; 7:26-27; 9:11-28, 10:10,12; 1 Petro 1:18,19; 2:21-25; 1 Yohana 4:9,10 na Ufunuo 7:9,14.

Ingekuwa vizuri kusoma na kutafakuri kuhusu ujumbe wa nyimbo hizo kama *"Ninapo Chunguza Maajabu ya Msalaba", "Oh Vina na Utajiri",* na *"Kugongomelewa Msalabani".* Kwa kusoma na kutafakuri Maandiko yaliyotajwa hapo juu na nyimbo, ndugu aliye na wajibu wa kuongoza sala katika Meza ya Bwana anapaswa kuwa na umakini wa mawazo katika kile kinachotakiwa kuwa na maneno sahihi katika kusali. Sala inapaswa kufanywa kwa dhati na juhudi kutoka  katika utulivu wa kina wa moyo, kuonesha shukurani kubwa kwa ajili ya upendo wa Mungu na rehema kama ilivyofunuliwa katika Yesu Kristo na utayari wake wa kujitoa msalabani  badala yetu.

Tafadhali zingatia uchunguzi wa mambo matatu ya mwisho:

(1) Mara nyingi, sala ni maneno ya kumshukuru Mungu kwa ajili ya "mkate" na "mzao wa mzabibu" bila hata ya kutaja mwili na damu ya Yesu. Ndugu, huu si mkate wa kawaida, wala si juisi ya kawaida ya zabibu,  ambayo kwayo kimsingi tunashukuru, bali ni mwili na damu ya Yesu! Pekee katika mtazamo wa upili je, tunashukuru kwa nembo zenyewe. Ni kile nembo zinachowakilisha kwa hicho tunapaswa kushukuru!  Kwanini si neno maombi yetu pamoja na msisitizo inapotakiwa?

(2) Kila sala ya jumuiya inapaswa kutamkwa kwa sauti ya juu inayotosha na ya dhahiri ili watu wasikie na kuelewa. Ndugu kamwe hapaswi "kunong'ona" wakati wa sala ya jumuiya.

(3) Mwishowe, tafadhali ndugu, kumbuka, ni Mungu Baba tumwombaye, na kama ingekuwa Yesu Mwana wake mpendwa aliyekufa masalabani. Ni udanganyifu kumshukuru Baba kwa mwili wake (Yesu) uliotolewa na damu yake iliyomwagika. Mungu ni roho (Yohana 4:23,24) na roho haina mwili na mifupa (Luka 24:39). Alikuwa ni Yesu, Mwana pekee wa Mungu, ambaye alifanyika mwili (Yohana 1:1-4,14; 3:16-17) na kustahimili mateso ya msalaba kwa ajili yetu (Wafilipi 2:5-11). Ilikuwa, kwa hiyo, mwili na damu ya Yesu ambao ulisulibiwa Kalvari. Ingawa Uungu ni "moja (umoja)", Biblia inaweka bayana utofauti baina ya Baba wa mbinguni na Mwana ambaye alikuja duniani kama Mwokozi, na tunahitajika kuwa makini sana kupata ukweli huo. Kufanya vinginevyo ni kukosea, na kufundisha wengine vibaya hata tunaposali.

**Maxie B. Boren (1932-2016) alikuwa mhubiri wa Injili na mzee (Askofu) wa kusanyiko la Brown Trait huko Bedford, Texas, Marekani.**

# Je, Umesali?

Chad Ezelle



Bwana wetu ameliweka hili wazi sana kwa watu ambao kwanza walimfuata Yeye, walipaswa kumwomba Mungu akutane na haja zao. Sisi hatupaswi? Kihalisia, sala inayotoka moyoni inaweza kuzaa mabadiriko yenye nguvu katika maisha yetu na ulimwengu. Tunapoinua mioyo yetu kwa Mungu, kuomba hekima yake, tunajifunua kwa chanzo kikuu cha hekima na upendo.

Je, una maswali kuhusu leo? Maswali kuhusu baadaye yako ambayo huwezi kujibu? Maswali kuhusu chaguzi au maamuzi ambayo utatakiwa kuyafanya hivi karibuni? Mahitaji ambayo huwezi kuyakidhi wewe mwenyewe? Umetafuta hekima ya Mungu? Umeomba kwa ajili ya mwongozo? Ulinzi? Nguvu? Ujasiri? Kama umefanya, je, unaendelea kuomba hekima yake? Mungu wetu ana uwezo mkamilifu wa kujibu sala zako, lakini kwanza, unatakiwa kuomba. Tufuta muda leo kusoma Yakobo 1:5. Tafakari kuhusu hilo. Liweke katika matendo.

# Maneno ndio kila kitu?

**Andy Robison**

Kwa kuhusiana na uimbaji wa kusanyiko, mara nyingi huweka mzaha, “Sawa, maneno ndiyo yanayojalisha, hata hivyo.” Hii ni faraja kwa waabuduo viziwi wa toni, lakini, kidunia, mithali inayokusudiwa inaweza kufika mbali sana.

Kama maneno yangekuwa, kwa kweli, ndiyo kila kitu, uenda Mungu angesema kitu fulani kama, “Someaneni katika mashairi, zaburi na tenzi za rohoni.” Je, hiyo ingekuwa mpangilio wa muziki (uakapela) wenye umuhimu zaidi kuliko unaotambulika mara nyingi?

Muziki ni kitu cha hisia. Watengenezaji muziki wa ala (kutoka simfoni [aina ya muziki upigwao kwa kutumia ala nyingi kwa pamoja.] na maigizo yakuimbwa kwa muziki aina ya punk rock na muziki aina ya country) wanafanya kazi ya kutengeneza noti (nota) za muendelezo, toni (sauti) na miunganiko kuunda hisia, mara nyingi huonesha baadhi ya tukio au tukio la kihistoria. Mshindo wa matarumbeta kwa ajili ya Michezo ya Olimpiki ni wito wa mashindano na uwezekano wa kushinda, ni kumbukizi ya sauti mfululizo iliyopangiliwa kwa sauti za haraka za tarumbeta zenye muunganiko. Maombolezo ya huzuni, kwa kutofautisha, inaweza kuchukua nyuzi za chini kwa taratibu, kwa miondoko makini.

Kibari cha uimbaji akapela kwa makusanyiko, muziki kwa ujumla unaoshikamana na maneno. “Karibu Nawe Mungu Wangu” kamwe yasingepangwa kufanya mfuatano wa uzani (kama katika “Mzunguko wa Ujumbe”). Msisimko wa “Wimbo Mpya” ni bora pamoja na mkito wake na kiitikio kikuu; isingefanya vizuri kwa mtindo wa kuimba wa kurudia maneno na tafakari, “Ninapotafakari Maajabu ya Msalaba” kwa hisia. Watengenezaji wa muziki wanatafuta kukuza matokeo chanya ya kutamka (kuimba).

Uimbaji unaweza kutazamwa kama mlango wenye kibari cha uungu kwa ajili ya mwanadamu kutoa (kuelezea) hisia. Makundi mengi ya madhehebu ya kidini hutumia hisia kinyume na viwango vya kimaandiko, kutikisika kusiko sahihi na kuzunguka, kupunga mkono (mikono) na kuomboleza kwa kujawa na Roho. Mungu ni wa utaratibu (1 Wakorintho 14:40) kwa kweli ametupa uwanja kwa sisi kuonesha ni jinsi gani tunajisikia kwake (hata na wengine) katika nyakati maalumu. Hii ndiyo sababu baadhi ya hisia za ndani sana za huzuni, masikitiko, uchungu, furaha, ushindi na sifa zinakwenda kwa vizazi vyote zinapatikana katika kitabu cha….umekiotea…Zaburi. kihalisia ziliimbwa. Zaidi, uenda hii ni sababu moja (kwa namna fulani angalau ni matokeo) ambayo kuimba kulichaguliwa kama kibari cha matumizi ya muziki katika ibada. Ala za muziki zinaweza kumfanya mtu ajihisi kwa namna fulani bila sababu ya kielimu kama kwanini (sababu ya kufanya hivyo). Kwa kuimba, elimu inaingizwa kwanza na zaidi. Mtu anajua kwamba anatafiti kipande cha tukio la maajabu ya msalaba. Halafu, muziki unasaidia kukuza wazo.



Hatuna budi ndugu, kufanyia kazi uimbaji kwa kadiri ya uwezo wao wote. Mungu anambariki aabuduye kwa kidatu kimoja (toni moja) ambaye anadakia kwa kidokezi cha mwimbishaji. Hata hivyo, wale ambao wanajipa kisingizio kwa mzaha wa kutowahi kujaribu kuelewa sauti (ya wimbo), toni, kutamka, muunganiko na mambo yote ambayo yanafanya uimbaji uwe na maana zaidi wanakosa fursa nzuri katika huduma ya Mungu. Ili ***"tuzingatiane"*** (Waebrania 10:24-25) katika

mpangilio wa ibada, hatupaswi sisi sote tuwe na dhumuni la kusonga mbele katika kila tendo la ibada kutokana na uzingatiaji katika kujifunza kujielezea katika wimbo?

Maneno yanajarisha. Bila maneno, hakungekuwa na fundisho lolote au kuonya. Hata hivyo, kumbuka kwamba bila muziki (akapela/kuimba bila vyombo), hakungekuwa na uimbaji wowote au wimbo.

**Andy Robison ni Mkurugenzi wa Shule ya Mahubiri Virginia Magharibi (www.wvsop.com). Ni mpokeaji wa B.A kutoka Harding (ambapo alipokea ufadhili wa L.O. Sanderson kwa uandishi wa mashairi), pamoja na yote mawili makuu katika Biblia na Sauti ya Muziki. Ameandika nyimbo nyingi na kusaidia kuzalisha CDs za akapela akiimba kufaidisha kambi ya Vijana Wakristo Virginia Magharibi, ambapo anatumika katika Bodi ya Wakurugenzi. Ni Mhariri wa vitabu vya nyimbo** Kufundisha na kuonya na nyimbo 100 kwa Utukufu wa Mungu. **Nyimbo nyingi halisi zinaweza kufikiwa kwa www.churchofchrist-songs.com. Yeye na mke wake Marsha wana watoto wawili, Hannah na Andrew.**



Mkazi wa zamani wa Vermont (mji uliopo Uingereza) aliketi kwa muda mrefu na kimya katika ukumbi wake jioni moja ya majira ya kuchipua na mkewe mwenye umri wa miaka 50. Ghafla aliropoka, "Wakati mwingine ninapofikiri kile ulichomaanisha kwangu hii miaka yote, ndicho niwezacho kufanya kujizuia kutokwambia,"

Askari Polisi mpya (mwanafunzi) aliulizwa wakati wa mtihani, "Nini ungefanya kama ungetakiwa kumkamata mama yako mwenyewe?"

Akajibu, "Ningeomba masaada!"

Mwanamke mmoja jirani alizungumza kuhusu uzoefu aliokuwa nao ameupata punde. Alisema, "Najihisi kama mwili wangu umekosa kabisa umbo zuri, kwa hiyo nilipata ruhusa ya daktari wangu kujiunga na klabu ya mazoezi na kuanza mazoezi.

Niliamua kuchukua darasa la mazoezi ya viungo ya kuongeza hewa kwa watu wazima. Niliinama, niligeuka, nilizunguka, niliruka-ruka juu na chini, na nilitokwa na jasho kwa muda wa saa moja. Lakini,nilipovaa vazi langu (vazi la kubana la mazoezi au wanalovaa wana sarakasi katika onesho), darasa liliisha…"

Wanawake wanne walijikuta katika mabishano mabaya. Baada ya kufoka sana, kupiga kelele, na kuvutana nywere, mmoja wao akasema, "Naenda kituo cha Polisi kuwashitaki." Wale watatu wengine walitaka wao wafike kwanza. Matokeo yakawa kwamba wote wanne wakakimbilia kituo cha Polisi, kila mmoja akijaribu kuwa wa kwanza kutoa malalamiko yake. Mashitaka na juu ya mashitaka yakajaa hewani.

Mwishowe askari akataka utaratibu. Wakati utulivu uliporejeshwa, alionesha hekima ya Sulemani pale

alipotangaza, “Sawa, wakina mama, nitamsikiliza mmoja mmoja kwa zamu. Mkubwa (wa umri) anaweza kuzungumza kwanza.”

Kesi ikafungwa!

Mke mlizi (anayelialia). “Yohana, umesahau tena siku yangu ya kuzaliwa.” Mume akafikiri kwa haraka: “Lakini mpenzi, unatarajia vipi mimi nikumbuke wakati kamwe hutazami siku ya ukubwa?”

Aah! Nilipitia hali ya kukaribia kifo ambayo imebadilisha maisha yangu milele. Siku moja nilienda kuendesha farasi. Kila kitu kilikuwa kinaenda vizuri mpaka pale farasi alipoanza kugoma na kurukaruka. Nilijitahidi kwa uwezo wangu wote kumshikilia, lakini nikatupwa chini.

Wakati ambapo mambo yasingeweza kuwa mabaya zaidi, mguu wangu ukanasa kwenye kamba ya kupandia. Hili lilipotokea, nikadondokea kichwa ardhini. Kichwa changu kikaendelea kujipigiza kwa nguvu na kwa nguvu, na farasi hakuacha wala hata kutulia.

Wakati napoteza matumaini na kupoteza fahamu meneja wa Wal-Mart (duka) alikuja na kuuchomoa.

Rafiki yangu mwenye hekima Leon alitoa ushauri wenye ushahidi wa kipuuzi kunisaidia kuamka kitandani kila asubuhi. Weka mtego wa panya juu ya kengele ya saa. Inasaidia kukuzuia kubiringita na kurudi tena kulala baada ya kupata kifungo cha usingizi.

Tulibahatika pindi tuliposikia Piedmont Hoteli ya zamani iliyoko Atlanta ilikuwa ikirekebishwa na milango yake mizuri ya mbao ilikuwa inapatikana kwa kuuzwa kama bidhaa zilizonusurika kuharibika. Tulinunua kadhaa na tukaiweka katika nyumba yetu ya karne ya 19.

Nikawa namtembeza rafiki yangu kwenye nyumba ili kumwonesha, “ Unajua, hii milango inatoka Piedmont Hoteli.” Rafiki yangu alinyanyua kope na kusema, “Watu wengi wanachukua tu mataulo.”

Mwanasheria alipiga simu nyumbani kwa mkuu wa mkoa muda mfupi baada ya usiku wa

manane. “Nahitaji kuongea na mkuu wa mkoa, ni dharura!” alisema mwnasheria.

Baada ya kumbembeleza, msaidizi wa mkuu wa mkoa alikubali kumwamsha. “Kwa hiyo, ni kitu gani hicho muhimu ambacho hakiwezi kusubiri hadi asubuhi?” alilalamika mkuu wa mkoa.

“Hakimu Cooper amefariki, na ninataka kuchukua nafasi yake,” alisihi mwanasheria. “Oh, ni sawa kwangu kama ni sawa pamoja na msiba wa nyumbani,” alijibu mkuu wa mkoa.

Kama unakabwa na barafu, kunywa kikombe cha maji yanayochemka yatelemke kwenye koo lako. Kizuizi mara moja kitajiondoa.

# Bado Sauti ni Ndogo

**Rani Timoti**



Wanakushambulia katika moyo. Akili yako inazunguka, kugeuka, na kujua inatakiwa kubadilika. Unapewa changamoto, unachochewa, na kupitia maumivu makali ya uchochezi wa fikra. Mazingira yako yamesheheni majaribu, njia panda za maadili, na chaguzi zenye maumivu. Ungeweza kuepuka, kukwepa, kusitisha, au kuacha, lakini bado wangeendelea kuwepo wakijibanza na kuhitaji kushughulika nawe.

Maswali ya dhamiri kutoka katika Biblia yanahitajika. Yanakukumbusha kuwa Mungu ni nani na wewe ni nani! Uhusiano wako na Mungu ukoje? Haya ni Maandiko machache ya kuyatafakari.


**Mwanzo 4:7**- Mungu alizungumza na Kaini kuhusiana na uchaguzi wa kuwa na wivu, uchungu, na mauaji. "***Kama ukitenda vyema, hutapata kibali? Usipotenda vyema dhambi iko, inakuotea mlangoni, nayo inakutamani wewe, walakini yapasa uishinde."***

**Mwanzo 39:9**, "***Hakuna mkuu katika nyumba hii kuliko mimi, wala hakunizuilia kitu cho chote ila wewe, kwa kuwa wewe u mkewe. Nifanyeje ubaya huu mkubwa nikamkose Mungu?"*** Hili lilikuwa jibu la Yusufu kwa mke wa Potifa kuhusiana na jaribu la uzinzi.

**Mwanzo 50:20**, Yusufu alionesha roho ya msamaha kwa kaka zake. "***Nanyi kweli mlinikusudia mabaya, bali Mungu aliyakusudia kuwa mema, ili itokee kuokoa taifa kubwa, kama ilivyo leo."***

**Esta 4:14**, Mordekai alizungumza na mpwa wake Esta katika kipimo cha imani. "***…ni nani ajuaye kama wewe hukuujia ufalme kwa ajili ya wakati kama huo?"***

**Rani Timoti anaishi Auckland, New Zealand, na ni mwalimu wa darasa la wanawake na mwandishi.**



# Kielelezo cha Ukristo

**Neil Richey**

Bwana wangu alisema, (Mathayo 5:16). ***"Vivyo hivyo nuru yenu na iangaze mbele ya watu, wapate kuyaona matendo yenu mema, wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni."*** Kikubwa ninachoweza kusema, hakuna mpaka katika hili.

Kwa maneno mengine, kuangaza mbele ni mfano mzuri ambao haujazuiliwa katika jengo la kanisa, katika ibada ya Jumapili, au wakati ukaribu na marafiki wa kanisa. Ukweli uzungumzwe, pale ambapo ni muhimu sana kuiacha nuru yetu iangaze nyumbani, kazini, shuleni, na hata katika mitandao ya kijamii. Ukristo wa kweli unaangaza kutokea ndani na kuonekana kila sehemu na wakati wote.

Swali. Je, watu wanajua kuwa wewe ni Mkristo? Hawatakiwi kukuuliza. Wanapaswa kuwa na uwezo wa kukutolea ushahidi wao wenyewe. William Barclay aliandika. "Ukristo wetu unapaswa kuleta mabadiriko kwa namna tunavyoagiza chakula kutoka kwa wahudumu au tunavyomtendea mhudumu wa dukani. Ukristo unapaswa kuleta mabadiriko katika dhamira ya kazi yetu, na katika fadhila ambayo katika hiyo tunaitumikia jamii, na katika uzingatiaji pamoja nao tunaishi ndani ya nyumba zetu wenyewe."

Ukristo ni kazi ya kutwa nzima. Sio ya muda tu wa kutenda katika siku za Jumapili pekee. unahitaji tabia zetu njema kila siku. George Bailey (sio "Ni Maisha Mazuri" ndugu) alisema, "Hakuna kinachoambukiza zaidi kuliko mfano." Ni aina gani ya kielelzo

unachokiweka? Ni uambukizaji. Nini marafiki wanachochukua kutoka kwako?

**Neil Richey anahubiri katika kanisa la Kristo Piedmont Road huko Marietta, Georgia, Marekani.**

# Nini kinachomfanya Mtu kuwa Mtumishi wa Mungu?

**Bob Plunket**

1. **Mara nyingi wanaanza na wazazi mashuhuri.** Elkanah na Hannah walikuwa wazazi wa Samweli. Alikuwa tasa na hakuwa na uwezo wa kupata mtoto. Aliomba kwa bidii ili kwamba Bwana ampe mwana. Alisema, ***Kama utanipa mtoto wa kiume, nitamtoa kwako."*** Siku moja alipata ujauzito na baadaye kupata mtoto wa kiume. Alitunza ahadi yake. Alipomwachisha kunyonya, alimpeleka katika nyumba ya Mungu na kumkabidhi kwa Eli amfundishe. Ikiwa watoto wetu wanampenda Mungu na kumtumikia, lazima tuwapeleke katika nyumba Yake mara nyingi na mapema.
2. **Aliitikia wito wa Mungu.** Baadaye pindi Mungu alipomwita Samweli alisema, ***"Sema Bwana, mtumishi wako anasikiliza."*** Wengi mno leo wanasema, "Sikiliza, Bwana, mtumishi wako anasema."
3. **Mwaminifu katika kweli ya Mungu.** Samweli alilazimika kumwambia mzee Eli, mtu aliyempenda na mtu aliyemlea, kwamba Mungu alikuwa anakwenda kumwondoa na watoto wake kwa sababu watoto wake walikuwa waovu. Inahitaji ujasiri kuwaambia watu kwamba tunapenda vitu ambavyo hawataki kuvisikia. Baadaye angeliambia taifa, ***"Kama mkimgeukia Bwana kwa moyo wenu wote halafu mkajiondoa nafsi zenu na miungu ya kigeni."*** Katika sura ya 13 alilazimika kumkemea mfalme mpya wa Israeli.
4. **Mtu awezaye kumtia mafuta na kumbusu mtu wa mbadala wake.** Samweli aliumia kwa sababu alidhani kuwa Israeli walimkataa yeye, lakini Mungu alimwambia, ***"Wamenikataa mimi sio wewe."*** Mtumishi mwema wa Mungu alitambua kwamba kazi ya Mungu ni

kubwa kuliko mtu awaye yote, na alipenda zaidi matokeo ya Mungu kuliko yak wake.

5. **Mtu ajuaye wakati na jinsi ya kuaga.** Katika sura ya 12, Samweli alisema, ***"Mimi ni mzee na mwenye mvi. Nani ambaye ng'ombe wake au punda wake nimemchukua? Nani niliyemdanganya? Watu wakajibu, 'Hakuna mtu.'"*** Alikuwa mwaminifu.

Hakuna mahali popote panaposema alikuwa mrefu, mtanashati, fasaha, hodari, au mjanja, lakini badala yake ni kwamba alikuwa mwaminifu na mkweli. Sisi sote tunaweza kuwa hivyo. Zingatia kwa umakini 1 Samweli 1 – 13.

**Bob Plunket anahubiri katika kusanyiko la Colbert Heights huko Tuscumbia, Alabama, Marekani.**

# “Baba yangu, Mhubiri”

**Mark N. Posey**

Kifungu, ***“Enendeni ulimwenguni mwote, mkahubiri Injili kwa kila kiumbe,”*** kinatuita kila siku katika maisha yetu. Kuhubiri Injili ya Yesu ni taaluma kuu zaidi ya nyingine na ndiyo niliyoichagua “kuitenda” kwa siku zangu zote katika dunia hii.

Watu wengi wamechangia katika maisha yangu, kuna wale walionivutia, kunitia moyo, na kunipenda. Pamoja na hayo, hakuna mwingine kama baba yangu, mhubiri! Baba yangu hapendi kingine zaidi ya “kuhubiri Injili kwa kila kiumbe”. Kuhubiri kulikuwa kunaishi mbele ya macho yangu kila siku ya utoto wangu; kile nilichosikia katika mimbari ndicho nilichikiona nyumbani.

Katika ulimwengu wa unafiki, tunahitaji watu, wahubiri wa Injili, ambao wanatenda kile wanochohubiri. Niliona kwa baba yangu, mapema sana katika maisha, kile nilichotaka kuwa. Jambo zuri ni kwamba hakuwahi kubadilika au kuweka matatani kile alichohubiri au kile alichokiishi, na sijawahi kubadili kile nilichotaka kuwa. Maadam naweza kukumbuka, kitu pekee ambacho nimewahi kutaka kukifanya katika maisha yangu kilikuwa ni kuhubiri Injili; nilitaka kuwa kama baba yangu.

Tuzo za kuhubiri ni nyingi! Mhubiri anafanya kazi na watu bora zaidi, akitangaza ujumbe mkuu zaidi, na kumtumikia Mungu mwema zaidi. Mfano tunaouweka ni ule ambao wengi watauona. Mfano wa mhubiri niliouona, nia yake, matendo yake, na mawazo yake pekee yaliakisi wema na usafi. Niliona maisha ya utumwa, kutoa na kusamehe, na ya kusifu kwa mtu ambaye alikuwa hodari na mwenye nguvu.

Katika viapo vya ndoa ambavyo mke wangu na mimi tulipeana, baba yangu alisema, “Ndoa yenu na iwe nzuri, yenye furaha, na iwe mfano wa ndoa ya Kikristo ili wengine waweze kuona na kutaka kuingia

katika ndoa.” Vijana wadogo ulimwenguni mwote watavutwa na taaluma ya uhubiri ikiwa watakuwa na vielelezo vizuri vya uwajibikaji vya kuvitazama na kutamani. Ni wajibu mzuri kiasi gani uliopo katika maneno yetu, kuishi, na mifano!

Kama mwanangu Yoshua (Joshua) Posey sasa ni mhubiri wa kutwa nzima, najua hata kuvuka mashaka yote kwamba kielelezo changu katika neno na mwenendo unaangaliwa kila siku. Najua kwamba kama nikiishi maisha kama baba yangu alivyofanya, ambayo mhubiri katika mimbari na mhubiri nyumbani ni yuleyule, hapo nitaweka mbele yake mfano ambao ni pongezi katika taaluma ya kuhubiri na utukufu kwa Mungu.

Mungu na awabariki baba wote waishio maisha ya wema na usafi ili kuwainua wahubiri wa kesho. Baba, ahsante kwa kunionesha kwamba kazi ya uhubiri ni kazi bora katika ulimwengu.

**Mark N. Posey ni mhubiri wa kanisa la Kristo Austinville huko Decatur, Alabama, Marekani**

## Je, Ulijua?

Maneno ya Mungu, BiBLIA, yaliandikwa na watu 40 kwa takribani miaka 1,600. Watu hawa walikuwa tofauti tofauti, kutoka wavuvi hadi wafalme, kutoka watu wasiona elimu hadi waandishi waliokuwa na elimu kubwa. Pamoja na hayo, Biblia ni waraka mmoja uliounganika bila ya makosa. Ni Mungu pekee anayeweza kulifanya hilo liwezekane! Soma 2 Timotheo 3:16-17 na 2 Petro 1:20,21

# Sikufanya vya kutosha!

**Dayton Keesee**

Miaka kadhaa iliyopita makala kuhusu Oskar Schindler, aliyekuwa mwanachama wa chama cha Nazi (chama kilichokuwa kikiongaza nchini Ujerumani, hasa wakati wa utawala wa Adolf Hitler). Ni kisa kinachoumiza moyo cha mpito wa Schindler kutoka kufaidika, mtu wa kudumu kwenda kuwa mtu mwenye mapenzi kwa ajili ya kupotea. Kwa wakati muafaka, Myahudi mdogo, mwenye hekima, Itzhak Stern, alipanda mbegu ya mawazo katika moyo wa Schindler ambayo ilimbadilisha kutoka kuwa mvinyo, wanawake, na wimbo kuwa mfanya kazi wa kujitolea, kuunda orodha ambayo iliwaokoa Wayahudi 6,000 kutoka katika maangamizi makuu. Hawa 6,000 walijulikana kama Schandlerjuden "Wayahudi wa Schandler".

Aliwapeleka Wayahudi wakafanye kazi katika kiwanda, watengeneze vyungu na masufuria. Wayahudi zaidi ya 1,000 walisafirishwa kutoka Potland hadi Czechoslovakia ambapo aliwaweka wafanye kazi katika kambi ya kutengeneza maganda ya mizinga. Alitumia fedha zake kununua maisha ya watu hawa. Kwa sababu ya orodha ya Schindler  na kazi, Wayahudi walimtangaza kuwa "Mtu mtakatifu" katika mwaka wa 1961. Baada ya kifo chake, alizikwa Israel katika mwaka 1974.

Kisa kinaamsha roho ya mtu wakati wazo la nyongeza linapotolewa. Wakati Wayahudi walimchukulia kuwa ni shujaa, kamwe hakufarijiwa! Kwanini? Angalia katika muda ambapo Vita ya pili ya Dunia ilipoisha. Schindler na mkewe walilazimika kukimbia. Alipokuwa akienda katika gari yake, aweze kuondoka, aliifikiria orodha, na kulia, "Sikufanya vya kutosha! Gari hii…watu kumi sehemu ile!" Alibandua nembo ya Nazi kutoka katika koti la suti yake. "Pini hii ya dhahabu…watu wawili! mtu mmoja zaidi! Kwa machungu yaliyorudi mara kwa mara, alipiga magoti na kulia, "Mtu mmoja zaidi! Ningeweza kumpata mtu mmoja zaidi! Na sikufanya!" Katika wakati huo mbaya

Schindler angeweza kutoa dhahabu zake zote, mtu aliyeheshimika na mwenyenguvu ya kuweza kujiunga na Paulo kwa kusema ***"…mimi sina hatia kwa damu ya mtu awaye yote."*** (Mdo 20:26).

Ndugu msomaji, ni wangapi wetu wanaoweza kuhitaji kusema pamoja na Oskar Schindler, "Sikufanya vya kutosha"? nakumbushwa na wimbo ulioandikwa na B.B. Edmisston.

***"Kuna mtu anahitaji msaada wako,***
***Kuna mtu ana huzuni na mpweke;***
***Kuna mtu amechoka na dhaifu,***
***Kuna mtu amekaribia kuondoka.***
***Anayoyoma mbari, anakufa leo;***
***Kuna mtu, 'Ni mtu unayempenda;***
***Kwanini unasubiri? 'muda umekwenda sana,***
***Waoneshe juu mbinguni."***

Tendo jema la uokoaji lililofanyika leo litamaanisha baraka zaidi na furaha ya kesho (Yohana 13:17).

**Dayton Keesee ni mzee (askofu) katika kanisa la Bwana huko Choctaw, Oklahoma, Marekani**

# Kazi yangu iko wapi? **Louis Rushmore**

**Kazi yangu iko wapi?** Kama Mkristo, kazi yangu iko wapi (Mathayo 5:16)? Ni mbali sehemu fulani (Marko 16:15,16). Au ni karibu pia (Luka 10:25-37)? Kama baba, kazi yangu iko wapi (Waefeso 6:4)? Kama mume, kazi yangu iko wapi (Waefeso 5:25)? Kama mwinjilisti, kazi yangu iko wapi (Mdo 20:27)?

Kama umuhimu wa kuzingatia, **kazi yangu ni nini?** Kazi yangu ni nini kama Mkristo (Waefeso 5:8)? Kazi yangu ni nini kama baba (Kum 6:7)? Kazi yangu ni nini kama mume (1 Petro 3:7)? Kazi yangu ni nini kama mwinjilisti (2 Timotheo 4:2)?

Zaidi sana, **mimi ni mmishonari kwa ajili ya nani** (Wakolosai 3:24)? Ni mimi natakiwa kijipendeza mwenyewe (Wagalatia 1:10), au kuna mwingine ambaye natamani kibari chake (Yohana 12:26)?

Kwa hakika, hakuna uungwana kuliko ule wa Bwana wetu Yesu Kristo, (2 Wakorintho 12:10)! (2 Wakorintho 4:5).

# Ndoa Kipimo cha Jaribu?

**Dnny Boggs**

Daima najisikia kuheshimiwa kwa kualikwa kuhudumia sherehe za harusi. Napenda kuwasaidia watu kufanya makubaliano ya busara na Mungu, pia wao kwa wao, na hapo hupata furaha na ulinzi ambao kwa ajili hiyo aliitengeneza mahusiano ya ndoa. Wakati mwingine, kujitoa kwangu kusaidia kuleta pekee aina za ndoa ambazo Biblia inaruhusu zinaniweka katika mazingira magumu.

Pindi mwanamke mpendwa ambaye tayari aliolewa mara ya kwanza, tayari alipata mtoto kutoka katika ndoa, na tayari walikuwa wakiishi pamoja kwa miaka kadhaa iliyopita na yuko na mwanaume mwingine kwa sasa akitaka kuolewa naye, aliinita kwa ghafla na kuniomba niwe mtu wa kati katika sherehe. Sikuweza. Mazingira yanayozunguka talaka yake yalikuwa na kiulizo. Mara ya kwanza alichagua mwenza katika hali dhaifu sana, na kila mtu aliyemjua yule mwanaume alijua hili kabla uamuzi huo kufanywa. Bado hajajifunza kuchagua kwa hekima zaidi.

Alikuwa akitukanwa mara nyingi kwa namna nyingi na mwanaume ambaye sasa anataka kumfanya awe mumewe, na kwa vipindi ambavyo hawakuishi pamoja vilikuwa kwa sababu ya ukweli kwamba huyo mwanaume alimfukuza. Huyo mwanamke hakuwa Mkristo. Nilimshirikisha mafunzo ya Biblia. Nilimwelezea kutoka katika Biblia kwamba mpango wa Mungu kuhusu ndoa ni mwanaume mmoja na mwanamke mmoja kwa maisha (Mathayo 19:4-6). Nilifikiri, kama ilivyo kawaida ya visa, kwa kuwa walikuwa wakiishi pamoja pia walikuwa wakijihusisha na mahusiano ya kingono, zawadi ambayo Mungu alihifadhi kwa ajili ya wale ambao wameoana kwa mamlaka yake ya kibiblia. Sikuwa najua kwamba alikuwa mjamzito pindi aliponiita. Hakuonesha kuvutiwa na msaada wangu kumsaidia awe na

uhusiano sahihi na Bwana. Badaye, nilimwendea nikiwa na maelezo ya kidunia ambayo pekee yanashirikiana na mafundisho ya kiroho ya Biblia.

Nadhani kila mmoja anapaswa kutunza haya maelezo katika kasha (file) kama kumbukumbu kwao wenyewe au ili kuwasaidia wengine. Wakati wa sensa ya mwaka 2000 ilikuta kwamba watu wanaishi na washirika waliotofauti kijinsia bila ya kuwa wameoana kwa idadi (4,571,992 wanafanya hivyo Marekani). Wachunguzi wamegundua kwamba imani zilizoko kwa watu wengi wanaoishi kinyumba wanakosea. Katika makala yenye kichwa cha habari *“Mama, Nataka Kuishi na Rafiki yangu wa kiume” (Mmeng’enyo wa Msomaji 1994, 77-80).* K.C. Scott alishirikisha ugunduzi huu uliopatika kutoka katika masomo mengi:

- Makadirio ni kwamba si zaidi ya 50% ya wenza ambao wanaishi pamoja watafunga fundo katika darasa moja, pekee 19% ya wanaume katika mahusiano ya jinsi hiyo walifanya.
- Ikiwa kuishi pamoja ni ndoa, wako kwenye hatari kubwa ya talaka. Katika taarifa iliyotolewa na *Mradi wa Taifa wa Ndoa* uliofanywa na *Chuo kikuu cha Rutgers katika mwaka 2002.* Nasoma kwamba talaka ni 46% zaidi sana ambapo wenza kwanza wanaishi pamoja. Kwa hakika tunaweza kuona kwamba kuishi pamoja si mafunzo mazuri kwa ajili ya ndoa.
- Kuachana kunaweza kuumiza sana kama tu vile talaka.
- Hata kama wakioana, kwa kawaida wanafuraha kidogo.
- Kuishi kinyumba kunaweza kupelekea kukosekana kwa utulivu, ikijumuisha vurugu.
- Kuishi pamoja huzaa matatizo ya ndoa bila ya tuzo.
- Kuishi pamoja kunaweza kuua mahaba.

Katika hali fulani, kuishi pamoja bila kuoana kunaashiria ujinga wa kutokujua mpango wa Mungu, na toba ya haraka juu ya kusikia ushahidi wa kweli wa mioyo mizuri ya wale ambao hakufahamishwa, kwa neema ya Mungu wenza hao wanaweza kustawi katika ndoa.

Katika visa vingi, vipaumbele, na mpango wa Mungu kwa ajili ya ndoa hautiliwi maanani. Ahadi (kujitoa) na tabia ambazo zinafanya ndoa nzuri zinakosekana katika mpangilio wa kuishi kinyumba, na ni vigumu kuondoa vifungo dhaifu vya uhusiano kama mnaishi pamoja mwishowe hutoa njia kwenda katika ndoa. Ndoa zinazodumu hazitokani na kipimo cha chupa hizo za majaribu.

**Katika mazingira mengine, kuishi pamoja bila ya kuwa mmeoana inaashiria ujinga wa kutoelewa mpango wa Mungu, na toba ya haraka juu ya kusikia ukweli wa ushahidi mioyo mizuri ya wale waliokuwa hawajafahamishwa; kwa neema ya Mungu wenzi hao wanaweza kustawi katika ndoa.**

Kwenda na mshirika wa jinsia tofauti pekee kunakusudia kumsogeza mtu mbali na Mungu. Mungu anataka kilicho bora kwa ajili yetu. Daima anajua nini anachokizungumzia.

**Dnny Boggs anahubiri katika kanisa la Hillcrest huko Neosho, Missouri, Marekani**

# Familia Yako Inaendeleaje?

## John Gipson

**Familia ni chanzo na usimamizi wa maisha ya baadaye.** Mwana saikolijia maarufu, H.A. Ovaerstreet, amefafanua familia kama eneo ambalo mtoto anaweza kukua, kutoka ujinga kuelekea maarifa, kutoka kutokuwa na majukumu kwenda kuwa na majukumu, kutoka kutengwa kwa mazungumzo hadi mawasiliano, kutoka hali ya kutopevuka hadi kupevuka, kutoka kuwa mbinafsi hadi kujali wengine, na kutoka kuona jambo moja hadi kuona yote.

Kama unafikiri familia si muhimu, sasa kwanini Biblia inayo mengi ya kusema kuhusu waume, akina baba, wake, akina mama, na watoto?



katika kila mkono tunavuna mazao yaliyopandwa na familia zinazougua. Kukosekana kwa upendo kumezalisha wavulana na mabinti ambao hawakufundishwa, kutiwa moyo, kusahihishwa, kunidhamishwa, au kuonywa. Kwa upande, familia hii isiyo na afya ya maisha imeleta mwanga katika shule zetu, katika sehemu zetu za kazi, makanisa yetu, na katika jamii yetu kwa ujumla.

Tunaweka wagunduzi wa chuma kuwachunguza wanafunzi wanaoleta silaha shuleni, tunaunda programu za ukarabati kwa ajili ya waraibu wa madawa ya kulevya na tunatunga sheria mpya kusimamia ulevi na uendesheji magari. Hapo hapo tunatafakari kuhalalisha

madawa na tunahalalisha utoaji mimba, na tunatangaza (tukuza) “ngono salama”; tunatafuta tiba ya UKIMWI; na hadithi inaendelea.

Matatizo yetu hayatatatuliwa mpaka tutakapozifanya familia zetu kuwa kamili.

**John Gipson anafanya kazi na Windsong kanisa la Kristo huko Litle Rock, Arkansas, Marekani**

# Okoa Ndoa

Dale Grissom

Kuna ongezeko la talaka miongoni mwa Wakristo na ushawishi wa dunia unaokua katika kanisa. Wakati mwingine maisha yanaonekana kukosa mwelekeo, na mmoja au wana ndoa wote wawili wanaweza kufikia hatua ambapo wanakuwa na ugumu sana kuwa sawa. Njia za mawasiliano zimefungwa, na hawawezi kuongeleshana bila ya kuumia na kutokuelewana. Kwa kawaida, kwa hatua hii, kiburi na usumbufu huchukua nafasi na wenzi kuhitaji msaada.

Ndoa nyingi zinaweza kuokolewa ikiwa washirika wote wawili wakiwa kweli wanataka ndoa yao iendelee, na ikiwa wako tayari kuweka kando usumbufu na kiburi ambavyo huingilia njia yao. Ushauri wa Kikristo unaweza kuwa wa faida nzuri kama wote wataridhia. Ufunguo ni kwamba wote wawe na shauku ya kuiokoa ndoa yao.

Ndoa ya Kikristo inakuwa yenye tatizo pale ambapo wanandoa wanaanza kwenda mbali na Bwana. Wakati mwingine wanaanza kupuuzia ibada, na katika maisha yao binafsi wanapuuzia kusali, kutafakuri, na kujifunza Biblia. Upuuziaji hufungua mlango wa dhambi, na wakati dhambi inapoingia, inaleta kuumiza na maumivu. Kufikiri kwao kunakuwa na wasiwasi. Wanakuwa na ugumu wa kupata njia ya kurudisha uhusiano imara bila ya msaada wa Mkristo mwema na Mshauri.

Hakuna kinachowafaidisha wana ndoa zaidi kuliko kumwamini Mungu na kuwa na uwezo wa kumtwika mizigo yeye (Mungu). Anatuongoza kwa kupitia Neno lake, kwa sababu Biblia ni kitabu kikuu kuwahi kuandikwa, masomo bora ya saikolojia yanapatikana katika kitabu hiki. Ndoa nzuri hazipatikani kwa ajali, bali ni matokeo ya kufanya kazi kwa bidii. Waume na wake lazima waweke kando kiburi

na majivuno, na kuvaa unyenyekevu, ambao unatuwezesha kutoa jibu zuri. Kanuni ya Dhahabu ni lazima kwa wale wanaotamani kuwa na ndoa nzuri. ***"Basi yo yote myatakayo mtendewe na watu, nanyi watendeeni vivyo hivyo;.."*** (Mathayo 7:12) kulizingatia hilo kutafanya kila ndoa kukua vizuri kadiri miaka ipitavyo.

Fanya suluhu kubaki karibu na Mungu na kufanya kazi kwa bidii kujenga ndoa nzuri. **Vuta pamoja na mbaki pamoja!**

**Dale Grissom (1927-2014) alikuwa ni mtenda kazi aliyejitoa kwa Bwana kama alivyotumika kwa miaka mingi katika kanisa la Bwana huko Dexter, Missouri, Marekani.**



# DAKIKA 5 ZA KUJIFUNZA BIBLIA

Paula Bates

## Shukurani

1. “wenye shina na wenye kujengwa katika yeye; mmefanywa imara kwa…………………., kama…………………………; mkizidi…………………………….” Wakolosai 2:7
2. “……………………..kwa neno lo lote; bali katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru,………………..zenu na zijulikane na Mungu.” Wafilipi 4:6
3. “Ingieni malangoni mwake kwa kushukuru; ……………..mwake kwa……………..; ………………………., lihimidini jina lake;” Zaburi 100:4
4. “Mungu ashukuriwe kwa sababu ya………….. chake, tusichoweza kukisifu kama ipasavyo.” 2 Wakorintho 9:15
5. “ Wakati ule Yesu akajibu, akasema, Nakushukuru,……………., Bwana wa mbingu na nchi, kwa kuwa mambo haya………………….. wenye hekima na akili, ukawafunulia……………………………………………..” Mathayo 11:25
6. “ Kwa sababu mambo yake yasiyoonekana tangu kuumbwa ulimwengu ………………………, na kufahamika kwa kazi zake; yaani, uweza wake wa………………… na Uungu wake; hata wasiwe na udhuru; kwa sababu, walipomjua Mungu …………………………………. kama ndiye Mungu wala …………………………..; bali walipotea katika uzushi wao, na mioyo yao yenye ujinga ikatiwa giza.” Warumi 1:20,21

**Majibu:**

1. Imani, mlivyofundishwa, shukrani.
2. Msisumbukie, haja.
3. Nyuani, kusifu, Mkishukuru.
4. Kipawa
5. Baba, uliwaficha, watoto wachanga.
6. Yanaonekana, milele, kumshukuru.

# SURA YA FURAHA KATIKA BIBLIA

## David Shannon

Kama ilivyo 1 Wakorintho 13 inachukuliwa kama "Sura ya Upendo" ya Biblia, kwa nini Luka 15 inaitwa "Sura ya Furaha" ya Biblia?

Luka 15 inahusu nini? Unaweza kujibu kwamba inahusu mpotevu aliyepatikana? Hiyo ni sahihi, lakini kama ungejibu swali hili kwa kuegemea msisitizo kupitia maudhui yanayojirudia, jibu lingetakiwa



kuwa tofauti kidogo. Luka 15 ni sura inayohusu furaha iliyopitiwa pindi mpotevu alipopatikana. Katika mfano huu Yesu anasimulia visa vitatu.

**Uthibitisho katika kisa cha Kwanza:** Kisa cha kondoo mmoja kupotea kutoka kwa wengine 99 kinasimuliwa katika aya 1,5. furaha iliyojaa aya 2,5. karibia mara mbili ya muda unatumika katika kufurahi. Kwanza mchungaji anafurahi



anapomweka kondoo mabegani mwake. Halafu, anawaita marafiki na majirani kufurahi. Baadaye, Yesu anafupisha kisa chote katika Aya ya Saba. Hakuelezea utafutaji, aliyepotea, au mchungaji. Yesu aliezea furaha iliyoko mbinguni wakati mwenye dhambi aliyepotea anapotubu.

Uthibitisho katika kisa cha Pili: Kisa cha mwanamke anayetafuta sarafu iliyopotea kinasimuliwa katika aya moja. Mara mbili kama aya nyingi zinavyoelezea kufurahi. Aya ya tisa inaelezea wito wake kuwaita rafiki zake na majirani kufurahi pamoja naye, na aya ya 10 inatoa muhtasari kama kisa kilichopita. Aya ya 10 inaelezea furaha

wanayoipitia malaika mbele za Mungu kwa sababu mwenye dhambi anatubu.

**Uthibitisho katika kisa cha Tatu:** Kisa cha tatu ni kirefu sana na mara nyingi kinachukuliwa kama moja ya visa vizuri zaidi na kifupi kuwahi kuandikwa. Kila kirai ni kama pigo la furaha ya uchoraji mkuu wa msanii katika nyumba ya Baba.



Kwa aya tisa maisha ya mwana mpotevu yanaelezewa. Aya tano zifuatazo zinaelezea hali ya Baba wakati mwanawe aliporudi. Katika neno ilikuwa "furaha". Mtoto mkubwa hakuwa na furaha kuhusu furaha ya Baba yake au kurudi kwa ndugu yake. Aya ya mwisho ya sura inafupisha mazungumzo ya Baba na ya ndugu yake. Pia inafupisha kisa. Vivyo hivyo inafupisha hoja ya visa vyote katika mifano mitatu. "***Tena, kufanya furaha na shangwe ilipasa, kwa kuwa huyu ndugu yako alikuwa amekufa, naye amefufuka; alikuwa amepotea, naye ameonekana."***

Nini kinapaswa kuleta furaha ya kweli katika maisha yako? Kuza moyo unaovumulia sana kwa ajili ya mpotevu kurudi nyumbani pale ambapo watafanya hivyo, furaha yako inafanana na furaha iliyoko Mbinguni. Nastahajabu ni mara ngapi Paulo alifikiria mfano wa Yesu

alipoandika maelezo kama vile "***Maana tumaini letu, au furaha yetu, au taji ya kujionea fahari, ni nini? Je! Si ninyi, mbele za Bwana wetu Yesu, wakati wa kuja kwake? Maana ninyi ndinyi utukufu wetu, na furaha yetu."*** (1 Wathesalonike 2:19,20).

Wewe ni aina ya "ndugu mzee" au "Baba"? Hebu angalia nini kinachokufanya uwe na furaha na utajua ni vipi ulivyo. Na tufanye kwa "usahihi" (Aya ya 32).

**David Shannon anahubiri katika kanisa la Kristo Mt. Juliet huko Mt. Juliet, Tennessee, Marekani**

MAFUNZO KATIKA KIFUNGU

# Mwisho wa Yote

**Jim Laws**

***"Hii ndiyo jumla ya maneno; yote yamekwisha sikiwa; Mche Mungu, nawe uzishike amri zake, Maana kwa jumla ndiyo impasayo mtu. Kwa maana Mungu ataleta hukumuni kila kazi, pamoja na kila neno la siri, likiwa jema au likiwa baya."*** (Mhubiri 12:13,14). Bilashaka hii siyo mara ya kwanza kwa wewe kusoma kifungu hiki cha Biblia kinachovutia. Kinatoka katika kitabu cha Mhubiri, ambacho ni kitabu cha ushairi kilicho andikwa na Sulemani. Kimepitia mambo muhimu sana ya maisha na kuja katika hitimisho ulilolisoma hapo juu. Aliandika kama mtu anayefanya kazi, kana kwamba aliweza kuuelewa ulimwengu. Mwandishi aligundua ukweli maisha hayana maana ikiwa mtu anaishi nje ya Mungu. Tunaposoma kifungu hiki, ambacho hutumika kama aina ya maelezo ya hitimisho kwa uzoefu wote wa maisha ya kuishi, tunapata makundi mawili ambayo yanahitaji kuelezewa.

Katika kundi la kwanza ni **mambo tunayopaswa kuyafanya**. Angalia kifungu tena uone kama unaweza kuchukua hoja hizi muhimu. Kwanza, alitaja ukweli tunapaswa ***"kumcha Mungu".*** Hii haimaanishi kwamba tunapaswa kumhofia Mungu kama nyoka au mnyama mkali, bali tunapaswa kumstahi sana, kumheshimu, na kumchukulia kwa uzito wa juu. Yesu aliwafundisha wanafunzi kusali ***"Baba yetu uliye mbinguni, jina lako litukuzwe."*** Mwenye hekima anatukumbusha ***"Kumcha BWANA ni chanzo cha maarifa,..."*** (Mithali 1:7).

Pili, alituambia ***"tushike amri zake".*** Amri mbalimbali za Mungu; hata hivyo, zinaweza kufupishwa kwa amri mbli. Ya kwanza, ***"nawe mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote, na kwa nguvu zako zote".*** Yapili ni, ***"Mpende jirani yako kama nafsi yako…"*** (Marko 12:30,31). Katika kundi la pili ndizo sababu zilizoteuliwa kwa ajili ya mambo

tunayopaswa kuyafanya. Angalia maelezo yake kuhusu ***"jumla ya kazi yote ya mwanadamu".*** Azimio hili linafanya kazi kama aina ya maelezo ya lengo kwa ajili ya wajibu wa hapo juu. Hii ndiyo jumla na kiini cha maisha na hiyo ni nzuri sana. ukimpenda Mungu aliye mkuu, utamtii kwa furaha. Unaona, sio mzigo kumtii mtu unayempenda (Yohana 14:15; 15:14; 1 Yohana 5:3). kama ukimpenda jirani yako kama nafsi yako, hutamdhuru (Warumi 13:8-10), kwa kweli, utamsaidia safarini (Luka 10:25-37). Zaidi sana, alifunua ukweli tunaojifunza kutoka katika Agano Jipya (kwa mfano, matendo tunayoyafanya sasa yatafufuka na kutufuata). Anasema, *"Kwa maana Mungu ataleta hukumuni kila kazi, pamoja na kila neno la siri,.."*

Kile tunachokifanya katika maisha haya kitaendelea kutufuata. Matendo yetu yatatufuata hata upande mwingine wa maisha. Katika Siku kuu ya mwisho, yatasimama kama mashahidi mbele ya Kiti cha enzi. Matendo yetu yatashuhudia upande wetu au kinyume chetu. Matendo ya hekima yatazungumza kwa niaba yetu, matendo maovu kinyume chetu (2 Wakorintho 5:10).

Mchanganuo wa sehemu zake, kifungu kizuri cha Andiko kimegunduliwa. Aya hii inaweza kuwa ni muhtasari, lakini imejaa hisia ya kweli, ambayo ndiyo tunayoipata katika vifungu vyote tunavyojifunza kwa umakini.

**Jim Laws ni mhubiri katika kusanyiko la Bwana Brodadway huko Tyler, Texas, Marekani**

## Kwanini Waliitwa Wakristo? Jerry Bates

Katika Mdo 11:26, tunapata maelezo ya kuvutia, ***"Na wanafunzi waliitwa Wakristo kwanza hapo Antiokia."*** Petro alisema kuwa tunapaswa kujivuna kulivaa jina hilo. "Lakini ikiwa kwa sababu ni Mkristo asione haya, bali amtukuze Mungu katika jina hilo." (1 Petro 4:16).

Kwa nini wanafunzi wa kwanza waliitwa Wakristo kwanza hapo Antiokia badala ya Yerusalemu? Kwanza kabisa, kanisa lilikuwepo kwa miaka kadhaa (inawezekana ni miaka 10), kwa hiyo kwanini jina lilitolewa au kupatikana hapo Antiokia baada ya miaka kadhaa badala ya Yerusalemu? Kwanza, Kanisa liliundwa na Wayahudi pekee na lilikuwa linachukuliwa kuwa ni madhehebu ya Wayahudi. Hata hivyo, hapo Antiokia, muundo huu usingefaa kwa sababu hili lilikuwa kanisa la kwanza kuwa la Mataifa (watu wa mataifa). Hawakuwa Wayahudi kuliko walivyokuwa wapagani. Wote Wayahudi na Mataifa sasa walikutana katika istilahi sawa, kwa hiyo jina jipya lilitakiwa kuwatambua hawa watu. Sasa ukabila uliondolewa kwa utambulisho wa Kristo. Ujumbe wa Luka katika Mdo 11:26 ni kwamba kanisa lilitambuliwa sana kwa (jina la) Kristo kiasi kwamba hata watu wa nje hawakuweza kupata nembo bora ya kulipachika kundi hili.

Tunahitaji kuunganishwa kwa undani zaidi na Kristo ambapo ukweli unatakiwa uwe vilevile hata leo. Pindi watu watuonapo na kutazama maisha yetu, kwa haraka sana wanapaswa kufikiri kuhusu mafundisho ya Yesu na kututambua kwa Yeye. Huu ndio ukweli wa maisha yako?

# Je, Majibu Haya Yanafaa?

Betty Burton Choate

Huu ni uchambuzi mfupi wa mada za Biblia, nataka kutoa baadhi ya hoja za wazi ambazo zinaweza kutusaidia kutuleta katika hitimisho.

## Vipi kuhusu "Injili" ambazo zinamsimulia Yesu akifanya miujiza kama Mwana

Yesu mwenyewe alionya katika Mathayo 12:22-32 kwamba kumkufuru Roho Mtakatifu hakusamehewi. Nini kiliharakisha onyo hilo? Mashitaka ya Mafarisayo kwamba alikuwa akitoa pepo kwa uwezo wa Beelzebuli. Maonyo yake yalitambulisha nguvu ambayo kwayo alifanya miujiza, kwa Roho Mtakatifu aliyemjia ***"bila kipimo"*** (Yohana 3:24) katika wakati wa ubatizo wake. Yohana 14:24 inafundisha ***"…neno mnalolisikia silo langu, ila ni lake Baba aliyenipeleka."*** Ilikuwa ni katika ubatizo wa Yesu ambapo Mungu aliongea kutoka Mbinguni na hapo Roho Mtakatifu akamshukia Kristo. **Kabla ya ubatizo wake, hakuna kumbukumbu yoyote ya kibiblia ya uvuvio wa fundisho lolote au muujiza wowote.** Yeye mwenyewe alihusisha maneno yake na matendo yake kwa **Baba** na kwa **Roho Mtakatifu**, sio kwa matumizi ya nguvu zake mwenyewe. Wafilipi 2:5-7 na Waebrania 2:17 zinaonesha kwamba katika mwili alimtegemea Mungu, kama sisi tulivyo.

## Mwizi msalabani aliokoka bila kubatizwa?

Mara nyingi dhana huundwa kwamba mwizi aliokolewa bila kubatizwa, na kwa hiyo hilo linapaswa kuwezekana leo. Dhana ya jinsi hiyo inakosa mambo mawili muhimu: (1) Mwizi aliishi na kufa kabla Agano Jipya halijaanza kufanya kazi na kutiwa muhuri kwa damu ya Kristo. Kama ilivyooneshwa kwa kurudiwarudiwa katika vitabu vya

Injili, Yesu kama Mungu alikuwa na mamlaka ya kusamehe dhambi (Marko 2:3-12).

(2) Uligundua nini kuhusu alichokisema yule mwizi? Angali akiwa juu, akifa msalabani na kujua kuwa Yesu pia alikuwa katika kufa, alimtaja kama ***"Bwana"!*** ni wazi, hii haikuwa mara ya kwanza kwa mwizi kukutana na Yesu na dai lake la kuwa Yeye ni Mwana wa Mungu! Ingawa kundi la mitume inaelekea walipoteza kuona kila kitu ambacho Yesu alikuwa amefundisha kuhusu kuanzisha ufalme wake, mwizi alimwomba amkumbuke pindi ajapo katika ufalme wake! Hii inaonesha kwamba si tu kwamba alijua kuhusu ujumbe wa Yesu, bali kwamba alielewa kuwa ahadi ya ufalme ilikuwa ni ya kiroho ambayo isingeweza kuharibiwa kwa kifo cha mwanzilishi wake! Ni maarifa makubwa na imani kubwa!

## "Mhubiri Kristo lakini sio kanisa"

Kanisa, kwa kweli, ni ufalme ulioahidiwa, kama inavyofahamika katika Mathayo 18:19, Mathayo 3:2 inasema kwamba Yohana alikuja akihubiri, ***"Tubuni kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia!"*** Mathayo 4:17 inatupa somo la hotuba za Yesu: ***"Tubuni kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia!"*** ikiwa mtu atachukua muda kusoma vitabu vya Injili na kupigia mstari kila kifungu ambapo Yesu alihubiri kuhusu yeye mwenyewe na jinsi alivyo, na vifungu ambapo alihubiri kuhusu ufalme, ujumbe uko wazi. Kanisa lilipatikana katika mwamba ukweli kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu, kama Petro alivyokiri katika Mathayo 16:16. Mtazamo wa Yesu, hata hivyo, ulikuwa ni maisha mapya ya kiroho aliyokuwa akiyaleta ulimwenguni kwa kuanzisha ufalme, kanisa, ili kwamba wote watakaosikia waweze kuiacha dunia na kuzaliwa katika familia ya Mungu. Hatuwezi kumhubiri Kristo bila ya kuhubiri kanisa!

## Fundisho letu lazima liwe la upendo, kama Yesu siku zote alivyoonesha upendo

Ndiyo, daima ujumbe wetu lazima uruhusiwe kwa upendo ambao ulimleta Yesu ulimwenguni na ambao ulimpeleka msalabani. Ni lazima

tutekeleze uvumilivu na huruma kwa kadiri tunavyoshiriki ile Kweli na wale ambao hawajasikia na kuelewa. Hata hivyo, umegundua ni uvumilivu mdogo kiasi gani Yesu aliokuwanao kwa waalimu wa uongo na wanafiki? Pitia vitabu vya Injili na hesabu mara zote alipojibu baadhi ya maelezo kama ***"Ole wenu, Mafarisayo, wanafiki…" "Ole wenu, viongozi vipofu…" "Wapumbavu ninyi na vipofu…"*** (Mathayo 23).

## Nani aliandika kitabu cha Waebrania?

Mara nyingi inajumlishwa kwamba Paulo aliandika Kitabu cha Waebrania, hata ingawa kinakosa utambulisho alioutoa katika nyaraka alizoziandika. Pamoja na hayo, mtu aliyeandika alisema katika 2:3, ***"sisi je! Tutapataje kupona, tusipojali wokovu mkuu namna hii? Ambao kwanza ulinenwa na Bwana, kisha ukathibitika kwetu na wale waliosikia;"*** Ni wazi, mtu aliyeandika hakuwa mtume, na uelewa wake kuhusu mafundisho ya Kristo yalithibitishwa kwake ***"na wale waliosikia (waliosikia kutoka kwa Kristo)",*** Hata hivyo, katika Wagalatia 1:12 Paulo alisema, ***"…injili hiyo niliyowahubiri, nawajulisha ya kuwa siyo ya namna ya kibinadamu. Kwa kuwa sikuipokea kwa mwanadamu wala sikufundishwa na mwanadamu, bali kwa ufunuo wa Yesu Kristo.."*** Mistari 15-18 inatufahamisha kwamba baada ya ubatizo wa Paulo, alikaa kwa kipimo sawa cha muda akijitenga huko Uarabuni na Dameski kama ilivyokuwa kwa mitume wengine pamoja na Yesu kipindi cha huduma Yake duniani. Ilikuwa mwisho wa muda ule tu ambapo Paulo alikwenda Yerusalemu na kukutana na Petro. Kwa kuwa kitabu cha Waebrania ni somo la umakini la kutofautisha baina ya Sheria ya Kale na Mpya, huenda Apolo alikuwa mwandishi, kwa kuwa alikuwa ***"…hodari katika Maandiko."*** (Mdo 18:24).

## Kutakuwa na ishara zinazoashiria ujio wa Kristo?

Waalimu wengi wa uongo wanazitaja ishara na kuweka tarehe, wakitangaza kwamba wanajua kipindi ambacho Kristo atarudi. Katika hali ambayo, kwa ujasiri wanadai kujua zaidi kuliko Yesu alivyojua, kwa

maana alisema katika Mathayo 24:36, ***"Walakini habari ya siku ile na saa ile hakuna aijuaye, hata malaika walio mbinguni, wala Mwana, ila Baba peke yake."*** Watu watakuwa wakioana na kula na kunywa, ikionekana kawaida kuhusu mambo ya kila siku. Hata zaidi, kuna mkazo katika maelezo yake. Itakuwa kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu! Nuhu aliishi katika ulimwengu wa aina gani? ***"Bwana akaona ya kuwa maovu ya mwanadamu ni makubwa duniani na kwamba kila kusudi analowaza moyoni mwake ni baya tu sikuzote.*** (Mwanzo 6:5. Nuhu alihubiri kwa muda gani bila ya mtu kuongoka? Inaonekana kwamba Bwana atarudi wakati ambapo kuna uovu kila sehemu, wakati huo kiasi kwamba waliookoka watakuwa wachache, na hakuna roho itafutayo ukweli.

## Kwa nani na kwa kupitia nani tunapaswa kuomba?

Tunasikia Wakristo wazoefu wakiomba, "Baba yetu, tunakushukuru kwa kwa ajili ya mwili wako ambao uliangikwa kwa ajili yetu…kwa damu yako ambayo ilimwagika kwa ajili yetu…" au wanaomba, 'Baba yetu" na halafu wanahitimisha, "katika jina lako takatifu". Kwa uwazi Maandiko yanaonesha **Uungu:** Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu (Mathayo 28:19), katika Roho (Warumi 8:26) tunaomba kwa Baba, kwa kupitia upatanishi wa Mwana (Yohana 16:23). Mungu Baba hakufa kwa ajili yetu, bali Mwanawe, Yesu Kristo alitoa mwili wake, na tunaomba katika jina lake. Tafadhali, tuwe wa kimaandiko katika sala zetu!

**Betty B. Choate anafanya kazi na timu ya Uinjilisti Duniani huko Winona, Mississippi, Marekani**




# Mwokotezaji Mawindo

## Kupitia Daniel

**(Majibu ndani ya gamba la nyuma)**

1. Miaka mingapi ya mafunzo mfalme aliagiza kwa ajili ya mateka vijana wa Yuda?
2. Taja majina ya Kiebrania ya Shadraka, Meshaki, na Abednego.
3. Taja nyenzo ambazo zilitumika kutengenezea sanamu katika ndoto ya mfalme Nebukadneza.
4. Taja ala zilizopigwa kuwaashiria watu kuwa ni lazima waisujudie sanamu ya dhahabu iliyosimamishwa na mfalme Nebukadneza.
5. Tanuru ilitiwa moto mara ngapi kuliko desturi yake pale ambapo Shadraka, Meshaki, na Abednego walipogoma kuisujudia sanamu ya dhahabu?
6. Taja tuzo mfalme Nebukadneza aliyoiahidi kwa mtu atakayetafsiri maandishi ya kiganja yaliyoandikwa kwenye ukuta.
7. Kwa siku ngapi tangazo liliharamisha mtu kuomba dua kwa yeyote mwingine zaidi ya mfalme Dario?
8. Danieli alimwomba Mungu mara ngapi kwa siku mbele ya dirisha akikabili Yerusalemu?
9. Nani alitupwa kwenye tundu la simba baada ya Danieli?
10. Wataje wafalme wa kigeni ambao Danieli alitumika chini yao.

# Hivi Sivyo Jinsi Unavyoanza

Jimmy Clark

***"Bali mwenye haki atakapoghairi, na kuiacha haki yake, na kutenda uovu, na kufanya machukizo yote kama yale afanyayo mtu mwovu, je, ataishi? Katika matendo yake yote ya haki aliyoyatenda halitakumbukwa hata mojawapo. Katika kosa lile alilolikosa, naam, katika dhambi yake aliyoitenda, atakufa."*** (Ezekieli 18:24).

Petro aliandika, ***"Kwa maana wale waliokwisha kuyakimbia machafu ya dunia kwa kumjua Bwana na Mwokozi Yesu Kristo, kama wakinaswa tena na kushindwa, hali yao ya mwisho imekuwa mbaya kuliko ile ya kwanza. Maana ingekuwa heri kwao kama wasingaliijua njia ya haki, kuliko kuijua, kisha kuiacha ile amri takatifu waliyopewa."*** (2 Petro 2:20,21).

Zingatia baadhi ya mifano ya kibiblia ya baadhi (ya watu) ambao walianza kwa imani, lakini mwishoni walianguka.

**1. Mfalme wa kisiasa Sauli.** Sauli, mwana wa Kishi, alianza kwa unyenyekevu sana na mwanzoni alikuwa mtumishi mzuri wa Mungu. Imeandikwa kuhusu yeye pindi Samweli alipokuwa akimleta mbele ya taifa, ***"Basi wakazidi kumwuliza Bwana, Amebaki mtu asiyekuja huku bado? Naye Bwana akajibu, Tazama, amejificha penye mizigo."*** (1 Samweli 10:22). Sauli alikuwa mwaminifu katika suala la ushindi dhidi ya Waamoni na dhidi ya Yabesh-gileadi (1 Samweli 11). Hata hivyo, mwishowe Sauli aliacha nguvu ya kuwa mfalme imtawale. Aliacha amri ya Bwana na kumwambia Samweli, "***Akasema, Nimekosa; lakini uniheshimu sasa, nakuomba, mbele ya wazee wa watu wangu, na mbele ya Israeli, rudi pamoja nami, nimwabudu***

***Bwana, Mungu wako."*** (1 Samweli 15:30). Taarifa yake ya kujirudia ya kujaribu kumwua mtumishi mwaminifu Daudi inaonesha badiliko lake la moyo kutoka kuwa mwenye haki hadi kuwa mwasi. Mwisho wake unaonesha huzuni inayofunga kwa kiongozi ambaye aliwahi kuahidiwa (1 Samweli 31:4). Mwanzo wake ulikuwa mzuri kuliko mwisho wake.

2. Kujidai kwa Anania na Safira. Kanisa katika Yerusalemu lilikuwa imara pamoja na kuwa na changamoto. Luka aliandika, "Na jamii ya watu walioamini walikuwa na moyo mmoja na roho moja; wala hapana mmoja aliyesema ya kuwa kitu cho chote alicho nacho ni mali yake mwenyewe; bali walikuwa na vitu vyote shirika." (Mdo 4:32). Barnaba alionesha kielelezo kizuri (Mdo 4:36-37). Anania na Safira walionesha kwamba ndani ya kanisa kulikuwa na chembe za wapenda mali (Mdo 5:1-11). Petro alimwambia Safira kabla hajafa, "Petro akamwambia, Imekuwaje hata mkapatana kumjaribu Roho wa Bwana? Angalia, miguu yao waliomzika mumeo ipo mlangoni, nao watakuchukua nje wewe nawe." (Mdo 5:9). Wanaonesha uongofu uliobadilika kuwa tamaa.

**3. Ulimwengu wa sasa aupendao Dema.** Paulo alikuwa na mshirika ambaye alitajwa miungoni mwa waaminifu katika kazi. Paulo aliwaandikia wapendwa wa Kolosai, ***"Luka, Yule tabibu mpendwa, na Dema, wanawasalimu."*** (Wakolosai 4:14). Alimwandikia Filemoni, ***"na Marko, na Aristarko, na Dema, na Luka, watendao kazi pamoja nami."*** (Filemoni 1:24). Hata hivyo, Paulo baadaye alimwandikia Timotheo, ***"Maana Dema aliniacha, akiupenda ulimwengu huu wa sasa, akasafiri kwenda Thesalonike; Kreske amekwenda Galatia; Tito amekwenda Dalmatia."*** (2 Timotheo 4:10). Hilo ndilo jambo la mwisho kuzungumziwa kuhusu yeye katika Agano Jipya. Ni wazo linalosikitisha kuwatafakuri wale ambao walianza kwa bidii kwa ajili ya Bwana, ili tu warudi tena katika ulimwengu wa

dhambi na huzuni. Daima itakuwa ni muhimu kukumbuka kwamba sio tu hivyo kuhusu jinsi mtu anavyoanza.

**Jimmy Clark anahubiri katika Kanisa la Kristo Bethel huko Athens, Alabama, Marekani**

***“Angalieni, ndugu zangu, usiwe katika mmoja wenu moyo mbovu wa kutokuamini, kwa kujitenga na Mungu aliye hai. Lakini mwonyane kila siku, maadamu iitwapo leo; ili mmoja wenu asifanywe mgumu kwa udanganyifu wa dhambi.”***

***(Waebrania 3:12,13. Angalia pia, Waebrania 4:11; Marko 14:38).***

# Stefano

**Jack Harriman**

Stefano alikuwa mmoja wa wanaume saba waliochaguliwa kuhudumia kundi maalumu la wajane ambao walikuwa wakibaguliwa. Akawa mtenda miujiza mwenye nguvu, na mtetezi wa imani. Tunamkumbuka vizuri zaidi kama Mkristo wa kwanza kufa kwa ajili ya imani. Taarifa yake imeelezwa katika Matendo ya mitume 6 – 7.

Kwa muda mfupi tu niliona ukuu wa mtu huyu kama Luka alivyomwakilisha katika Mdo 6. Alizungumziwa kuwa ni mtu aliyejaa imani (5), Roho Mtakatifu (5), hekima (3,10), neema (8), nguvu (8), na nuru (15). Kutoka Mdo 7, sifa tatu zaidi zinaweza kuongezwa. Alijaa Maandiko, ujasiri, na upendo.

Alexander Whyte alisema kuhuseu Stefano, "Kupigwa kwa mawe kwa Stefano kulikuwa na upotevu kwa kanisa mtume mwingine Paulo. Stefano alikuwa kijana mdogo wa aina halisi madhubuti na neema hiyo maalumu, hakukuwa na kitu ambacho asingeweza kukipata kumruhusu



kuishi. Akili yake nzuri iliyofunguka, uhuru wake mkamilifu kutoka chuki zote zisizo na sababu na ushirikina wote wa wakati wake; ujasiri wake; ufasaha wake; utu wake usio na doa; pamoja na uzuri fulani, na kwa wakati huo huo fahari, namna; kwa pamoja vinamweka Stefano katika daraja la mbele sana, yote mawili la huduma na la hatarishi. Katika mambo haya yote, na hususani katika

uwazi, ukaribishaji, na upevu wa akili yake, Stefano amewazidi hata mitume ambao ni nguzo kama Petro na Yakobo na Yohana…haya yote yalimfanya Stefano kuwa mtu wa daraja la juu kwa wakati wake, na, kama matokeo, mtu wa kwanza kupigwa na kuangushwa.”

**Jack Harriman ni mhubiri wa Injili anaishi Fayetteville, Arkansas, Marekani**

# Epafra, Mtumwa wa Yesu Kristo

**Harvey Porter**

Paulo alihitimisha nyaraka zake nyingi kwa kuwataja wale ambao walikuwa wakifanya kazi pamoja naye katika kuueneza Ukristo. Maranyingi sana alitoa maelezo kuhusu wao na kwa nini wao pia walikuwa wapendwa kwa kanisa au mmoja mmoja aliyekuwa akimwandikia.

Wakati Paulo alipoliandikia kanisa la Kolosai, alifunga kwa kusema, ***"Epafra, aliye mtu wa kwenu, mtumwa wa Yesu Kristo, awasalimu, akifanya bidii siku zote kwa ajili yenu katika maombi yake, ili kwamba msimame wakamilifu na kuthibitika sana katika mapenzi yote ya Mungu. Maana namshuhudia kwamba ana juhudi nyingi kwa ajili yenu, na kwa ajili ya hao walioko Laodikia, na kwa ajili ya hao walioko Hierapoli."*** (Wakolosai 4:12,13).

Epafra alielezewa na Paulo kwenye Wakolosai kama ***"mtu wa kwenu".*** Hili lilikuwa kusanyiko lake la nyumbani. Si tu kwamba, alijulikana sana kwa Wakristo wenzake wa Laodikia na Hierapoli, miji miwili iliyokuwa karibu na Epafra "alituma salamu." Walikuwa na maana sana kwake, na yeye pia kwao. Ni jambo la kupendeza kupendwa na kanisa zima, na katika upande mwingine kulipenda kanisa hilo.

Kwa kweli, Epafra alilipenda kanisa lile sana hivyo alikuwa akiomba wakati wote. Paulo alisema, ***"…akifanya bidii siku zote kwa ajili yenu katika maombi yake,..".*** neno "bidii" linatukumbusha kuwa Yakobo alishindana na malaika wakati akiwa katika maombi. Neno letu la Kiingereza "agony" (maumivu makali/masumbuko makubwa), linatokea katika neno hili la Kigiriki. Linamaanisha kufanya kazi ya kutaabisha kwa bidii, hata

kufikia hatua ya kuchoka sana. Ungependa kuwa na mtu mwenye haiba ya Kikristo kama Epafra anayeomba kwa ajili yako kila wakati?

Maombi yake hayakuwa kwa ajili ya chakula, nguo, hata kwa ajili ya afya ya kimwili, au kwa ajili ya pesa. Maombi yake kwa ajili yao yalikuwa kwamba waweze ***"…msimame wakamilifu na kuthibitika sana katika mapenzi yote ya Mungu."*** Hivyo ndivyo sisi sote itupasavyo kuomba kwa ajili ya kanisa tunalolipenda. Tungekuwa kanisa la namna gani kama kila mtu angesimama mkamilifu katika mapenzi yote ya Mungu. Msingekuwa na washirika wowote vuguvugu. Hakuna mtu ambaye angeshuka au ***"kuacha kukusanyika".*** Kanisa la leo linahitaji sana ***"kusimama kikamilifu katika mapenzi yote ya Mungu".***

Epafra alitaka wote aliowajua wawe "wamekomaa". Sote tunakubaliana na maombi hayo. Kanisa linahitaji Wakristo waliokomaa vya kutosha na kuacha tofauti za vitu vidogo vidogo, imara wa kutosha kuwapenda wale ambao tunatofautiana, na kuvumilia vya kutosha kutatua matatizo yote. Wakristo wakomavu kamwe hawaachi, kukata tamaa, au kukoma kuhudumu. Bwana siku zote anaweza kuwategemea, kwa maana daima wanapatikana.

Epafra aliomba kwamba waweze ***"…kuthibitika sana katika mapenzi yote ya Mungu".*** Mtoa maoni alisema, "wazo ni umakini wa utiifu ambao unashikilia utakatifu kwa kila maelezo ya maagizo ya Bwana." Chrysostom aliandika, "Haitoshi tu, kufanya mapenzi yake. Yeye ambaye amejaa,

**Wacha sote "tufanye bidii katika kuomba" kwa ajili ya ndugu zetu wa kiume na wa kike katika kanisa ambalo sisi ni sehemu yake. Kwa njia hii tunaweza kuwa "watumwa wa Yesu Kristo", kama alivyokuwa Epafra.**

wala hajisumbui kwa mapenzi mengine yoyote kuwa ndani yake, kwa maana ikiwa hivyo, basi hakujazwa kikamilifu." Mapenzi yote ya Mungu yanatosha kwa maisha yetu, hatuhitaji zaidi. Kwa hiyo, tunaomba pamoja na Yesu, ***"Si mapenzi yangu, bali mapenzi yako yatimizwe".***

Hakuna shaka kwamba Epafra lazima aliwapenda wale Wakristo, kwa sababu aliomba kwa bidii sana kwa ajili yao na kumwomba Bwana awabariki ***"…wasimame wakamilifu na kuthibitika sana katika mapenzi yote ya Mungu".*** Ni maombi mazuri kiasi gani! Inachukua maisha yetu yote ya Ukristo katika maneno machache. Ni maombi ambayo tunalazimika kuyaomba kwa ajili ya kusanyiko tunapoabudia leo. Mahitaji yetu ni sawa na yale ya Wakristo wa siku nyingi zilizopita. Mungu wetu na Bwana wetu Yesu ni walewale na wanataka kutubariki kama walivyofanya wakati ule. Kwa hiyo, sisi sote tuwe tuwezavyo kuwa "***watumwa wa Yesu Kristo",*** kama Epafra alivyokuwa.

**Harvey Porter (1929-1998) alihubiri kwa miaka mingi huko Albuquerque, New Mexico, Marekani**

# Vipi kuhusu Gharika?

**Dennis Gulledge**



**“Je, Gharika katika siku za Nuhu ilikuwa sehemu tu au ulimwengu mzima?”**

Ilikuwa ni gharika ya ulimwengu mzima. Biblia inasema, “*Na tazama, nitaleta gharika ya maji juu ya nchi, niharibu kila kitu chenye mwili na pumzi ya uhai, kisiwepo chini ya mbingu; kila kilichoko duniani kitakufa.”* (Mwanzo 6:17). *“Maji yakapata nguvu sana sana juu ya nchi; na milima mirefu yote iliyokuwako chini ya mbingu ikafunikizwa.”* (Mwanzo 7:19). *“ Kila kilicho hai juu ya uso wa nchi kikafutiliwa mbali tangu mwanadamu hata mnyama wa kufugwa, na kitambaacho, na ndege wa angani; vilifutiliwa mbali katika nchi, akabaki Nuhu tu, na hao walio pamoja naye katika safina.”* (Mwanzo 7:23). Petro aliandika, “*kwa hayo dunia ile ya wakati ule iligharikishwa na maji, ikaangamia.”* (2 Petro 3:6).

Wazo la gharika kuwa ya sehemu fulani katika Asia magharibi linaleta matatizo magumu. Kama gharika ilikuwa sehemu fulani, kwanini ilikuwa ni muhimu kutengeneza meli ya ukubwa wa safina? Kwanini wasingeenda kwenye milima? Wanyama kwa silika huenda katika kilele cha mlima kwenye hali ya mafuriko. Kwao kupona kungekuwa rahisi. Ndege wangeweza kuruka hadi kwenye maeneo makavu. Haiwezekani kuiamini Biblia na wakati huo huo kukubali wazo la gharika iliyokuwa na mpaka na sehemu fulani.

**Dennis Gulledge ni mhubiri wa kanisa la Kristo huko Mabelvale, Arkansas, Marekani**

# Mfano wa Ubatizo unaumuhimu gani?

**Charles R. Rose**

Wengi wa majirani zetu wa kidini watakwambia kwamba ubatizo si lazima linapokuja suala la wokovu wa roho. Hata hivyo, ili kuwa mshirika wa makanisa yao ni lazima mtu abatizwe. Mwandishi fulani mwenye hekima alitoa maoni yake miaka mingi iliyopita kwamba, "ni rahisi kuingia mbinguni kuliko kuingia katika makanisa mengi leo." Kwa kusemwa hivyo, bado, mashirika mengi ya kidini wanatenda na wanataka aina fulani ya ubatizo katika mafundisho yao, iwe ni kwa ajili ya wokovu, au "kujiunga" katika kanisa lao. Baadhi wanafanya tendo la "kunyunyiza" pale ambapo mtumishi au kuhani (padre) atanyunyiza maji kidogo juu yake mpokeaji. Wengine watachukua chombo kidogo chenye maji na "kukimimina" juu ya kichwa cha anayebatizwa. Bado wengine wanafanya "kuzamisha" kwa ajili ya ubatizo. Kati ya haya matatu, upi ulifundishwa na kuhubiriwa na Yesu Kristo na mitume wake waliovuviwa? Je, kweli hili linajalisha?

*Funk & Wagnall's Standard Desk Dictionary* inafafanua neno "batiza" kwa njia hii. "Kuzamisha katika maji au kunyunyiza maji juu ya Mkristo katika ubatizo." Kwa kutambua hilo Agano Jipya liliandikwa kwa Kigiriki, mtu anapaswa kutafuta kwa wasomi wa Kigiriki kuona ni ukweli gani Mungu aliomaanisha katika Neno lake Takatifu. Wanafunzi wake waliwabatizaje waongofu katika nyakati za Agano Jipya? Tafadhali zingatia maneno yafuatayo kutoka katika Kigiriki.

- "Nyunyiza" limetafsiriwa katika Kiingereza kutoka katika neno la Kigiriki "rantizo".
- "Mimina" linatokea katika neno la Kigiriki "cheo".
- "Zamisha" limechukuliwa kutoka katika neno la Kigiriki "baptizo".

Lipi limetumika katika Biblia? Tafadhali soma kutoka katika Biblia yako mwenyewe vifungu hivi vifuatavyo. Wakati Yesu alipokuwa akibatizwa, ***"…akapanda kutoka majini;.."*** (Mathayo 3:13-17). ***"Yohana naye alikuwa akibatiza huko Ainoni,..kwa sababu huko kulikuwa na maji tele;.."*** (Yohana 3:23). Wote wawili Filipo na towashi ***"…wakatelemka wote wawili majini, Filipo na yule towashi, naye akambatiza. Kisha walipopanda kutoka majini…"*** (Mdo 8:36-39). *"**Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima.*** (Warumi 6:3-4).

Upi kati ya mifano hii iliyoandikwa ulikuwa kunyunyiza au tendo la kumimina? Ni lazima kukili kwamba katika "kunyunyiza" au "kumimina", haichukui "maji mengi" kama katika Yohana 3:23, wala kuhitaji kutelemka chini na kupanda juu nje ya maji kama katika ubatizo wa Bwana wetu Yesu Kristo na towashi (Mathayo 3:16; Mdo 8:38). Wala mtu kwa huaminifu na ukweli (hawezi) kusema kwamba amezikwa (Warumi 6:3,4) kwa kunyunyizwa au kwa kitendo cha kumiminiwa maji.

Mtu anaweza kuviendea vitabu vya historia na kusoma maoni ya viongozi wa kidini ambao walikuwa ni mababa waanzilishi wa madhehebu yetu ya leo ambayo leo wanafanya unyunyizaji au umiminaji kuona kwamba viongozi hao wa kidini hawakuamini kama wafuasi wao wanavyofanya leo.



- **John Calvin (Presbyterian)** alisema, "Neno 'batiza' linaashiria kuzamisha. Bila shaka uzamishaji huo ulikuwa ni kitendo cha kanisa la kishamba."

- ***Martin* Luther (Lutheran)** alitoa maoni, "Ubatizo ni neno la Kigiriki, na linaweza kutafsiriwa, kuzamisha. Naweza kusema wale waliobatizwa wote walitumbukizwa."
- **John Wesley (Methodist)** alisema. "Kuzikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo – kunadokeza njia ya kale ya kubatiza kwa kuzamisha."

Hili linajarisha? Tafadhali angalia kwenye Biblia yako mwenyewe kwamba ubatizo katika Agano Jipya ulikuwa ***"kwa ajili ya ondoleo la dhambi"*** (Mdo 2:38), ***"kuosha dhambi"*** (Mdo 22:16), kwa ajili ya wokovo (1 Petro 3:21), na kumweka mtu ndani ya Kristo Yesu (Wagalitia 3:26,27; Warumi 6:3,4).

**Charles R. Rose ni mhubiri wa kanisa la Kristo huko Lincoln, Missouri, Marekani.**

# Wanikolai, Walikuwa Akina nani?

**Mike Riley**

Katika Ufunuo 2:6,15, tunasoma kuhusu "matendo" na "fundisho" la Wanikolai. Wanikolai walikuwa akina nani, matendo yao yalikuwaje, na fundisho lao lilikuwaje?



Neno, "Wanikolai" linamaanisha "uhaRibifu wa watu". Walikuwa ni madhehebu au chama chenye ushawishi wa uovu katika Ukristo wa awali, hususani katika makanisa saba ya Asia (Ufunuo 1:11). Fundisho lao potofu lilikuwa sawa na la Balaamu, ***"yeye aliyemfundisha Balaki atie ukwazo mbele ya Waisraeli, kwamba wavile vitu vilivyotolewa sadaka kwa sanamu, na kuzini."*** (Ufunuo 2:14,15; Hesabu 22-25; 2 Petro 2:15,16; Yuda 1:11). Nia yao haikuwa tu kufanya mambo mabaya ya mataifa. Kwa kupitia upinzani wa moja kwa moja dhidi ya agizo la kanisa lililotolewa katika Mdo 15:20,29, bali pia walijihusisha katika ulafi wa karamu za ibada ya sanamu. Inaonekana walileta vitu vichafu vya karamu hizo katika mikusanyiko ya awali ya kanisa la karne ya kwanza.wanatajwa kama manabii waongo katika 2 Petro 2:1.

Ingawa haijulikani sana kuhusiana na Wanikolai, tunajua kwamba kanisa la Efeso ***"walichukia matendo ya Wanikolai"*** (Ufunuo 2:6), na kanisa la Pergamo lilichukua upande wa maafikiano kwa fundisho lao potofu (Ufunuo 2:12-15). Kwa kukubali mafundisho ya Balaamu au Wanikolai lilikuwa ni jambo lililolaaniwa na Bwana wetu (Ufunuo 2:6,15,16). Kwa kweli, tendo la ibada yoyote ya sanamu linalaaniwa katika Biblia na linatakiwa kuepukwa kwa gharama yoyote (1 Samweli 15:23; 1 Wakorintho 10:14; Wagalatia 5:19-20; Waefeso 5:5; Wakolosai 3:5).

# Masomo Mazuri Kutoka kwa Ayubu

**Therman Hodge**



**I. Kitabu cha Ayubu kinatufundisha kwamba Shetani haachi katika juhudi zake za kukamata watu (1:7; 2:2).**

A. Petro anatuambia kwamba Shetani kila wakati anatafuta mtu wa kummeza (1 Petro 5:8).

B. Paulo anaashiria kuwa alijua Shetani aliajiri vyombo vingi tofauti kukatisha tamaa na kudhoofisha maendeleo ya kanisa (2 Wakorintho 2:11).

C. Shetani alituma mbwa-mwitu kutoka nje kuangamiza kundi la Mungu kwa mafundisho mapotofu na kuwaajiri hata baadhi ya viongozi wa kanisa wafundishe mafundisho mapotofu na kuwapeleka kondoo mbali na ukweli (Mdo 20:28-31); 2 Timotheo 4:3-5).

D. Pia alitumia mafarakano ndani ya makundi kwa waumini kuwafuata wanadamu badala ya Bwana (1 Wakorintho 1:10-13).

**II. Ayubu pia anatufundisha kwamba falsafa ya mwanadamu ina mapungufu (16:2-3).**

A. Nabii Yeremia anatuambia kwamba mwanadamu hana hekima ya kuongoza hatua zake mwenyewe (Yeremia 10:23).

B. Ni neno la Mungu ambalo linaweza kutufundisha kutenda matendo mema na kutuweka katika njia ya ukamilifu (1 Wakorintho 2:6-13; 2 Timotheo 3:16,17).
C. Kwa hiyo, Paulo angeweza kutuambia tuitupe chini hekima ya kibinadamu na kiburi (2 Wakorintho 10:5).

**III. Imani yote inapaswa kuwekwa kwa Mungu, kama Ayubu anavyoonesha kwa kina (42:1-6).**

A. Mwenye hekima wa kale pia anatuelekeza tumtegemee Mungu (Mithali 3:5-7).
B. Vivyo hivyo, Daudi, mwimbaji wa Israeli, anatuelekeza kwa Mungu kwa ajili ya kupata nguvu (Zaburi 33:8-12).
C. Si ajabu Paulo aliuliza swali lenye jibu, ***"kama Mungu akiwa upande wetu ni nani aliye kinyume chetu?"*** (Warumi 8:31).

**IV. Somo kuu katika Kitabu cha Ayubu ni kwamba maswali yote ya kutatanisha ya maisha yamejibiwa katika Yesu Kristo**

A. Ayubu alitamani kuwepo mwamuzi baina yake mwenyewe na Mungu (23:3; 9:33).
B. Tunajua kwamba Yesu anayo suluhu ya hitaji hilo (1 Timotheo 2:5; 1 Yohana 2:1; Waebrania 4:14-16).
C. Ayubu alistaajabu ikiwa kulikuwa na maisha baada ya kaburi (14:14).
D. Yesu alituonesha kwamba kuna ufufuo, kwa mafundisho yake na kwa kulishinda kaburi (Yohana 11:25,26; 14:1-6; 1 Wakorintho 15:1-26; Wakolosai 3:4).
E. Kama sisi sote, Ayubu alitamani sehemu ya amani (Mathayo 11:28-30; Waebrania 4:1-11).
F. Ni sehemu ambayo itatuweka huru mbali na wasiwasi wote wa maisha haya na huduma, huzuni na maumivu (Ufunuo 21:4-7).

**Therman Hodge ni mhubiri wa Injili na mmishonari wa muda mfupi katika nchi kadhaa. Anaishi huko Meridian, Mississippi, Marekani.**

# Kwenda Mbali (Wakolosai 1:23)

## Ken Tyler

**Utangulizi:** Inaumiza kusanyiko pale washirika wanapoondoka. Kuna aina nyingine ya kuondoka ambayo ni mbaya zaidi kwa kanisa. Tunapoondoka mbali na Yesu Kristo, tunaangamiza roho zetu na kuumiza kanisa. Zingatia maswali yafuatayo.

**I. Umeondoka mbali na ukweli wa Injili ya Yesu (Wagalatia 1:8,9; 2 Yohana 9-11)?**

- **A.** Mpango wa wokovu (Waebrania 11:6; Acts 17:30; Mdo 8:37; Mdo 2:38).
- **B.** Ibada (Yohana 4:23,24; Mdo 20:7; 1 Wakorintho 16:1,2; Waefeso 5:19; 1 Wathesalonike 5:17).
- **C.** Muundo wa kanisa (Wafilipi 1:1).

**II. Umeondoka mbali na upendo ambao Yesu alifundisha na kuuonesha (Mathayo 22:35-40; Luka 23:34)?**

- A. Upendo unamaasha tunazishika amri zake (1 Yohana 5:3).
- B. Upendo unamaanisha tunatekeleza Kanuni ya Dhahabu (Mathayo 7:12).
- C. Upendo unamaanisha tunasamehe (Mdo 7:60).
- D. Upendo unamaanisha tunawapenda maadui zetu (Mathayo 5:44,45).
- E. Upendo unamaanisha tunauonesha ulimwengu uwanafunzi wetu (Yohana 13:35).

**III. Umeondoka mbali na kanisa kuwa kipaumbele chako cha kwanza (Mathayo 6:22)?**

- A. Mahudhurio (Waebrania 10:25).
- B. Roho (Mdo 8:4; Wagalatia 6:1; Yakobo 5:19,20).

C. Kujenga (1 Wakorintho 14:12).
D. Kusali (Waebrania 13:18).
E. Kazi (1 Wakorintho 15:58).
F. Kutoa (Mithali 3:9,10).

**Hitimisho:** Hakuna kati yetu anayeweza kumudu kwenda mbali na kanisa. **Umekagua anuani yako hivi karibuni?**

**Ken Tyler anahubiri katika kanisa la Bwana huko Arab, Alabama, Marekani**

# Je, Marejesho ni Lengo la Kutamanika?

**D.Gene West**

Makanisa ya Kristo yaliyopo Amerika yenye zaidi ya miaka mia mbili yamekuwa yakijihusisha katika juhudi kubwa kwa kipindi chetu kulirejesha kanisa ambalo tunalisoma katika Agano Jipya. Wakati harakati hizi zilipoanza kwa kazi ya Stone, Campbell, Scott, Smith na mamia ya wengine, ilikuwa ikiaminika kwamba njia pekee ya kupatikana umoja wa kidini ingewezekana kwa watu kufanya mambo mawili. (1) Kurudi katika Biblia kwa yote tunayoyafanya katika mambo ya kidini. Thomas Campbell aliunda, katika njia yake ya kipekee, neno la kuchunga la harakati za awali ambalo lilikuwa, "Tunazungumza pale Maandiko yanapozungumza na tunanyamaza pale Maandiko yanaponyamaza." (Mtu fulani amesema hatuna tatizo katika kusema pale Maandiko yanaposema, lakini tatizo letu ni kuamua wakati yanapokuwa kimya. Kunaweza kuwa na ukweli fulani katika hilo). (2) Tunapaswa kujaribu kurejesha utaratibu na ibada ya kanisa kwa kitu kile kile ambacho kilikuwepo katika nyakati za mitume.

Inaonekana kwamba la kwanza kati ya haya kiasili linapelekea kwa la pili kama chochote kiwezavyo. Kwa mfano, kama Biblia inafundisha uzamishaji wa walioamini na kutubu kwa ajili ya ondoleo la dhambi na tukifanya kile tu ambacho kimefundishwa katika Biblia kuhusiana na njia ambayo mtu anaokolewa, basi hapo hakuna lingine bali ni kurejesha utaratibu wa mambo wa kale kwa kiwango kile. Tunaonesha zaidi kwa kusema kwamba ikiwa Maandiko yanafundisha kwamba kanisa la mitume liliweka katika mtindo wa kusanyiko wazee wengi wakichunga kila kundi moja la watu wa Mungu, na ikiwa tutafuata kile tu kinachoonekana katika Agano Jipya katika jambo hili, kihalisia tutarudisha utaratibu wa kale kwa ajili ya kanisa. Moja kati ya haya

mambo inaonekana kufuata lingine kwa hiyo kihalisia kiukweli hatuyafikirii kuwa na utengano.

Hili limeleta jambo kubwa la furaha miungoni mwa watu wa kidini ndani ya Amerika, na sehemu nyingine, lakini kwa wakati huo huo limetengeneza ushiriki wake wa huzuni. Au pengine tumetengeneza huzuni kwa kutokuzitumia kanuni zilizowekwa hapo juu. Katika siku za awali za watu wa harakati za marejesho walijikusanya katika mawazo haya, na ndani ya miaka michache idadi ya wale waliojiunga nao ilipanda hadi kukaribia milioni mbili.

Halafu shida ikaja! Watu wakitaka kufanya kazi ya umisionari kote nyumbani na ng'ambo kwa kutumia jamii zilizowekwa kwa lengo hilo kwamba zisiweze kudhibitiwa na makanisa. Watu waliamua kwamba tunapaswa kuongeza matumizi ya ala za muziki katika ibada zetu. Mfumo wa kichungaji uliwekwa katika namna ambayo mamlaka yanahamishwa kwa ajili ya ustawi wa makusanyiko kutoka katika mikono ya wazee (maaskofu au wachungaji) kwenda kwa wahubiri. Ndani ya miaka mia moja ya mwanzo wa hii biashara kubwa, maelfu waliondoka. Shida ilichanganywa na kila mkono miungoni mwa watakatifu. Utengano, huzuni, uchungu, huenda hata chuki ilifuata, na wachache tu kati ya mamilioni waliachwa wakisihi (kubaki) kwa ajili ya (katika) marejesho wa Ukristo wa Agano Jipya.

Wanafunzi wa Kristo hatimaye waliondoka na kutelekeza wazo la marejesho, wakati Kanisa lilikuwa tayari kurudi, (lakini) kwa kadiri walivyoweza kuabudu kulingana na tamaa zao, na kuratibu kulingana na tamaa zao walikuwa na utayari kujiita "tawi la harakati za marejesho". Makanisa ya Kristo pekee yalisimama peke yake katika jaribio hili mpaka robo ya karne ya mwisho. Sasa, wengi wanataka kuenenda katika njia ya Makanisa ya Kikristo kuhusiana na ibada na mambo mengine ya jinsi hiyo. Baadhi ya watu wetu, kwa shauku kuu wanauliza, "Hivi hili linatamanika hata kujaribu kurudisha Ukristo ambao tunasoma katika Agano Jipya?

,katika kujibu swali hili, tumechagua kuuliza maswali mfululizo. Kama tukiipa kisogo Biblia na Biblia pekee ndiyo mamlaka yetu katika

masuala ya dini, tutaendea chanzo kipi? Mmoja alisema, “Ah, hatushauri tuondokane na Biblia!” Bado, nini kingine tunachofanya wakati tunatelekeza mafundisho yake katika ibada au jambo lingine lolote?

Kama si jambo la kutamanika kurudisha utaratibu ambao ni sahihi unaopatikana katika Agano Jipya, tutageukia kitu gani? Tutawageukia viongozi wa marejesho, nyuma katika siku za awali za Kanisa Katoliki la Kirumi, au kwa Orthodox Mashariki? Tutaipa kisogo Biblia na kufanya chochote tunachokiona kuwa ni kizuri? Tutamwendea nani, kwa maana Bwana pekee ndiye mwenye maneno ya uzima wa milele (Yohana 6:68)? Wacha tuendelee kupambana! Hatuna sehemu nyingine ya kugeukia! Hakuna chochote kilicho bora huko nje!

**D.Gene West ni mhubiri wa Injili na mwalimu wa Shule ya Mahubiri West Virginia huko Moundsville, West Virginia, Marekani.**